# Nipashe

Ijumaa Agosti 2, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579986

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Waziri aonya ubaguzi utoaji vitambulisho Nida, Uhamiaji

UKURASA 3


Ukurasa 16

Hifadhi yenye mbega weupe, weusi na panzi wenye bendera ya taifa

Ukurasa 20

Brela yaeleza itakavyotinga Nanenane Simiyu na ajenda ya usajili kidigitali

BUFE

Ijumaa Agosti 2, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Maisha mapya ya 'Panya Road' mstaafu, Polisi sasa wateja wake

Ukurasa 15

Safari mpya SADC kuibua Utalii wa Ukombozi nchini

Na Judith Mhina, MAELEZO

SERIKALI tangu katika zama za uongozi wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, ilijitoa mhanga kupokea, kuwahudumia, kuwahifadhi na kuwasaidia kwa hali na mali wapigania uhuru wa nchi nyingi duniani hasa hasa wa ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Mwalimu Nyerere katika moja na nukuu zake aliwahi kutamka: "Uhuru wa Tanzania hautakuwa na maana yeyote kama nchi zinazotuzunguka na binadamu wenzetu popote pale duniani hawako huru".

INAENDELEA UK.18

UCHUMI

Habari katika picha

Ukurasa 17

Fursa nyingine ya SADC Dar kupitia haki makini ya kijinsia Ukurasa 14

UKURASA 13

# Saratani hatari kwa wasionyonyesha

- **Watoto** 20,000 hawapati maziwa ya mama, wasichana wadaiwa kutunza 'saa sita', waziri atoa neno... *Endelea ukurasa wa 2*




Rais John Magufuli akikata utepe kuashiria ufunguzi rasmi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni mkewe Mama Janeth, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika Job Ndugai, Mufti wa Tanzania Sheikh Abubakar Zubeiry bin Ally, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam Muadhama Polycarp Kardinali Pengo na viongozi wengine. **PICHA: IKULU**

## Sekta binafsi yapigiwa chapuo

UKURASA 2

## Spika Ndugai amkosha Magufuli utalii fukwe

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA SC SASA KIDIGITALI** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Sekta binafsi yatiliwa mkazo

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli amesema serikali inaipenda na inaithamini sekta binafsi kwa kuwa ndiyo injini ya uchumi wa nchi na inaongoza kwa kutoa ajira kwa wananchi.

Amesema kutokana na ukweli huo, serikali yake imefanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufuta kodi zaidi ya 54, kuhakikisha kunakuwa na umeme wa uhakika na ujenzi wa miundombinu ili kuwe na ustawi wa sekta hiyo.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana jiji Dar es Salaam alipozindua kiwanda cha kusaga nafaka cha 21st Century Food and Packing kinachomilikiwa na Kampuni ya Mohamed Enterprises.

"Nawaambia kwa dhati kabisa serikali hii ipo kwa ajili ya wawekezaji, serikali hii ipo kwa ajili ya sekta binafsi, nchi yoyote haiwezi kusonga bila sekta binafsi, nchi yoyote haiwezi kufanya biashara, biashara inafanywa na sekta binafsi.

"Sekta binafsi lazima iwe makini katika kufanya mambo yake. Kwa mfano, mliojiari hapa 380 wasingekuwa wamepata ajira ndani ya serikali, mwajiri mkubwa wa Watanzania ni sekta binafsi, haiwezi kuwa serikali, serikali haina uwezo wa kumwajiri kila mtu, tuko milioni 55, lakini ni sekta binafsi ndiyo inaweza kuajiri watu wengi.

"Nimefurahi kumwona Balozi wa Uingereza nchini, kwao umeme wanauza uniti moja senti 0.1, Marekani ni senti 0.12, nafikiri India ni senti 6.8, sisi hapa ni senti 11 hadi 12. Kwa hiyo, bidhaa unayoitengeneza hapa haiwezi kushindana kwa kuwa gharama yake inakuwa ni kubwa.

"Ukishakuwa na umeme ambao ni bei rahisi unaozalishwa kwa maji, ndiyo njia pekee ya kuuza bei rahisi na itaonekana kwenye viwanda ambavyo vitazalisha bidhaa ambazo ni rahisi na walaji watanunua kwa bei rahisi, ushindani utakwenda sawa na hiyo ndiyo nia ya serikali," alisema.

Aliongeza kuwa faida iliyopo kwa Tanzania ni kuwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ina watu milioni 165 na ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo ina watu zaidi ya milioni 400.

Aliwataka Watanzania na wawekezaji kutoka nje kuwekeza kwenye viwanda kwa kuwa ndiyo wakati sahihi.

"Ndiyo maana nasema ndugu zangu wawekezaji wa ndani na nje 'this is time' (huu ndiyo wakati) kwa sababu tuna uhakika na soko, na ndiyo maana nakupongeza sana Mohamed Dewji, wewe songa mbele, chapa kazi, wala usiwe mnyonge, wewe chapa kazi.

"Tanzania iko pamoja na wawekezaji wanaoanzisha viwanda, kazi unayoifanya (Dewji) ni nzuri sana," alisema.

Rais Magufuli pia aliwataka watendaji wa serikali kuacha kuwasumbua na kuwakatisha tamaa wafanyabiashara wanaotaka kuwekeza nchini.

"Nimepata taarifa kuna baadhi ya wawekezaji wanataka kuwekeza wa

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, akisajili simu yake kwa alama za vidole alipotembelewa na maofisa wa kampuni ya Vodacom, ofisini kwake, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ABOUBAKARY LIONGO**

# Wasionyonyesha hatarini kukumbwa na saratani

**Na Augusta Njoji,**

DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema wanawake wanaokataa kunyonyesha watoto wakidai kuwa matiti yao yataharibika wapo katika hatari kubwa ya kupata saratani ya matiti.

Pia ametishia kufuta likizo ya uzazi ya siku tano kwa wanaume kwa madai kuwa wengi wao wanaishia baa na vijiweni badala ya kuhudumia mama anapojifungua.

Waziri Ummy alitoa kauli hiyo jana, jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Wiki ya Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama ambayo kwa mwaka huu kaulimbiu yake ni: 'Wawezeshe wazazi, kufanikisha unyonyeshaji', iliyoandaliwa na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef).

Alitaka elimu zaidi itolewe kwa wanawake ambao hawataki kunyonyesha watoto kwa madai kuwa matiti yao yanaharibika jambo ambalo si kweli na linawaweka katika hatari ya kupata saratani.

"Kuna watu wanaogopa wanadai kuwa wanachakaa hasa visichana vya siku hizi dhana hii si sahihi, matiti yakiharibika kuna blazia sasa, kipi bora kuharibika au kupata saratani, kuna watu wananyonyesha watoto 10, lakini matiti ni saa sita," alisema.

Alisema mtu akinyonyesha anajiepusha kupata saratani na kupata mimba muda mfupi baada ya kujifungua.

"Hali ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama imepungua kwa asilimia moja, visichana vya sasa hivi asilimia moja havitaki kunyonyesha, kwa kila watoto 100 wanaozaliwa 97 wananyonyeshwa. Awali walikuwa 98 sawa na watoto 20,000 wanaozaliwa hawanyonyeshwi," alisema.

Kuhusu likizo ya wanaume, alisema kama hazileti matokeo yanayotakiwa atafuta na wala hatishii.

"Baba anapewa siku tano haonekani nyumbani, unatoka asubuhi unarudi saa nane za usiku sasa umesaidia kitu gani, sio kwamba natishia nipo serious (namaanisha), mnatakiwa kumsaidia na kumwezesha mke wako kunyonyesha na sio kukaa baa na

INAENDELEA UK. 8

# Ndugai amkosha JPM utalii wa fukwe

**Salome Kitomari na Gidion Msabula (Tudarco)**

RAIS John Magufuli ameunga mkono wazo la Spika Job Ndugai la kutaka maboresho kwenye fukwe nchini ili zitumike kwa ajili ya utalii.

Akizungumza baada ya kupewa nafasi na Rais Magufuli kutoa salamu za Bunge wakati wa uzinduzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Terminal III jijini Dar es Salaam, Spika Ndugai alisema kuna haja ya kuboresha utalii wa fukwe.

Alisema wageni wengi wanatembelea nchi jirani na Tanzania, wanatalii fukwe zilizoko Bahari ya Hindi kuanzia Mombasa, Malindi, Watamu na Lamu ambako kote kuna hoteli za kitalii.

Alisema Tanzania ina hifadhi nzuri ya mwambao wa Bahari ambao ni mzuri na mkubwa kuliko nchi yoyote Afrika.

"Tanzania tuna hifadhi za mwambao wa Pwani kuanzia Pangani hadi Mtwara, hazijatumika vizuri kwa sababu zipo Wizara ya Mifugo.

"Utalii wake hauonekani vizuri, zikipangwa vizuri ndani ya serikali, zikaunganishwa na utalii wa Pwani na Bara, watalii watakuwa mara mbili," Spika Ndugai alisema.

Katika hotuba yake, Rais Magufuli aliunga mkono hoja hiyo ya Spika, akieleza kuwa fukwe hizo ni muhimu kwa utalii na uchumi na kwamba uwanja huo utumike vyema kutangaza hifadhi za taifa na vivutio vyote vya utalii nchini.

"La Mheshimiwa Spika ambalo amelichomekea hapa, mimi naona ni la msingi, ni jukumu la wizara kukaa chini ya uongozi wa Waziri Mkuu kulijadili kuangalia namna gani fukwe kutoka Moa hadi Msimbati zaidi ya kilomita 1,422 zitatumikaje kuboresha uchumi na utalii," alisema.

**AKUMBUSHA PUSH UP**

Katika hatua nyingine, Raia Magufuli jana aliwafurahisha wananchi waliohudhuria hafla hiyo baada ya kushiriki kupiga 'push up' zilizokuwa zinafanywa na wasanii watatu wa bendi ya TOT waliokuwa wakitumbuiza.

Baada ya viongozi mbalimbali kushuka jukwaa kuu na kuwapongeza watoa burudani hao, Rais Magufuli naye alishuka na kuungana naye kukumbushia kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mwezi Agosti hadi Oktoba mwaka 2015, akiwa mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Rais Magufuli na wapambe wake walikuwa wakitumia mtindo huo wa 'push up'.

## HABARI KITAIFA

# Waziri akemea ubaguzi utoaji hati, vitambulisho

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amesema kuna sauti kwenye mitandao ya kijamii zikielezea kuhusu ubaguzi unaofanywa katika utoaji wa hati za kusafiria na vitambulisho vya taifa.

Kutokana na madai hayo, Masauni amewataka watumishi wa Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuwahudumia wananchi walioiweka serikali madarakani ili kuepuka baadhi ya mbinu zinazotumiwa na watu wasio na nia njema kuvuruga amani ya nchi.

Masauni aliyasema hayo jana baada ya kutembelea Makao Makuu ya Uhamiaji Zanzibar na kukagua utolewaji vitambulisho vya taifa na ubadilishaji wa hati za kusafiria.

Naibu Waziri huyo alitoa kauli hiyo baada ya kupokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi waliofika kwenye ofisi hizo kwa ajili ya kupata huduma.

"Hizi sauti zinazotembea mitandaoni bado siamini kama kweli watumishi wetu mnafanya hivyo. Muhimu ninawataka mfanye kazi ya kuwahudumia wananchi bila ubaguzi," alisema. Masauni alisema hawawezi kuwa serikalini alafu wanashindwa kuwahudumia wananchi inavyopaswa na kutoa huduma za kibaguzi.

Abdallah Kheri Said, mkazi wa Vuga, visiwani humo akizungumza mbele ya Masauni, aliiomba wizara hiyo iongeze idadi ya watumishi kwenye ofisi hizo hasa kipindi hiki cha kukaribia mwisho wa kubadilisha hati za kusafiria ili kuondokana na foleni zisizo za lazima.

"Tangu asubuhi saa mbili tuko hapa na huduma zimekuwa zikienda taratibu sana, tunaomba kuwapo na uharaka wa kupata huduma. Wiki nzima tunakuja hapa lakini huduma haziridhishi, tunaomba watumishi waongezwe," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa NIDA, Hassan Hassan, alisema hadi ifikapo mwishoni mwa mwaka huu mamlaka inatarajia kusajili watu 8,36,000 kwa ajili ya vitambulisho vya taifa.

Alisema kuwa wanatarajia kuchukua Tanzania Bara mashine 15 za usajili wa vitambulisho vya Taifa ili kuweza kuwahudumia watu wengi zaidi kwa wakati mmoja na kupunguza foleni zisizo za lazima.

Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Johari Suluhu, alisema moja ya changamoto iliyopo ni kipato kwa raia waloezi ni kidogo ikilinganishwa na gharama ya kupata kibali cha kuishi ambacho hutolewa kwa Sh. milioni mbili.

# Waziri Jafo aagiza Takukuru kuchunguza ujenzi hospitali

**Na Idda Mushi,** MOROGORO



WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (pichani), ameiagiza Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufanya uchunguzi mara moja juu ya matumizi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na kuelekeza kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wake.

Akiwa Mvuha wilayani Morogoro Julai 11, mwaka huu, Jafo, alisema haiwezekani serikali ikatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, huku ujenzi wake ukishindwa kufanikishwa kwa wakati.

Jafo alihoji ni namna gani shilingi bilioni moja zimetumika kujenga jengo hilo bila kukamilika, huku mradi huo ukiwa haujafikia hatua nzuri huku fedha zilizobaki zikiwa ni Sh. milioni 400 pekee.

"Hii hali hairidhishi, Mkuu wa Mkoa (Dk. Kebwe Stephen Kebwe, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro) njoo uchunguze, huku kazi inaendelea, lakini ofisi yako fanya ije kuchunguza, ije kuchunguza haya makandokando yanayoendelea hapa Morogoro Vijijini, Takukuru waje kufanya kazi yao," alisema na kuongeza:

"Lakini hii Manpower (nguvu kazi) haitoshi kabisa kwa kazi kama hii, tunamuona fundi anaweka tofali hapa wakati sehemu zingine ziko idle (hazina watu), hapa ni ubabaishaji mkubwa, na hata ukiangalia hizo tofali zinazowekwa, huenda kwa sababu Jafo amesikika anakuja hapa ndio wengine wakaja site (eneo la ujenzi)."

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Kayombe Masoud Lyoba, alisema kuchelewa kukamilika kwa ujenzi huo kunatokana na mabadiliko ya hali ya hewa zaidi ya miezi miwili, ambapo wakati mwingine hali huwa sio nzuri wilayani humo, na kwamba tayari kila hitaji la samani za ukamilishaji wa jengo hilo lilishanunuliwa.

"Kama unavyoona pale vifaa vyote vipo tayari, mchanga, kokoto, tunachofanya ni kuvifaulisha (kuhamisha) taratibu kuvileta hapa eneo la site," alisema Mkurugenzi huyo, lakini Jafo akaonyesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi huo hasa kutokana na kubaini uchache wa mafundi na kumwagiza Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Stephen, kuunda timu ya kufanya uchunguzi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kibena Kingo, alisema Baraza la Halmashauri waliona mwenendo hauendi vizuri na kumwagiza Mkurugenzi huyo wa Halmashauri kumwandikia barua Mkuu wa Mkoa ili apeleke watu kwa ajili ya kufanya ukaguzi maalum wa ujenzi huo wa hospitali ya wilaya, Kituo cha Afya Duthumi na Kituo cha Afya cha Mkuyuni ambapo kazi zilikuwa zikiendelea.

Dk. Kebwe, alisema alishabaini upungufu kabla ya kuandikiwa barua ya maelekezo ya Baraza la Madiwani na kumtaka Ofisa Takukuru wa Mkoa kufuatilia matumizi ya fedha katika ujenzi wa hospitali hiyo.


NMB Close to you

Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

NMB BANK Plc ("NMB")
(Imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya kampuni ya Tanzania ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ya ukomo, cheti cha usajili namba 32699)

## TANGAZO KWA UMMA
## MATOKEO YA MAUZO YA TOLEO LA TATU LA PROGRAMU YA HATIFUNGANI YA MUDA WA KATI YA BENKI YA NMB PLC

Benki ya NMB ("NMB") inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 30 Mei 2019 Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ilitoa idhini kwa NMB kuuza toleo la tatu la programu ya hatifungani ya muda wa kati yenye thamani ya shilingi za kitanzania bilioni 25 ikiwa ni sehemu ya programu ya hatifungani ya NMB yenye jumla ya shilingi za kitanzania billioni 200.

**MATOKEO YA MAUZO YA TOLEO LA TATU LA HATIFUNGANI YA NMB**
Mauzo ya toleo la tatu la hatifungani ya benki ya NMB yalifunguliwa tarehe 10 Juni 2019 na kufungwa tarehe 8 Julai 2019, ambapo benki ya NMB ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi za kitanzania bilioni 83.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25 zilizotarajiwa kukusanywa.

**IDHINI YA KUONGEZA KIASI**
NMB imepata idhini kutoka kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kupokea maombi yote ya mauzo yenye jumla ya shilingi bilioni 83.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25 zilizotarajiwa kukusanywa, ikiwa ni mafanikio ya asilimia 333.

**MUHTASARI WA TOLEO LA TATU LA HATIFUNGANI YA NMB**
Muhtasari wa takwimu muhimu za ofa ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Mtoaji** | NMB Bank Plc |
| **Maelezo** | Programu ya hatifungani za muda wa kati za NMB |
| **Muda** | Miaka 3 |
| **Aina ya Hatifungani** | Daraja la kwanza, isiyokuwa na dhamana, kiwango cha riba kisichobadilika |
| **Toleo la** | 03 |
| **Namba ya Kumbukumbu** | NMB-FXD03/2019/03* |
| ** Ufafanuzi wa namba ya kumbukumbu: NMB – NMB Bank PLC; FXD03 – Hatifungani ya toleo la tatu lenye kiwango cha riba kisichobadilika; 2019 – mwaka wa kutolewa; 3 – muda wa hatifungani* | |
| **Tarehe ya Kutoa** | 15 Julai 2019 |
| **Jumla ya kiwango kilichotole-wa chenye marekebisho (TSH.)** | 25,000,000,000 (na ongezeko la hadi shilingi 58,349,190,000) |
| **Jumla ya mtaji uliokusanywa (TSH)** | 83,349,190,000 |
| **Kiwango cha matokeo (%)** | 333% |
| **Jumla ya kiasi kilichokubaliwa (TSH.)** | 83,349,190,000 |
| **Kiwango cha riba** | 10% kwa mwaka |
| **Bei ya Hatifungani** | Ni ile iliyotangazwa |
| **Kiwango cha chini** | Shilingi 500,000 (pamoja na nyongeza ya mafungu ya shilingi 10,000) |
| **Matumizi ya Mtaji uliopatikana** | Mtaji uliopatikana kupitia mauzo ya toleo hili zita-tumika kugharamia shughuli za maendeleo ya benki ya NMB, ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa kampuni ndogo na za kati za ujasiriamali (Small and Medium Enterprises - SMEs) pamoja na wawekezaji wadogo (Retail Investors) |

**SERA YA UGAWAJI**
Kutokana na maombi zaidi kupokelewa, Bodi
i. imeamua kutekeleza kiwango cha nyongeza kwa kuongeza kiwango cha ugawaji wa hatifungani kutoka shilingi 40,000,000,000 hadi shilingi 83,349,190,000; na
ii. imekubali maombi yote sahihi yaliyopokelewa. Waombaji wote watapokea asilimia mia (100%) ya maombi yao.

**MAELEZO YA ZIADA**
Endapo mwombaji wa Hatifungani atahitaji ufafanuzi, anashauriwa kuwasiliana na dalali wa soko la hisa au NMB kupitia nmbbond@nmbtz.com au +255 22 2322000 au Stanbic Bank Tanzania Limited, Msajili wa Hatifungani, kupitia nmbbond@stanbic.com.

**TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU**

Tafadhali angalia tarehe zilizopendekezwa kufuatia ufungaji wa ofa:

| Maelezo | Tarehe |
|---|---|
| Tarehe ya kutaarifiwa (kupitia baruapepe/ simu) | saa 8.00 mchana, Jumatano ya tarehe 31 Julai 2019 |
| Tarehe ya Malipo (kwa taasisi za uwekezaji zenye sifa tu) | saa 8.00 mchana, Jumatatu ya tarehe 15 Julai 2019 |
| Tarehe ya Kutoa | Jumatatu ya tarehe 15 Julai 2019 |
| Tarehe ya kuweka katika akaunti ya CDS | Alhamisi ya tarehe 01 Agosti 2019 au kabla ya tarehe hiyo |
| Tarehe ya kuorodhesha hatifungani kwenye soko la hisa | Ijumaa ya tarehe 02 Agosti 2019 |

**SHUKRANI**
Menejimenti ya benki ya NMB inatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote zilizofanikisha uuzwaji wa toleo la tatu la hatifungani ya NMB. Taasisi hizi ni pamoja na Bodi na Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Bodi na Uongozi wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam, Mshauri kiongozi wa benki ya NMB, Stanbic Bank Tanzania Limited na Dalali Mfadhili wa benki ya NMB, Orbit Securities Company Limited.

Imetolewa na:
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**NMB Bank PLC,**
**Barabara ya Ohio/Ali Hassan Mwinyi,**
**S.L.P 9213, Dar es salaam, Tanzania**

**TAREHE: 01 Agosti 2019**

215356902

www.nmbbank.co.tz

## Wakili wa serikali akwamisha kesi ya mkurugenzi wa OBC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imeshindwa kumsomea maelezo ya awali Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwindaji ya Oterlo Business Cooperation (OBC), Isack Mollel (59) na wenzake 10, kutokana na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Nuda Halili, kuugua.

Mollel anakabiliwa na mashtaka 37 yakiwamo ya kuajiri raia wa kigeni 37 kinyume na sheria za nchi za kutoa ajira kwa wageni.

Licha ya Mollel ambaye ni mshtakiwa wa kwanza, washtakiwa wengine ni Darweshi Jumma, Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, MartinCrasta, ImtiazFeyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali, ambao ni raia wa kigeni.

Kutokana na wakili hiyo kuugua, washtakiwa sasa watasomewa maelezo ya awali ya kufanya kazi nchini bila ya kuwa na vibali Agosti 7, mwaka huu.

Kesi hiyo ilitajwa jana kwa ajili ya watuhumiwa kusomewa maelezo ya awali, lakini Wakili wa Jamuhuri, Janeth Sekule, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Niku Mwakatobe, aliiomba mahakama kuahirisha kesi hiyo kwa kuwa wakili mwandamizi Halili aliyetakiwa kuwasomea maelezo hayo ni mgonjwa.

"Mheshimiwa Hakimu ni kweli kesi hii imekuja mahakamani hapa kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali, lakini kwa bahati mbaya Wakili Nuda ni mgonjwa, hivyo tunaomba tarehe nyingine ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Mwakatobe alihoji upande wa utetezi uliokuwa unawakilishwa na Daudi Haraka akisaidiwa na Goodlucky Peter iwapo wana pingamizi juu ya maombi hayo.

Akijibu hoja hiyo, Haraka aliiomba mahakama tarehe itakayopangwa ya kesi hiyo wateja wake wasomewe maelezo ya awali pamoja na kuanza kusikilizwa siku hiyo hiyo maana wamekaa siku nyingi.

"Mheshimiwa Hakimu hatuna pingamizi na hoja iliyowasilishwa ya upande wa Jamuhuri, lakini tunaomba kesi hii itakapokuja tena mahakamani hapa wateja wetu wasomewe maelezo ya awali pamoja na kuanza kusikilizwa siku hiyo hiyo kwa kuwa raia hawa wa kigeni wamekaa hotelini kwa muda mrefu na wanatumia gharama kubwa," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mwakatobe aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 7, mwaka huu na kusema iwapo upande wa jamhuri hautasoma maelezo ya awali, ataifuta kesi hiyo.

Kabla ya kusomewa mashtaka hayo, Mollel alifutiwa kesi namba moja ya mwaka huu iliyokuwa inamkabili ya kuajiri raia 10 wa kigeni kinyume cha sheria za ajira na kuunganishwa kwenye kesi namba 74 ya mwaka huu, inayowahusu washtakiwa kumi hao waliokamatwa eneo la Loliondo kwa kosa la kufanya kazi bila vibali.

Licha ya kesi hiyo, pia Mollel anakabiliwa na kesi zingine mbili za uhujumu uchumi katika mahakama hiyo ambazo upelelezi wake haujakamilika.




Mchuuzi wa matunda akisubiri wateja katika kona ya Barabara ya Uhuru na Mtaa wa Sikukuu, jijini Dar es Salaam jana, bila ya kuyafunika kitendo ambacho ni hatari kwa afya ya walaji. **PICHA: JOHN BADI**

# Wamasai, Wasandawe kuvutia wageni SADC

**Na Beatrice Moses**

UTALII wa utamaduni ukiwamo wa Wamasai na Wasandawe umetajwa kuwa miongoni mwa vivutio vinavyotarajiwa kuwavutia wageni kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Wageni hao wanaotarajiwa kuwasili nchini kuhudhuria Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi wanachama wa SADC ni pamoja na wakuu wa nchi 16 wa serikali hizo watakaoambatana na viongozi na maofisa waandamizi mbalimbali.

Akizungumza jana, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano Bodi ya Utalii ( TTB), Geofrey Tengeneza, alisema wamejiandaa vyema kuwavutia wanaohudhuria mkutano huo utakaofanyika jijini Dar es Salaam, kutembelea vivutio hivyo na vinginevyo ikiwamo mbuga za wanyama na Mlima Kilimanjaro.

Alisema kabila la Wamasai ni kivutio kutokana na utamaduni wao wa namna mbalimbali, ikiwamo kujitibu kwa tiba za jadi, makazi yao na mavazi.

"Utamaduni wa Wamasai ni kivutio hata kwa nchi za Sweden, Denmark na Canada, wamekuwa wakivutiwa na tamaduni za makabila hayo, hiyo inatokana na maisha na tiba zao za jadi zinatajwa kuwa ni za hakika kuliko za makabila mengine, pia mavazi yao yamekuwa ya pekee yanavutia kiasi cha baadhi ya watu kuwaiga,"

Tengeneza alisema. Alizungumzia pia kuhusu kabila la Wasandawe ambao wamekuwa na tamaduni za kuishi porini, kula matunda, hivyo kuonyesha kwamba kuna jadi na mila na desturi ambazo zimesimama kuwa za kipekee kwenye jamii.

Aliwasisitiza wananchi walio kando ya maeneo ya utalii kuhakikisha wanajipanga vizuri kuitumia fursa hiyo kwa kutumia kazi zao za mikopo za ubunifu na kuchora michoro ya viongozi wapambanaji wa nchi kadhaa za SADC ili waweze kupata soko.

Tengeneza alisema serikali imejipanga vyema ikitarajia pia miongoni mwa wageni wengi kutoka katika nchi hizo watatembelea maeneo ya nyumba walizoishi viongozi wao wapigania uhuru.

Tanzania ndiyo mwenyeji wa mkutano huo ambao umewahi kufanyika nchini miaka 16 tangu ufanyike nchini mwaka 2003, hivyo wito umetolewa kwa watu wa nyanja mbalimbali ikiwamo wajasiriamali na wafanyabiashara kuitumia vyema fursa hiyo.

Mkutano huo unatanguliwa na maonyesho ya Wiki ya Viwanda ya SADC, maadhimsho na maonyesho hayo yatafanyika kuanzia Agosti 5 hadi 8.

Awali, mwaka jana Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alikaririwa na vyombo kadhaa vya habari akiahidi kufikisha taarifa ya hatua ambayo Tanzania imefikia katika harakati za kutafiti na kuhifadhi kumbukumbu za ukombozi wa Bara la Afrika. Taarifa hizo ziliandaliwa kufikishwa kwa mawaziri wa utamaduni wa nchi za Kusini mwa Afrika ili nchi hizo wanachama ziweze kuchangia katika ujenzi wa kituo cha kuhifadhi kumbukumbu hizo.

# MOI yaanza matibabu ya mifupa mikoa ya kusini

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), imeanza kutoa huduma za matibabu ya kibingwa za mifupa kwa wakazi wa mikoa ya kusini katika Hospitali ya Nyangao, mkoani Lindi.

Lengo ni kuwapunguzia wananchi changamoto ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo jijini Dar es Salaam.

Huduma hizo zimeanza jana kufuatia mkataba wa ushirikiano uliosainiwa Julai 19, mwaka huu na Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, pamoja na Dk. Richard Jankiewics, ambaye aliuwakilisha uongozi wa Hospitali ya Nyangao Lindi.

Katika kambi hiyo ya wiki mbili, Daktari Bingwa wa Mifupa wa MOI, Bill Haonga, atafanya kliniki, upasuaji pamoja na kuwafundisha madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Nyangao.

Dk. Boniface alisema MOI imeanzisha huduma katika mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi kwa lengo la kuwapunguzia wananchi changamoto ya kusafiri umbali mrefu na kutumia gharama kubwa kufuata huduma MOI.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha huduma zetu zinawafikia wananchi katika ngazi zote za mikoa na wilaya, hivyo wananchi wa ukanda huu wa kusini wataanza kupata huduma za mifupa na madaktari bingwa wetu watakuwa wanakuja hapa wanatoa huduma kwa wananchi," Dk. Boniface alisema.

Alisema taasisi hiyo inatekeleza kwa vitendo agizo la serikali la kusogeza huduma za kibingwa kwa wananchi ipo kwenye mpango wa kusogeza huduma katika mikoa mingine ambayo inakabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa wa mifupa.

# JKCI yatibu wenye matatizo ya umeme wa moyo

**Na Joseph Mwendapole**

WAGONJWA 10 wenye matatizo ya umeme wa moyo ambao mapigo yake yanadunda haraka kuliko kawaida na wengine yaliyo chini ya asilimia 30, wamefanyiwa matibabu kwenye kambi maalum inayoendelea katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Matibabu ya moyo yanafanywa na madaktari bingwa wa magonjwa ya moyo wa JKCI kwa kushirikiana na wenzao wa shirika la Madaktari Afrika la Marekani.

Mkurugenzi wa Idara ya Magonjwa ya Moyo, Dk. Peter Kisenge, alisema hayo wakati alipozungumza na vyombo vya habari kuhusu umeme wa moyo.

Alisema kati ya wagonjwa 10 waliofanyiwa upasuaji katika kambi hiyo, wagonjwa wanne ambao mioyo yao ilikuwa imechoka na mapigo ya moyo kuwa chini ya asilimia 30 wamewekewa kifaa maalum cha kuongeza utendaji kazi wa moyo kijulikanacho kwa jina la kitaalamu la "Cardiac Resynchronization Therapy implantable cardioverter Defibrillator" (CRTD).

Dk. Kisenge aliongeza kuwa kwa mara ya kwanza JKCI imeanza kuziba maeneo ambayo yanapitisha umeme wa moyo kwa wingi na kuleta shida katika moyo kwa kutumia mashine maalum iliyotolewa hivi karibuni na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya matibabu ya moyo hapa nchini.

"Mashine hii ya Electrophysiology ina kazi ya kupima umeme wa moyo kama kuna mahali unapita bila kufuata njia ya kawaida pataonekana na baada ya hapo inatumika kuziba njia hizo," alisema.

Aliongeza kuwa tatizo hilo huwatokea zaidi wagonjwa wenye shinikizo la juu la moyo la muda mrefu, wagonjwa wanaopata mshtuko wa moyo na wenye hitilafu ya umeme wa moyo katika baadhi ya vyumba vya moyo," alisema Dk. Kisenge.

Daktari huyo bingwa wa magonjwa ya moyo alisema matibabu ya kuziba maeneo yanayopitisha umeme wa moyo bila kufuata njia yake awali hayakuwapo hapa nchini, hivyo kusababisha wagonjwa wenye shida hiyo kupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu.

Hata hivyo, alisema kuanzia Julai 22, mwaka huu matibabu hayo yalianza kutolewa hapa nchini.

Naye mtaalamu wa mashine ya kuchunguza, kutathmini na kutibu umeme wa moyo unaoenda kwa haraka (Electrophysiologist) kutoka Shirika la Madaktari Afrika la nchini Marekani, Profesa Mathew Sachest, alisema madaktari wa Afrika wamekuwa wakishirikiana na wa JKCI kwa kipindi cha miaka mitatu sasa.

# Diwani atupwa jela kumpiga makofi trafiki

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Mwanzo Mwandiga katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, Mkoa wa Kigoma imemhukumu Diwani wa Kata ya Mwanga Kaskazini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Clayton Revocatus (34) maarufu Baba Revo, kutumikia kifungo cha miezi mitano jela kwa kosa la kushambulia kwa kumpiga askari polisi Kikosi cha Usalama Barabarani.

Askari aliyefanyiwa kitendo hicho ni mwenye namba F 8350 Msafiri, aliyeshambuliwa kwa ngumi na makofi sehemu mbalimbali za mwili wake.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu wa Mahakama hiyo, Florence Ikorongo, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuwa na shaka yoyote.

Hakimu Ikorongo alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa viongozi wengine wenye tabia kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi watatu na kielelezo kimoja ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimshambulia askari kwa kumpiga ngumi na makofi sehemu mbalimbali za mwili wake.

Hakimu alisema ameangali ushahidi wa pande zote pamoja na washauri wawili wa mahakama, na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa pasipokuacha shaka yoyote.

Mshtakiwa huyo akijitetea jana mahakamani alisema: "Mimi ni Diwani wa Mwanga Kaskazini, ninawaongoza wananchi wengi, wananchi walinichagua endapo mahakama hii ikinifunga kifungo cha mwaka mmoja nitakuwa nimepoteza sifa ya kuwa diwani.

Hivyo basi kwa busara na kwa hekima kubwa, naomba mahakama hii itafute la kufanya ili kunusuru udiwani wangu pia utakuwa umewasaidia wananchi wa Mwanga Kaskazini, kwa sababu wana imani kubwa na diwani wao."

Alisema pia kwamba mahakama kwa kufanya hivyo, itakuwa imeipunguzia serikali gharama kwa sababu akifungwa mwaka mmoja jela, serikali itafanya uchaguzi katika kata yake ili kumpata diwani mwingine.

Aliiomba mahakama imuonee huruma kwa kuangalia namna ya kufanya kwa kuwa pia ana watoto wanne wanaomtegemea kwa chakula, shule, mavazi na mahitaji mengine, hivyo kuiomba mahakama impe onyo kali.

Hakimu Ikorongo alisema mahakama pamoja na washauri wa mahakama wameangalia kwa makini utetezi wa mshtakiwa huyo, lakini mahakama hii inajiuliza mshtakiwa huyo alipita kwenye taa nyekundu na askari aliingia barabarani ili kuwanusuru watembea kwa miguu ili wasigongwe.

"Chakushangaza mshtakiwa wakati alipita kwenye taa nyekundu akijua kuwa amefanya kosa, lakini akarudi tena na kuanza kumshambulia askari wa usalama barabarani hadharani kwa kumpiga ngumi na makofi, ambacho ni kitendo kibaya sana na wakati akijua yeye ni diwani," alisema Hakimu huyo.

Hakimu Ikorongo alisema pamoja na utetezi wa mshtakiwa huyo ni lazima mahakama hii itowe adhabu juu ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa viongozi wengine wenye tabia ya kuwapiga askari wakiwa kazini.

Alisema kitendo alichokifanya mshtakiwa ni kitendo cha makusudi kabisa haiwezekani kabisa diwani kama kiongozi wa wananchi kufanya kosa la usalama barabarani kisha kurudi kumshambulia askari wa usalama barabarani inaonyesha alikuwa amedhamilia kumpiga askari huyo makofi na ngumi.

Hakimu Ikorongo alisema kutokana na kitendo alichokifanya mshtakiwa huyu akiwa ni diwani ni kitendo cha ajabu kwa viongozi, hivyo basi mshtakiwa utakwenda jela miezi mitano ili akajifunze tabia ya kuishi na jamii.

WOMEN FUND TANZANIA
Empowering Local Women Heroes

## CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST TO PROVIDE COMMUNICATION AND MEDIA TECHNICAL SUPPORT SERVICES TO WFT

**1.0 BACKGROUND**

WFT was registered in Tanzania in 2008 as a non-profit organization and became operational in 2011. WFT is a growing women's rights fund and the first of its kind in the country WFT's overall goal is to contribute towards women's rights and empowerment, and to women's movement building through implementing a functional funding mechanism for women in Tanzania.

**2.0 THE CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST**

WFT is inviting firms and individuals with the requisite expertise to provide Communication and Media technical support on a yearly retainer basis. The firm or individual(s) will support WFT to develop and maintain a public presence in traditional electronic and social media platforms as well as support the advancement and/or refining of WFTs internal and external communications strategy. The key objective of this assignment is thus to assist WFT in its on- going processes towards strengthening its communication strategy to match its Strategic Plan and growth. During the assignment, the consultant will support the production of communication deliverables, event management and women rights advocacy campaigns.

**3.0 SCOPE OF THE CONSULTANCY**

In collaboration with WFT staff and specifically its Executive Director and Communications Speciality, main tasks of consultant will include:

**3.0.1 REVIEW OF THE EXISTING COMMUNICATION STRATEGY**

- To assess the current WFT Communication Strategy by identifying areas which need improvement and best communication practices, in support of WFT's vision, mission, goals and growth.
- Examine WFT's Strategic Plan and determine its communication requirements, including key areas of grants making and coalition building.
- Identify critical issues related to information, education and communication that would be required to strengthen women's rights, empower women's movements and raise awareness on sextortion's, HERstory and other matrixes.

**3.0.2 MEDIA RELATIONS**

- Organize and coordinate media engagements, visits, interviews, press conferences, press statements when required to do so)
- Write news stories, feature articles and special supplements on women activities and issues that retard their development such as gender based violence (GBV) and few oppressive laws and traditions.

**3.0.3 SOCIAL MEDIA FOOTPRINT**

- The social media is currently a major landscape that is used to educate, inform, challenges and inspire. The consultant should propose best ways to promote WFT and its coalition partners on using online media outreach, effectively and positively.

**3.0.4 EVENTS MANAGEMENT**

- To organize and ensure improved visibility of WFT and its coalition groups on timely/active participation of women's commemorations, community affairs, social responsibilities, fundraising, anniversaries, awards, seminars exhibitions and such events.
- Manage effectively public representations in gender festivals, launches, conferences, rallies and such programmes.

**3.0.5 BRANDING**

- Improve WFT's identify and branding through well printed brochures booklets, banners, billboard, profiles and other distribution materials.

**EXPECTED DELIVERABLES**

1. Review the existing communication strategy (2015 – 2019) and develop a new one for internal and external stakeholders (2020 – 2024)
2. Develop a media outreach plan to identify, build and maintain good relationships with a network of traditional, electronic and specialized media ( Journalists, broadcasters and social media editors)
3. Actively create media visibility opportunities for WFT and its coalition groups through production of informative articles, TV and radio interviews and other necessary media coverage that will create a positive image.
4. Assist in the production of WFT's online magazine (English and Kiswahili versions). The magazines (online and printed) will be non-political but very firm on the feminist leadership.
5. Assist in the production of a quarterly WFT's printed magazine. The consultant should advise as why it will have an impact, if online magazine is already in place. Attach one or two samples of how the printed magazine will look like, its size and number of pages.
6. Assist in arranging for online/interest TV (mobile and through their cell phones and computing devices.
7. Assist in production of video documentaries that will have an impact on our agenda.
8. Arrange for quarterly training of staff and board members on media and communicate issues (when required to do so).
9. Write a specific paper on crisis management and communication, to guide and inform management and Board Members for preparedness of crises in future.
10. Provide monthly communication reports to the management.

**ELIGIBILITY CRITERIA**

1. The applicant (individual or firm) must have recognized qualifications in public relations / mass communication/-journalism/advertising /marketing fields
2. Minimum of six (6) years of experience in the relevant fields of public relations and communication as well as journalism.
3. Experience at the national or international level in public relations, communications, consultancies/advocacy will be highly desirable.
4. Have effective communication and training skills
5. Awareness on gender issues and issues of concern for the women's movement at community and national level.

**DURATION OF WORK:**

The assignment will be for an initial period of one year. The assignment will be effective on the date of signing the contract.

**INTELLECTUAL PROPERTY**

WFT shall, solely and exclusively, own all rights in and to any work created and handled over to WFT within this contract. The fellow shall not be allowed to post or publish or distribute (electronically or in print) any materials or information without the explicit consent of its Executive Director or her appointed representative.

**SUBMISSION FORMAT**

The individual or firm must submit two envelopes of expression of interest. One that has details on issues **(TECHNICAL PROPOSAL)** and it should not exceed 15 typed pages. And another **(FINANCIAL PROPOSAL)** which give approximate costs for each activity detailed in the Technical Report. The two envelopes shall then be enclosed in a single envelope and marked: **EXPRESSION OF INTEREST FOR PROVISION OF COMMUNICATION AND MEDIA SUPPORT SERVICES.**

**The deadline for submission will be on 16th August 2019.**

The bid(s) can be sent by hand to the physical address provided in the WFT website, or by post to the address below:

**THE EXECUTIVE DIRECTOR,
WOMEN FUND TANZANIA,
P. O. BOX 79235,
NAMANGA, MSASANI
DAR ES SALAAM
TANZANIA**

Bids in soft copy may be sent via **email to info@wft.or.tz** with subject as **EXPRESSION OF INTEREST TO PROVIDE COMMUNICATION AND MEDIA TECHNICAL SUPPORT SERVICES TO WFT** not later than **16th August 2019.** Late expression of interest shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

***N.B only shortlisted candidates/firms will be considered.***

21535/002

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Angalizo la Makamu wa Rais mazingira litekelezwe

**UTEKELEZAJI** wa miradi mikubwa umekuwa ukifuatiliwa kwa karibu sana na serikali pamoja na wadau wa mazingira, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mazingira yanabaki salama bila kuathiriwa.

Serikali ina utaratibu wa kufanya tathmini ya athari za mazingira pale mwekezaji anapojiandaa kuanzisha mradi, na pale inapobainika kuwa kutakuwapo na athari za mazingira mradi huo hauwezi kukubaliwa wala mhusika kupewa cheti kutoka kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Aidha, wadau na mashirika yasiyo ya kiserikali hususan yanayojihusisha na masuala ya mazingira yamekuwa yakifuatilia kwa karibu miradi inayotekelezwa nchini, na pale inapobainika kuwa itasababisha athari za mazingira wamekuwa wakiendesha kampeni za kukosoa serikali isiikubali kutekelezwa.

Moja ya miradi mikubwa ambayo wadau wa mazingira walifanya kampeni kubwa ya kuupinga ni wa kufuga samaki aina ya kamba katika Delta ya Rufiji mkoani Pwani mapema miaka ya tisini. Hakika jitihada zao zilifanikiwa baada ya ukweli kubainika bila kuacha shaka yoyote kwamba ungesababisha uharibifu wa mazingira, ikiwamo kukatwa kwa miti aina ya mikoko. Jitihada mbalimbali za kulinda mazingira ambayo ni moja ya ajenda muhimu katika suala la maendeleo endelevu zimekuwa zikiendelea kufanywa na serikali pamoja na wadau.

Kwa mfano, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema kuna mzigo mkubwa wa kutunza mazingira katika mradi mkubwa wa uzalishaji umeme Rufiji ili kuhakikisha maji yanatiririka na hayazuiliki kwa shughuli yoyote.

Makamu wa Rais alitoa kauli hilo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifungua Jukwaa la Maendeleo Endelevu kuhusu usimamizi bora wa misitu kwa upatikanaji wa rasilimali maji endelevu lililoandaliwa na Taasisi ya Uongozi.

Samia alisema kwamba ni lazima kujipanga vizuri ili maji yaweze kutiririka kuanzia vyanzo vya juu vya eneo hilo na yasizuilike popote.

Kwa mujibu wa Samia, kila mmoja anajua mabwawa ya maji makubwa yanayozalisha umeme ni kwa maendeleo ya taifa, na tunajua mradi mkubwa wa uzalishaji umeme Rufiji utategemea mtiririko endelevu wa maji kutoka vyanzo vikuu ikiwamo mito na madakio ambayo yanaanzia kwenye misitu na maeneo mengine.

Kwamba mwaka juzi kulikuwapo na kampeni ya utiririshaji maji katika Mto Ruaha kutokana na hali yake kuwa mbaya kwa kipindi hicho. Samia alisema wanyama wanahitaji sana maji katika maeneo ya hifadhi kiasi cha kuweka foleni kiasi cha kutegemea tembo wakati mwingine wawasaidie wengine kuchimba kama alivyowahi kushuhudia katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Kwa hiyo jamii nzima ya Watanzania tunapaswa kuichukulia kauli ya Makamu wa Rais kama changamoto katika suala zima ambalo yeye ameliita kuwa ni mzigo mkubwa wa kutunza mazingira katika mradi mkubwa wa uzalishaji umeme Rufiji ili kuhakikisha maji yanatiririka na hayazuiliki kwa shughuli yoyote.

Samia akisema hivyo akimaanisha umuhimu mkubwa wa kulinda mazingira katika eneo hilo ambalo limeanza kujengwa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji megawati 2,100, hivyo kuisaidia nchi yetu kumaliza changamoto kubwa na ya muda mrefu ya uhaba wa nishati ya umeme.

Tumaamini kuwa kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha anazingatia ushauri huo, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa maji ya Rufiji yanaachwa yatiririke bila kuzuiliwa kwa ajili ya shughuli nyingine ambazo zinaweza kusababisha athari za mazingira.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge

## Diplomasia ya uchumi itilie mkazo bidhaa ya mkulima

Na Reubeni Lumbagala, KONGWA

**WAKULIMA** wa mazao ya chakula na biashara na wazalishaji malighafi viwandani, wana nafasi kubwa kuongeza mauzo yao na hatimaye kuwa milionea, kama masoko ya uhakika yatafanyiwa kazi kikamilifu.

Uzalishaji bidhaa za kilimo na viwandani, bila ya kuwapo masoko ya uhakika, ni hasara kwa wazalishaji.

Kilimo ndicho kinawaajiri Watanzania wengi, pia ndio uti wa mgongo wa uchumi kitaifa. Hivyo, hakuna namna wawekezaji viwandani wanaweza kubadili maisha kwa kupitia faida ya jasho lao, kama masoko ya bidhaa yatasuasua.

Ni vyema kumkwamua mkulima mdogo nchini, jambo linalowezekana kupitia wawekezaji viwandani kuandaa mazingira ya kuuza mazao yao kwa bei nzuri, inayoendana na uhalisia sokoni.

Juhudi za ukuzaji uchumi duniani zinachagizwa na diplomasia ya uchumi, inayokuza ushirikiano baina ya nchi moja na nyingine. Diplomasia ya uchumi ni ushirikiano kati ya nchi moja na nyingine katika ukuzaji uchumi kwa maslahi ya wanaoshirikiana. Ni faraja kuona Tanzania haiko nyuma katika maendeleo ya viwanda na ukuzaji uchumi wake. Zipo juhudi zinazofanywa na serikali kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchini, kuwekeza katika sekta mbalimbali hasa kilimo, viwanda na huduma nyingine za kijamii.

Ni juhudi zilizozaa matunda, kwani wawekezaji wamevutiwa kuwekeza nchini na kuchangia ukuaji wa uchumi wetu.

Eneo jingine la upatikanaji wa masoko kwa mazao na bidhaa kutoka Tanzania, ambayo juhudi za makusudi zinapaswa kuongezwa kusaidia maendeleo ya kilimo, viwanda na ukuaji uchumi. Viongozi serikalini na wananchi wanapaswa kutoishia kuonyesha maeneo ya uwekezaji. Ni wakati wa kujikita kutangaza mazao na bidhaa zinazozalishwa, ili kupata soko la uhakika na kuongeza uzalishaji.

Tanzania imebarikiwa ardhi ya kutosha na nzuri, iliyojaa rutuba kwa mazao ya chakula na biashara kuzalishwa kwa wingi.

Nitatoa mifano ya mahindi, ufuta, alizeti, maharage, mbaazi, mawese, matunda, mboga, viazi, chai, katani, kahawa, korosho, pamba zinazozalishwa kwa wingi.

Viwanda vyetu zinazalisha bidhaa bora zinazomudu vigezo vya ushindani katika masoko kitaifa na kimataifa, yayohitaji masoko ya uhakika, ili wakulima wafaidi jasho na mitaji waliyowekeza.

Ni wakati sahihi, balozi zetu katika mataifa mbalimbali kutangaza na kutafuta masoko ya mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini. Mabalozi wajibu wao ni kuwa viungo wa wakulima na wazalishaji nchini na wanunuzi waliopo katika nchi waliko, ili upatikanaji masoko ya uhakika kwa mazao na bidhaa nchini, liwe jambo halisi.

Kila balozi anapaswa kuwa na deni la kuhakikisha anafanya kila linalowezekana, wakulima na wawekezaji wanazalisha bidhaa kutoka Tanzania, ili kuboresha maisha ya wananchi husika.

Bidhaa na mazao yanayozalishwa nchini, yanahitajika sana katika nchi mbalimbali duniani, lakini tatizo linaodumu ni kushindwa kuyachangamkia masoko. Ulimwengu wa sasa ni wa ushindani katika kila jambo. Watanzania hatupaswi kujifungia kusubiri masoko yatafute, bali sisi ndio kuyatafuta masoko.

Mkulima kijijini kabisa, ukimwambia changamkia soko la mbaazi lililoko India, ni kumchanganya zaidi, kwani atashindwa kujua aanzie wapi na pa kuishia nako kufanikisha kuiuza mbaazi yake India.

Serikali kupitia balozi zetu zitakapoandaa taratibu nzuri wa namna ya wakulima watakavyouza mbaazi zao India, itakuwa rahisi wakulima kufanikisha hayo. Mabalozi wetu wanaandaa mikutano ya kuonana na wafanyabiashara na wanunuzi wa mazao na bidhaa, ili kutangaza fursa za mazao na bidhaa kutoka Tanzania.

Hakuna sababu Tanzania kuwa watazamaji wa masoko ya uhakika yaliyopo nje ya nchi, wakati tuna vigezo vya kuchuana. Diplomasia ya uchumi inapaswa kutumika kikamilifu, kubadili maisha ya shambani. Jambo muhimu ni kuzingatia wakulima kuzalisha mazao na bidhaa bora zinazokidhi viwango kimataifa.

Tanzania ya Viwanda kusonga katika safari ya uchumi wa kati na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 inawezekana kama diplomasia ya uchumi itajikita kutafuta masoko kuwasaidia wakulima wasilanguliwe mazao yao.

Bado naamini nchini, mkulima akiinuka, hapana shaka uchumi wa nchi utakuwa kwa kasi.

# Wafanyakazi wanaolima, kufuga sasa kukopeshwa

**Na Enock Charles**

WAFANYAKAZI wa sekta ya umma na binafsi wanaolima na kufuga, wamepata neema baada ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Benki ya Stanbic kusaini makubaliano ya kuwakopesha vifaa na nyenzo za kilimo ili kuchagiza maendeleo na ukuaji wa sekta ya kilimo na mifugo hapa nchini.

Akizungumza baada ya kusaini randama ya makubaliano hayo jijini Dar es Salaam,

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema kuimarika kwa sekta ya kilimo na mifugo kutafanikisha azma ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Makubaliano haya kati ya TADB na Stanbic yatasaidia sana wafanyakazi kunufaika na mikopo hiyo kutokana na uzoefu wa wenzetu wa Stanbic walionao katika eneo hili na hasa katika kushughulika na wafanyakazi," amesema Justine. Justine aliongeza kuwa makubaliano hayo ni ya kimkakati zaidi kwa kuwa Stanbic wanamatawi katika maeneo mengi nchini hali itakayorahisisha kuwafikia wananchi wengi.

"Stanbic wapo katika maeneo mengi ya kimkakati kama Mwanza, Mbeya, Arusha na Dodoma hali ambayo itasaidia sana katika kuwafikia walengwa ambao ni wafanyakazi katika sekta za umma na binafsi," aliongeza. Justine.

Justine alizipongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na benki za biashara nchini katika kuunga mkono jitihada za Rais John

Magufuli za kuhakikisha wakulima wa ngazi zote wananufaika na shughuli zao za kilimo, na kuongeza kwamba makubaliano hayo nayo yamelenga kufanikisha azma hiyo.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Benki ya Stanbic, Fredrick Max, alisema benki yao imejipanga kutekeleza makubaliano hayo kama walivyoshirikiana na TADB katika makubaliano ya Machi juu ya mnyororo wa thamani wa mazao mbali mbali.

"Ni furaha kwetu kushirikiana na TADB katika kuifanya Tanzania iwe ya viwanda. Makubaliano haya pia ni neema kwa kila mwananchi atakayekopa kwani ukopeshaji wa vifaa vya kilimo utaongeza mapato kwa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alieleza Max.

Kadhalika, Max alisema makubaliano hayo yamelenga kuwakopesha wakulima vifaa na nyenzo za kilimo kama matrekta, mashine za kuvunia mazao, mashine za kuchakata mazao pamoja na magari ya kubebea mizigo.

# JPM ataja aliyotekeleza miezi 45

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli ametaja miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika miezi 45 aliyokaa madarakani tangu alipoapishwa Novemba 5, 2015.

Rais alieleza miradi hiyo wakati wa hafla ya ufunguzi wa jengo la tatu (Terminal III) la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam jana, ambalo lina uwezo wa kuhudumia abiria 6,000,000 kwa mwaka. Hafla hiyo ilihudhuriwa na wananchi na viongozi mbalimbali wakiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Job Ndugai, Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim, mawaziri na makatibu wakuu mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, wabunge, viongozi wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa na wakuu wa mikoa.

Katika hafla hiyo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (Tanroads), Patrick Mfugale, alisema ujenzi wa jengo hilo umegharimu Sh. bilioni 722 na kwamba kukamilika kwake kutaufanya uwanja huo kuongeza uwezo wa kuhudumia abiria kutoka 2,000 hadi kufikia 8,000.

Rais Magufuli aliipongeza Tanroads kwa kusimamia ukamilishaji wa uwanja huo, hasa baada ya ujenzi wake kukwama mwaka 2016 kutokana na mkandarasi kutolipwa fedha alizokuwa anadai, huku akimpongeza Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, kwa kuanzisha ujenzi wa uwanja huo.

Rais Magufuli aliwataka Watanzania kujivunia mafanikio hayo, huku akibainisha kuwa kufanikiwa kwa mradi huo na miradi mingine mikubwa ambayo serikali yake inaitekeleza, kutokana na uamuzi thabiti, usimamizi mzuri na nidhamu ya serikali katika matumizi ya fedha za umma na kuwabana mafisadi.

"Ndugu zangu Watanzania tunaweza, kinachotakiwa ni kujiamini na kuamua kufanya, bila kuamua Watanzania tutaendelea kuwa wategemezi katika miradi ya maendeleo ya taifa letu," Rais Magufuli alisema.

Aliitaja miradi mikubwa ambayo imetokana na uamuzi thabiti uliofanya kuwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (SGR) utakaogharimu Sh. trilioni 7.5, mradi wa umeme katika Mto Rufiji (Sh. trilioni 6.5), ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi (Sh. bilioni 699) na ujenzi wa barabara za juu Ubungo - Dar es Salaam (Sh. bilioni 247).

Mingine ni ujenzi wa Daraja la Selander (Sh. bilioni 270), ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha (Sh. bilioni 140), ujenzi wa viwanja vya ndege 15 (Sh. trilioni 1.868) na ununuzi wa ndege (Sh. trilioni 1.03), akibainisha kuwa serikali imeamua kununua ndege zingine tatu.

Miradi mingine ni ujenzi wa barabara na madaraja (Sh. trilioni 5.37), ujenzi wa bandari kuu (Sh. trilioni 1.2), ujenzi wa meli katika maziwa makuu (Sh. bilioni 172.3), ujenzi wa barabara za lami katika Jiji la Dar es Salaam (Sh. bilioni 660), ujenzi wa majengo ya halmashauri (Sh. trilioni 1.35) na ujenzi wa hospitali na vituo vya afya (Sh. bilioni 361).

Mingine ni ununuzi vifaa vya hospitali (Sh. bilioni 64), ujenzi wa rada nne katika viwanja vya ndege (Sh. bilioni 67), mikopo kwa elimu ya juu (Sh. trilioni 1.612), kutoa elimu bure (Sh. bilioni 348.67) na kukarabati shule na vyuo vikongwe (Sh. bilioni 308.1).

Rais Magufuli alisisitiza Tanzania siyo masikini na akawataka Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali za kujipatia kipato ikiwamo kuutumia uwanja huo vizuri na kuongeza uzalishaji mali katika maeneo mbalimbali.

Awali, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema kuwa baada ya kukamilisha uwanja huo, wizara yake inajipanga kukarabati jengo la pili la uwanja huo ili kuliongeza uwezo kutoka kuhudumia abiria 1,500,000 kwa mwaka hadi kufikia 3,000,000.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akionyesha mpango mkakati maalum wa kupambana na hasara zitokanazo na mambo ya kilimo, baada ya kuuzindua kwenye uzinduzi wa Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu jana. Kulia ni Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga na ( kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka. **PICHA: OMR**

# Moto wateketeza maduka Pemba

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

MOTO mkubwa uliozuka stendi kuu ya magari soko kongwe mjini Chake Chake umeteketeza idadi kubwa ya bidhaa zilizo kuwamo ndani ya maduka hayo, huku moja likiteketea lote.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo jana asubuhi waliona moshi ukifuka ndani ya duka moja ndipo walipompigia simu mmiliki wa duka hilo, hakupokea simu ndipo walipoamua kulivunja na kushuhudia moto huo.

Said Ali Saidi, moja kati ya watu wa kwanza kushuhudia moto huo, alisema waliudharau kwa kwenda kuchukua kifaa cha kuzimia moto wakiamini watauzima, lakini walipojaribu kuuzima uliongezeka zaidi ndipo walipowapigia simu Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chanjaani Chake Chake.

Alisema muda mfupi Zimamoto walifika na magari mawili kwa ajili ya kuzima, na walijitahidi kuuzima, lakini maduka sita yakawa yamepata athari kati ya 14 yaliyomo ndani ya jengo hilo.

Maduka yaliyoteketea vibaya ni sita ambayo yanamilikiwa na Abdalla Anasi Ali ambaye ana maduka mawili, Juma Ali Juma, Rukia Bakari Khamis na Rabia Omar Said ambao hawakuwapo wakati wa moto unatokea.

Mmoja kati ya wamiliki hao, Rabia Omar Saidi, alisema kwenye duka lake vitu vingi vimeharibika. Alisema ingawa kuna vilivyonusurika, lakini amepata hasara kubwa na kusababisha mtaji wake kutetereka. Kamanda wa Polisi Mkoa Kusini Pemba, Hasan Nasiri Ali, alisema moto huo umeleta hasara kubwa ikiwamo fedha na tathmini inatarajia kufanyika baadaye. Alisema hasara ya mali ni kubwa, lakini hasara ya fedha ingeweza kuepukika kama wafanyabiashara hao wangekuwa na tabia ya kuweka fedha benki na kutaja fedha ambazo walifanikiwa kuziokoa na kumkabidhi miliki wa duka moja ni zaidi ya shilingi milioni 35. Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Pemba, Simai Haji Siamai, alisema kwa mujibu wa uchunguzi wa awali, moto huo umesababishwa na hitilafu ya umeme ambao asubuhi ulikuwa unawashwa na kuzima kiholela.

Mkuu wa Wilaya Chake Chake, Rashid Hadidi Rashid, aliyefika eneo la tukio na kuwapa pole waathirika, alielezea kusikitishwa kwake na jinsi moto huo ulivyo leta athari kubwa kwa wafanyabiashara hao.

# Madiwani wa CUF wagomea kikao

**Na Said Hamdani,** LINDI

MADIWANI 11 kati ya 29 katika Manispaa ya Lindi, mkoani hapa wamegoma kuhudhuria kikao cha baraza kipindi cha robo ya nne, kwa kile kinachoelezwa kutolipwa kwa posho zao mbalimbali kwa muda mrefu.

Kikao hicho kwa ajili ya kupata taarifa kwa kipindi cha kuanzia Aprili mosi hadi Juni 30 mwaka huu kilifanyika ukumbi wa DDC mjini hapa.

Madiwani hao 11 kupitia Chama cha Wananchi (CUF) ni wa kata na viti maalumu, na waligoma kuhudhuria kikao hicho Julai 31, mwaka huu.

Kabla Mwenyekiti, Mohamedi Lihumbo, hajakifungua kikao hicho, Diwani wa Wailesi, Khalifa Mbaruku (CCM), aliomba mwongozo kutaka kufahamu sababu za wenzao kutoonekana ukumbini na ni halali kufanyika kutokana na mapungufu yaliyopo.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujulishwa upande wa wenzetu wa CUF viti vipo tupu. Je, kanuni zinaruhusu kufanyika kwa hiki kikao?" Alihoji Mbaruku.

Baada ya maelezo hayo, Mwenyekiti wa Kikao hicho, Mohamedi Lihumbo ambaye pia ni diwani wa RahaLeo, alimtaka Kaimu Mwanasheria, Kennedy Wembe, kutoa ufafanuzi na kueleza ni halali kuendelea kwani idadi ya wajumbe waliopo sheria inaruhusu kuendelea na kikao.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Jomary Satura, alisema madiwani hao walimegoma kuhudhuria kikao wakishinikiza kulipwa posho zao zikiwamo za vikao vya kamati mbalimbali.

Alisema yeye akiwa ni Mtendaji Mkuu wa Manispaa hiyo, hajawalipa posho hizo bila kutaja kiwango chake, kutokana na hali mbaya ya kifedha, huku akiahidi kulipa madiwani wote pale hali itakapokuwa mzuri.

"Sijakataa kulipa posho zenu waheshimiwa, lakini kwa sasa hali ya manispaa yetu kifedha sote tunaifahamu, pale mambo yatakapotengamaa mtalipwa posho zenu," alisema Satura.

Pia Mkurugenzi huyo amewaomba madiwani wa vyama vya CUF na CCM waliopewa dhamana ya kuwatumikia wananchi, kujenga uvumilivu kipindi hiki cha mpito na pale hali itakapokuwa nzuri kifedha watalipwa kama kawaida.

Hawa Kipara (Viti maalumu) na Hafidhi Kitutu wa Kata ya Mitandi, wakizungumza kwa niaba ya wenzao, walisema walifanya hivyo kutokana na kutolipwa kwa posho zao zikiwamo vya kamati mbalimbali na baraza kuanzia Aprili 2019 hadi sasa.

Pia walitaja sababu nyingine ni kutowapa taarifa mapema, badala yake wanaelezwa muda wa kufanyika vikao ukiwa umemalizika, huku baadhi yao wakiwa wametegemea kupata nauli ya kurejea kwenye maeneo ya kata zao.

"Wapo baadhi ya madiwani wenzetu, acha sisi tunaoishi mjini hapa, wanatoka mbali na wamejenga matumaini ya kupata nauli ya kuwarejesha kwao, wanapokosa inakuwaje hapo?" Alihoji Kipara.





Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi, akimkabidhi mifuko 300 ya saruji Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Avodi Mmanda (kulia), kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Mtwara, katika hafla hiyo iliyofanyika mjini Mtwara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania waambiwa kukaa mguu sawa fursa za SADC

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wakumbushwa kujitokeza kwa wingi kushiriki katika Maadhimisho na Maonyesho ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) yatakayoanza Agosti 5 hadi 8 mwaka huu.

Maonyesho hayo yatafanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Viwanja vya Karimjee na Gymkana jijini Dar es Salaam. Wito huo ulitolewa Dar es Salaam jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Joseph Buchweishaija, ambapo alisema wanatarajia nchi 16 wanachama wa SADC zitahudhuria. Alisema kuwa wiki hiyo ya SADC itawawezesha wananchi kuona fursa mbalimbali ikiwamo kupata malighafi za kilimo ambazo viwanda huzitumia kuzalisha bidhaa viwandani. Prof. Buchweishaija aliongeza kuwa miongoni mwa faida watakazozipata Watanzania kupitia maonyesho hayo ni kujifunza kubadilishana uzoefu na nchi nyingine za jumuiya hiyo ambazo zitashiriki pamoja na kuongeza wigo wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Nafasi kwa kila Mtanzania kujisajili bado ipo mpaka tarehe 2/7/2019 na wale ambao watakuwa hawajajisajili wasiwe na wasiwasi maana nao watatembelea maeneo ya maonyesho kama wengine na kuweza kujionea bidhaa za nchi nyingine, hivyo watu wote wanakaribishwa sana kwa ajili ya tukio hilo la kihistoria ambapo litatokea tena baada ya miaka 15 kupita," alisisitiza.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ludovick Nduhiye, alifafanua lengo kuu ni kuweka utayari kwa wananchi hususan wa Tanzania kushiriki kwa wingi na kujionea fursa lukuki ambazo zitaonekana katika maonyesho hayo.

Alizitaja fursa pekee zitakazopatikana katika wiki hiyo ya maonyesho ni pamoja na upatikanaji wa masoko, kubadilishana mawazo, uzoefu na namna ya kuanzisha viwanda ambapo pia watakaoshiriki watajulishwa fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye nchi hizo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Maonyesho na maadhimisho hayo, kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Mtengamano na Biashara, Ally Gugu, alihimiza wananchi kujisajiri kupitia tovuti ya wizara ambayo ni www.mit.go.tz na kisha kubofya link mbili za haraka (quick link) ambazo niza usajiri wa Wiki ya Viwanda na Mkutano wa 39 wa SADC.

# Wataka mbunge kuwatatulia kero

**Na Elizabeth Faustine,**

MWANZA

WAKAZI wa vijiji vya Kata ya Buhumbi wilayani Magu mkoani Mwanza, wamemwomba mbunge wa jimbo lao kutatua changamoto ya ukosefu wa maji na umeme inayowakabili katika maeneo yao.

Hayo waliyabainisha katika mikutano iliyofanyika kata hiyo, wakati wa ziara ya mbunge kutembelea kijiji kwa kijiji kwa lengo la kuzungumza na kusikiliza kero za wananchi ambapo alipata fursa ya kutembelea vijiji vitano vya Kata ya Buhumbi vikiwamo vijiji vya Kitongo, Nyashoshi, Misungwi, Buhumbi na Mwamibanga.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyashoshi, Samweli Mpandachalo, alisema dhamira ya sera ya maji ni kumtua mama ndoo kichwani ila mpaka sasa katika kijiji hicho bado wanayo ndoo kichwani kutokana na kukosekana kwa maji, hivyo alimwomba mbunge kuwasaidia kutatua changamoto hiyo.

Mmoja wa wananchi wa kijiji cha Kitongo, Paul Maduka, alisema maji kwao ni shida wanayahitaji sana katika shughuli zao za kila siku pia suala la umeme katika kijiji chao ni changamoto na wananchi wana hamu ya kupata nishati hiyo, hivyo walimwomba mbunge huyo awasaidie hupatikanaji wake.

Kwa upande wake Mbunge wa Magu, Boniventura Kiswaga, alisema maji yatafika katika vijiji vyote na anaamini Rais atawasaidia kupatikanaji kwake kwa kuwapatia fedha, hivyo aliwaomba wananchi kuwa na subira na kuahidi kuwa Kijiji cha Nyashoshi kuwa cha kwanza.

"Naomba suala la maji nilibebe kwani limekwamisha hadi ujenzi wa zahanati, hivyo nitaenda kumwomba Rais Magufuli pamoja na mbunge aweze kutusaidia kutatua changamoto hii ili kijiji cha Nyashoshi kipewe kipaumbele," alisema Kiswaga.

Kiswaga alisema kuhusu suala la umeme Kijiji cha Kitongo mkandarasi yupo eneo la kazi 'mkandarasi yupo site' na serikali imeishamlipa fedha zake, hivyo wanachofanya ni kumsukuma ili nishati hiyo ifike kijijini hapo mapema na kupelekwa vijiji vingine.

## Manyanya afagilia maonyesho ya viwanda Ruvuma

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

NAIBU Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwezekaji, Mhandisi Stella Manyanya, amesema Maonyesho ya Viwanda na Kongamano la Uwekezaji Ruvuma litaleta fursa nyingi za kibiashara na uchumi mkoani humo imeelezwa mjini Songea mwishoni mwa wiki.

Alisema Mkoa wa Ruvuma umejaliwa kuwa na fursa nyingi sana na kwa muda mrefu hawakuwa wakifanya tukio kama hilo, lakini sasa kupitia kongamano hilo litawafungua kuwafahamisha watu mbalimbali kuwa nini kinapatikana mkoa huo.

Alisema changamoto zinazowakabili wawekezaji wadogo ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, lakini kwa sasa mkoa wa Ruvuma umepata mkombozi hususani Benki ya NBC ambayo inatoa mikopo mikubwa na midogo kwa masharti nafuu sana kinachotakiwa ni uaminifu.

"Nawakaribisha sana wawekezaji na wadau wote ambao wana nia thabiti ya kuja kuwekeza Ruvuma kwani mkoa huu umekuwa na nishati ya umeme ya kuridhisha inayoweza kukidhi mahitaji," alisema.

Kwa upande wake Meneja wa Tawi la NBC Songea, Simon Ntwale, alisema kuwa maonesho hayo yamekuwa fursa nzuri kwa Benki ya NBC kwa sababu wameweza kukutana na wadau mbalimbali watakaoweza kufungua fursa mbalimbali za kibiashara, Waziri Mkuu na Mkuu wa Mkoa huo wamesema kuwa Ruvuma itakuwa na wawekezaji mbalimbali.

Alisema NBC imepata faida ya kuingia mkataba na taasisi ya PASS ambapo wanakwenda kuwawezesha wakulima kupata mikopo ya kilimo ambapo mkopaji anaweza kupata pembejeo za kilimo.

Ntwale pia aliwatoa shaka wakulima wakubwa na wadogo pamoja na wachakataji na wawekezaji wadogo kujitokeza kwa wingi ili kupata mkopo endapo kampuni ya PASS itakuwa imeadhimisha kwa mteja husika kupata mkopo huo.

"Wawekezaji na wakulima wadogo msiogope kuitumia Benki ya NBC kwani ni benki yenu ambayo ipo tayari kuwasaidia ili mtimize malengo yenu kwani wengi wamenufaika na mikopo hiyo hadi sasa wanafanya biashara za mazao yao hadi nje ya nchi," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahamudu Mgimwa, akizungumza katika mkutano wa jimbo wa kutoa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya CCM 2015 - Juni 2019 jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# DC atoa angalizo wananchi kujichukulia sheria mkononi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Saraha Chiwamba, amewataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mikononi mwao, badala yake wavitumie vyombo vya sheria kupata ufumbuzi wake pale panapotokea tatizo dhidi yao.

Chiwamba alitoa onyo hilo alipokuwa akizungumza na waandishi wa vyombo vya habari Mjini Liwale.

Mkuu huyo ambaye pia ni mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama wilayani humo, alitoa onyo hilo baada ya kuzuka ugomvi kati ya wafugaji na wakulima wa vijiji vya Kimambi na Miruwi kisha kusababisha kifo cha mkulima mmoja. Akizungumzia tukio hilo, Chiwamba alimtaja aliyefariki dunia ni Mohamedi Chande Mpalila, mkulima wa Kijiji cha Kimambi na majeruhi ni Abuu Nakundi wa Miruwi, ambao inadaiwa walipigwa na vitu vizito vichwani wakiwa mashambani.

Chiwamba alitaja chanzo ni Julai 25 na 27 mwaka huu kutokana na wafugaji kugeuza mashamba ya wakulima kulisha mifugo yao.

Alisema kufuatia tukio hilo, ndipo mashambulizi yalipoanza na kusababisha majeruhi na mauaji.

Alieleza kwamba baadhi ya watu wamekamatwa, na wanaendelea kuhojiwa na Jeshi la Polisi ili kuwabaini waliohusika na matukio hayo.

"Hivi tunapozungumza na nyinyi hapa leo tayari baadhi ya watu wapo polisi wakiendelea kuhojiwa ili kuwafahamu wahusika," alisema Chiwamba.

Mkuu huyo wa Wilaya ya Liwale alisema kitendo cha mtu au watu kuchukua maamuzi ya kujeruhi au mauaji kwa wanaowakosea ni kosa, hivyo serikali kwa upande wake haipo tayari kuona wananchi wake wakipotezeana maisha.

Pia, aliwashukuru wananchi kwa utulivu waliouonyesha wa kutojibu mashambulizi dhidi ya wahusika kwani kama wangejibu, hali ya usalama ndani ya wilaya hiyo ingekuwa mbaya zaidi.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kimambi waliieleza Nipashe kuwa kuwa Chande baada ya kuuawa, wahusika waliuchukua mwili wake na kuutelekeza barabarani, kisha kutokomea kusikojulikana.

# Wadau wajadili kikwazo cha maendeleo endelevu

**Na Yasmine Protace**

MAENDELEO endelevu yatapatikana kama hakutakuwa na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa jamii.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Kivule, Anna Masawae, katika mdahalo ulioandaliwa na TGNP Mtandao na kuwashirikisha wana kamati za mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto (Mtakuwa) na wadau wa semina za maendeleo na jinsia (GDSS).

Anna ambaye pia ni katibu wa Mtakuwa katika kampeni ya kupambana na masuala ya ukatili wa kijinsia, alisema wamefanikiwa kupunguza matukio hayo katika kata hiyo.

Alisema mafanikio makubwa yamepatikana baada ya kutoa elimu kwa jamii juu ya kupambana na matukio hayo.

Akizungumzia Mtakuwa alisema ni mpango ulioanzishwa kwa ajili ya kutokomeza masuala ya ukatili. "Mpango huo niwa miaka mitano ambapo umeandaliwa kwa ajili ya kutokomeza ukatili wa kijinsia," alisema.

Aliongeza kuwa kila wanawake 10, wanawake sita wanaonekana wamefanyiwa vitendo vya ukatili kijinsia," alisema.

Aliongeza kuwa kila penye watoto 10, sita wanakuwa wamefanyiwa ukatili wa kijinsia.

Alisema matukio ya ukatili wa kijinsia yalikuwapo Kivule, lakini elimu ilipotolewa, jamii imekuwa ikitoa taarifa na sasa ukatili ambao unafanywa sio ule wa wazi bali ni wa kificho.

Deogratias Temba, Ofisa Programu Mwandamizi TGNP Mtandao, alisema serikali ilisema kuwa kila panapokuwa na maendeleo endelevu matukio ya ukatili wa kijinsia hayapaswi kuwapo. Aliongeza kuwa katika kutekeleza Mtakuwa inatakiwa kuwapo na mazingira mazuri ya mtoto.

Alisema 2021/2022 mpango wa serikali ni kuhakikisha matukio ya ukatili wa kijinsia yawe yamepungua kwa asilimia 50.

Paulo Ezira, mwanafunzi wa Shule Sekondari Msitu, alisema kamati ya Mtakuwa itembelee katika shule mbalimbali ili wasikilize kero za watoto ambazo wanakumbana nazo kuhusiana na matukio ya ukatili wa kijinsia.

# Zaidi ya 5,000 wanufaika fedha za Tasaf

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

JUMLA ya fedha za ruzuku Sh. bilioni 4.1 za mpango wa kunusuru kaya maskini (Tasaf) 111 zimetolewa kwa wananchi zaidi ya 5,000 kutoka kaya maskini za Halmashauri ya Meru wanaotoka vijiji 47 vya halmashauri hiyo na kuwawezesha kuanzisha miradi ya maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Emmanuel Mkongo, akizungumza jana na Nipashe alisema, fedha hizo zinatolewa kwa utaratibu na kuwa kaya yenye mtu mmoja hupewa Sh. 20,000 na kaya yenye watoto inatolewa kulingana na wategemezi wa familia ikiwa ni pamoja na watoto.

Mkongo alisema anajivunia kuona jinsi serikali inavyojali wananchi wake kupitia mpango huo kwa kuwaondolea wananchi umaskini baada ya kuanzisha shughuli za uzalishaji.

Alisema mpango huo umetekeleza miradi iliyopo kwenye ilani ya CCM na kuwa Tasaf III imeleta ukombozi Meru na kwa watu kutoka kaya maskini na kuwataka wanufaika kutunza miradi waliyoanzisha kwa fedha za mpango huo. Alisema fedha za ruzuku zimewasaidiwa wanufaika kutoka katika kaya maskini kujikomboa na kuupa umaskini kisogo kwa kuanzisha vikundi vya vikoba, ambavyo 122 vya vikoba vimeanzishwa na vinawanufaisha watu 1,700 kati yao wanawake wakiwa 1,500. Mratibu wa Tasaf Halmashauri ya Meru, Boniface Mwilenga, alisema mabadiliko ya maisha ya kaya zinazopata msaada huo zimetokana na mafunzo waliyopatiwa ya jinsi ya kutumia fedha hizo kabla ya kuingia katika mpango.

Mwilenga alisema mwaka 2014 wananchi kutoka kaya maskini, walipatiwa mafunzo jinsi ya kujiendeleza kutumia fedha wanazopokea na msaada wanaopewa na kuwa tangu waanze kupokea fedha hizo mwaka 2015, wamefanikiwa kujikomboa kutoka katika lindi la umaskini.

"Lakini mbali na kuimarika kwao kiuchumi pia watoto wao wameendelea kusoma vizuri kutokana na kumudu mahitaji muhimu ya watoto shuleni," alisema. Namvua Iddi (70), mkazi wa Kata ya Kikwe, alisema kabla ya kupata fedha hizo alikuwa anakula mlo mmoja kwa siku, lakini sasa anakula milo mitatu na ameweza kujenga nyumba bora ya kuishi ya bati na kuondokana na nyumba ya udongo. Alishukuru serikali kwa kuwajali wanyonge na kuomba waongezewe fedha zaidi ili waweze kujiimarisha kiuchumi kwa kuwa fedha inayotolewa kwa sasa haiwatoshelezi mahitaji.

Meru ni miongoni mwa halmashauri saba za Mkoa wa Arusha na imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kusimamia miradi ya kaya maskini ya Tasaf 111 bila ubabaishaji.



Waziri wa Nishati, Dk. Medadi Kalemani, akizungumza na viongozi wa Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara, katikati ni Mkuu wa wilaya hiyo, Joseph Mkirikiti, Mbunge Dk. Mary Nagu na Mwenyekiti wa CCM, Mathew Darema, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC amwagiza mkandarasi kuweka mifereji ya maji

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya Arusha, Gabriel Daqarro, amemwagiza mkandarasi wa kampuni ya Synohiydro Co. Ltd., ya nchini China inayojenga barabara za ndani katika Jiji la Arusha, kujenga mifereji ya maji pembeni mwa barabara hizo, pamoja na vituo vya kushushia abiria.

Daqarro alitoa agizo hilo jana wakati akifanya ziara yake ya kikazi ya siku moja ya kutembelea ujenzi wa barabara hizo, ujenzi wa uwanja wa michezo Ngarenaro.

"Nawaagiza wekeni mifereji ya maji pembeni mwa barabara ili kuleta usalama kwa wananchi wakati wa masika wasipate mafuriko, lakini tunalinda barabara zetu kusombwa na maji," alisema.

Miradi hiyo inasimamiwa na mradi wa mji mkakati Tanzania (TSCP) awamu ya tatu, Jiji la Arusha ambayo yote kwa pamoja inagharimu Sh. bilioni 22.3 huku utekelezaji wake ukiwa umefikia asilimia 87. Daqarro alimwagiza mkandarasi huyo katika eneo la Hospitali ya Mtakatifu Elizabeth, maarufu kwa jina la Kwa Babu, kuweka kituo cha kushushia abiria kutokana na kutokuwa na kituo, licha ya wagonjwa wengi wanaofika katika hospitali hiyo teule kupata huduma za matibabu.

Miongoni mwa barabara hizo zilizotembelewa ni pamoja na Barabara ya Oljoro Murieti yenye urefu wa kilomita 2.85 na ujenzi wake umekamilika kwa kiwango cha lami huku ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua, vivuko na njia ya waenda kwa miguu pamoja na uwekaji wa kingo za barabara ukiwa unaendelea.

Nyingine ni Sombetini-FFU yenye urefu wa kilomita mbili, Barabara ya Njiro yenye urefu wa kilomita 2.702 pamoja na barabara ya Krokoni yenye urefu wa kilomita 0.575 zote zikiwa zimekamilika kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua na uwekaji wa kingo za barabara, ukiendelea pamoja na Barabara ya Ngarenaro ya Kilomita 4.37.

Vile vile, alisema ameridhishwa na kasi ya maendeleo ya miradi na kumpongeza Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni kwa usimamizi mzuri wa miradi hiyo, inayoratibiwa na Ofisi ya Rais (Tamisemi), chini ya mkandarasi huyo na Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya UWP Consult.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi Anna John na Caleb Pallangyo, walimlalamikia mkuu huyo kuwa hakuna mifereji ya kupitisha maji ya mvua, katika barabara hizo na kuwa wana hofu itakapotokea mvua inaweza kuathiri makazi yao, lakini pia kutokuwapo kwa matuta hali inayosababisha ajali za mara kwa mara.

# Wafugaji walalamika kwa Waziri Mpina

**Na Cynthia Mwilolezi**, MBULU

WAFUGAJI wa kabila la Barabaigi katika kijiji cha Esh Kesh Wilaya ya Mbulu, wamelalamikia baadhi ya viongozi wa serikali kukwamisha mradi wa uwekezaji wa ng'ombe wa kisasa kwa ajili ya kupata mbegu bora zinazowawezesha kubadilisha mifugo na kufuga kisasa kwa maslahi yao binafsi. Kauli za wafugaji kutoka kijiji hicho kilichopo katika bonde la Yaheda, wameitoa jana kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliyetembelea kijiji hicho kwa lengo la kukagua mradi huo na kutatua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu.

Wananchi hao walisema wameridhishwa na uwekezaji huo, lakini baadhi ya viongozi wamekuwa wakikwamisha kwa kisingizo cha kutofuatwa taratibu. Akizungumza mmoja wa wafugaji hao, Itamuka Ntaja, mkazi wa Esh Kesh, alisema walitoa ardhi yao kwa ajili ya uwekezaji wa ng'ombe wa mbegu bora, ili waweze kubadilisha ng'ombe waliyonao wafuge kisasa na kuondokana na ufugaji wa asili usiokuwa na faida.

"Ardhi hii tumeitoa kwa hiyari yetu, lakini tunashangaa kila kukicha tunakuja kuhojiwa kuhusu ardhi hii na tunawajibu kuwa tumetoa kwa manufaa yetu, wafugaji hatuelewi kwanini inakuwa hivyo sisi tumeridhika na uwekezaji huu, tunapata ng'ombe bora tumejengewa shule visima vya maji kwetu tuna faida," alisema Daniel Gudal.

Pia alisema baada ya kujitolea eneo hilo na mradi kuanza kufanyakazi, baadhi ya viongozi wa serikali wameanza kudai kuwa mwekezaji amekiuka taratibu za kupata eneo hilo, kauli ambayo siyo ya kweli.

Akizungumzia hilo mwekezaji mzawa kutoka kabila hilo, aliyewezesha mradi huo, Geso Bajuta, alisema wamekuwa wakisaidia kutoa mbegu za ng'ombe wa kisasa kwa gharama nafuu na kutoa mfano wa dume bora la ng'ombe aina ya Sawari linalouzwa kwa Sh. milioni 1.5, lakini wao wanawapatia wananchi kwa Sh. 400,000.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, alisema eneo hilo lina mgogoro na suala lake liko kwa Waziri Mkuu, hivyo inatakiwa kusubiri matokeo yake, huku akidai kuwa eneo hilo ni mapito ya wanyamapori, ndiyo maana wanazuia.

# Malezi ya watoto sehemu za biashara huleta athari za ubongo

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MFUMO wa malezi ya watoto wa umri wa miaka sifuri hadi sita katika maeneo ya ujasiriamali yakiwamo masokoni, vituo vya mabasi, karakana za magari na nyumba za starehe, una athari kubwa katika ukuaji wa ubongo.

Vilevile, malezi hayo yasipodhibitiwa yatachangia kwa asilimia kubwa kujenga taifa la kizazi kisicho na mwelekeo na chenye urahisi wa kujihusisha na matukio ya uhalifu, dawa za kulevya na unywaji wa pombe uliokithiri na hatari kwa afya. Daktari bingwa mwandamizi wa afya ya jamii, uzazi na magonjwa ya kinamama, Dk. Moke Magoma, alisema hayo akizungumzia mfumo wa maisha hatarishi ya watoto zaidi ya 250 wanaolelewa ndani ya masoko ya Memorial, Soko Kuu, Mbuyuni, Pasua na Manyema katika Manispaa ya Moshi.

Dk. Magoma alisema hayo kufuatia utafiti uliofanywa na mradi wa kuongeza uelewa na uwajibikaji wa huduma bora za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (ECD), unatekelezwa na muungano wa vilabu vya waandishi wa habari nchini (UTPC), kwa kushirikiana na taasisi ya CiC ya Ireland. "Ubongo wa mtoto huanza kujifunza vitu kuanzia miaka 0 hadi sita, leo unapomweka sokoni ambako kuna kelele, matusi, moshi, moto na mazingira mengine yasiyo salama ni kumwandaa kukua katika hali mbaya hapo baadaye ni nadra kutoa wataalamu kama daktari, mwanasheria na wengineo," alisema.

Kwa upande wake, wafanyabiashara katika soko la Memorial, Ester Ramadhani, Salma Ngowi na Yasinta Mathias, walikiri watoto wao kulelewa katika mazingira ambayo ubongo wao huathirika kwa kutoshika masuala ya msingi bali malezi yasiyostahili.

"Hapa watoto tunawalea chini ya vibanda vyetu vya biashara, tunajua akili zao zina haribika, lakini hayo yote tunamwachai Mungu maana yeye ndiye anajua maisha tunayoishi huku...utamwachia nani mtoto wakati hata fedha ya kula kuipata ni shida," alisema Ramadhani.

Walikiri mara kadhaa watoto wanaokulia katika mazingira yasiyo rafiki hujifunza mambo yasiyoendana na umri wao, lakini pia huathiri suala la akili pale wanapoanza shule za awali na msingi. Wakizungumzia suala hilo, wenyeviti wa masoko ya Memorial, Godfrey Shayo na Mwenyekiti wa Soko la Mbuyuni, Lameck Mziray, walikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kuahidi kuweka mpango maalum wa utoaji wa elimu kuhusu athari za kuchanganya malezi ya watoto katika maeneo ya ujasiriamali.

# Wasomi washauriwa kujiunga vyama vya ushirika

**Na Mary Mosha,** HAI

VIJANA wasomi nchini wameshauriwa kujiunga na vyama vya ushirika, na kuondokana na mtazamo hasi kuwa vyama hivyo ni vya wazee, hatua ambayo itawawezesha kuongeza nguvu ya kitaalamu na kufanikisha jitihada ya kuimarisha ushirika nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Joyce Mbwambo, wakati walipotembelea baadhi ya vyama vya ushirika katika Wilaya ya Hai, akiongozana na wanafunzi 60 wa chuo hicho ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo.

Mbwambo alisema vyama vingi vya ushirika hususani vyama vya msingi, vimekuwa vikiongozwa na wazee, huku vijana wasomi wakiwa mitaani, na kusema kuna haja sasa kwa vijana hao kuamka na kuona kuwa vyama hivyo ni moja ya fursa kwao katika kupeleka elimu waliyoipata vyuoni na kuvisaidia kujiendesha kibiashara na kujikwamua kiuchumi. "Ipo fikra mbaya juu ya vyama hivi vya ushirika, vijana wasomi wanaona hawawezi kufanya kazi kwenye vyama hivi kwa madai kuwa hakuna hela, lakini baadhi ya wazee wanafikiria kuwa vijana watakuwa wezi kwenye vyama vyao. Haya ni mawazo hasi ambayo hayapaswi kuendelezwa katika harakati hizi za kufufua vyama vya ushirika nchini," alisema Joyce. Husein Omary, ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu Shahada ya Sanaa katika Utawala wa Ushirika, MoCU, alisema, bado kunahitajika elimu ya kina ya namna ya uendeshaji wa vyama vya ushirika na kubuni miradi ambayo itaviwezesha kujiendesha kwa faida.

"Vyama vingi vya ushirika havina hali nzuri, katika kipindi hiki ambacho serikali imedhamiria kufufua ushirika nchini, maofisa ushirika wanapaswa kutoka ofisini kwenda kwenye vyama hivi na kutoa elimu, kwa kuwa vingi vinayumba kutokana na kukosekana kwa elimu na utaalamu wa kuviendesha," alisema Omary.

Naye Mashaka Laurent, alisema katika harakati za kuvifufua vyama vya ushirika, ipo haja kwa serikali, kuyatazama masoko ya mazao na usimamizi wa vyama hivyo, kwa kuwa vyama vingi vimekuwa vikiyumba kutokana na usimamizi mbovu na kukosekana kwa soko la uhakika.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Atanus Lucas, akikabidhi mkataba wa kupambana na ugonjwa wa utapiamlo kwa Mtendaji wa Kata ya Ukune, Jane Matiko, wakati wa ufungaji wa mkataba huo, baina ya ofisi ya mkurugenzi na watendaji wa kata na vijiji juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Polepole aagiza kutatuliwa mgogoro wakulima, wafugaji

**Na Paul William,** MOSHI

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humprey Polepole, ameziagiza kamati za ulinzi na usalama katika mikoa ya Manyara na Kilimanjaro pamoja na wataalamu wao kukutana Agosti 20, mwaka huu, katika kata ya Arusha Chini ili kutafuta ufumbuzi wa mgogoro wa wakulima na wafugaji unaohatarisha maisha.

Polepole alitoa kauli hiyo jana alipoenda na kamati ya ulinzi na usalama Mkoa wa Kilimanjaro katika kijiji cha Chemchem, Kata ya Arusha Chini, kusikiliza wananchi kuhusu mgogoro huo wa wakulima kutoka wilaya za Mwanga na Moshi pamoja na wafugaji kutoka Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Kabla ya kukutana kwa kamati hizo za mkoa, Polepole aliagiza kamati za ulinzi na usalama pamoja na wataalamu wao wa Wilaya za Mwanga, Moshi na Simanjiro kukutana Agosti 9, mwaka huu, pamoja na wananchi ili kutoa mapendekezo kwa kamati ya ulinzi na usalama za mkoa. Alisema kuwa, mgogoro huo wa wakulima na wafugaji umekuwa ni wa muda mrefu sasa ambao umefanya baadhi ya wananchi kupoteza maisha huku wengine wakipata majeraha makubwa na kudai kuwa endapo hautapatiwa ufumbuzi wa kudumu utasababisha madhara makubwa kwa wananchi.

"Sisi viongozi tunajukumu kubwa la kuhakikisha wakulima na wafugaji wanaishi kwa amani na kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa hivyo haiwezekani wananchi wakaendelea kuishi kwa hofu wakati serikali ipo," alisema Polepole.

Alisema, wafugaji kutoka Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara kuleta mifugo yao katika kijiji cha Chemchem na kuilishia katika mashamba ya wakulima na wanapohoji hufanyiwa fujo na kusema hali hiyo haikubaliki.

Vilevile, Katibu huyo wa itikadi alisikitishwa na kitendo cha Mtendaji wa Kata ya Arusha Chini anapopelekewa matatizo ya wananchi na kutaka kwenda kujiridhisha jinsi mazao yalivyoharibiwa na mifugo amekuwa akitishiwa na wafugaji hao na kusababisha kuwapigia magoti na kuomba msamaha.

Aliongeza kuwa, mgogoro huo umekuwa ukichangiwa kuletwa na baadhi ya wakazi wa Kata ya Arusha Chini akiwamo diwani wa kata hiyo, Rojas Mmari kwa kuwakaribisha wafugaji kutoka Wilaya ya Simanjiro kuleta mifugo yao kulisha katika mashamba ya wananchi.

"Wananchi mnapaswa kuwa makini mnapochagua viongozi wa kuwaongoza sasa mnaona diwani wenu badala ya kuwa mstari wa mbele kuwatetea na kuwatumikia kwa vitendo yeye ndio amekuwa mtu wa kwanza kuwakaribisha wafugaji waje na mifugo yao kulisha katika mashamba yenu," alisema Polepole. Pia alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Hamisi Issah, kwa kushirikiana na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Moshi kuhakikisha kuanzia jana kunakuwa na gari la polisi katika kata ya Arusha Chini litakalokuwa likipitapita maeneo hayo kufanya doria hii ni baada ya kuwapo kwa taarifa wafugaji wameanza kuzunguka eneo hilo kufanya fujo.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema kuwa mgogoro wa wakulima na wafugaji, viongozi wa vijiji katika Kata ya Arusha Chini wamekuwa wakihusishwa kuwa chanzo kutokana na kuwakaribisha wafugaji bila kufuata taratibu.

Alisema, tatizo lingine ambalo limechangia mgogoro huo kukua ni kutokana na kutokuwa na utekelezaji wa maagizo ambayo amekuwa akiyatoa kwa Wilaya ya Moshi na yeye alifika eneo hilo na kukamata ng'ombe 60 waliokuwa katika mashamba ya wakulima na kuagiza wauzwe kwa mnada ili iwe fundisho.

Pia aliagiza fedha hizo zilipwe kama fidia kwa wakulima kutokana na mazao yao yaliyoliwa na mifugo hiyo, lakini katika hali ya kushangaza agizo hilo halikutekelezeka na badala yake ng'ombe hao walirudishwa kwa wenyewe. Aliongeza kuwa ili kuondokana na tatizo hilo ipo haja ya kila kijiji kutenga maeneo maalum kwa ajili ya ufugaji.

Mgogoro huo wa wakulima na wafugaji katika Wilaya za Mwanga, Moshi na Simanjiro umedumu kwa miaka 30 sasa na zaidi ya wananchi 10 wameshauawa, huku wengi wakipata majeraha makubwa.



Ukurasa 16

Hifadhi yenye mbega weupe, weusi na panzi wenye bendera ya taifa



Ukurasa 20

Brela yaeleza itakavyotinga Nanenane Simiyu na ajenda ya usajili kidigitali


# BUFE

Ijumaa Agosti 2, 2019

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe




## Maisha mapya ya 'Panya Road' mstaafu, Polisi sasa wateja wake

Ukurasa 15



# Safari mpya SADC kuibua Utalii wa Ukombozi nchini

**Na Judith Mhina,** MAELEZO

SERIKALI tangu katika zama za uongozi wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, ilijitoa mhanga kupokea, kuwahudumia, kuwahifadhi na kuwasaidia kwa hali na mali wapigania uhuru wa nchi nyingi duniani hasa hasa wa ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Mwalimu Nyerere katika moja na nukuu zake aliwahi kutamka: "Uhuru wa Tanzania hautakuwa na maana yeyote kama nchi zinazotuzunguka na binadamu wenzetu popote pale duniani hawako huru".

**INAENDELEA UK.18**

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Fursa nyingine ya SADC Dar kupitia haki makini ya kijinsia

Ukurasa 14

UCHUMI

# Fursa nyingine ya SADC Dar kupitia haki makini ya kijinsia

• Wanaokeketewa wahamishiwa ujasiriamali • Shindano maalu
mshindi 'kukwea pipa' • Ajenda ya serikali ukatili kuondoka 50



Wajumbe wa baadhi ya matukio ya kijinsia, ndani ya Jumuiya ya SADC. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Yasmine Protace**

HIVI sasa kila kitu na kila anakopita ni mada kuhusu mkutano na maonyesho ya soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ambao utakuwapo ndani ya siku chache zijazo.

Ni suala lenye mustakabali mpana, lisiloishia kunadi bidhaa pekee, bali kutetea haki za kijinsia na afya kwa wahusika, ndani ya ulingo huo wa SADC, Tanzania ikibeba kofia ya uenyeji.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Mwanda, akizungumza katika utoaji vyeti kwa washindi wa tuzo hizo za SADC, kuhusu masuala ya jinsia, anasema;

"Gender Link na wenyeji wenu TGNP Mtandao, mmefanya kitu kizuri kwa nchi na kitasaidia kuwaelimisha wananchi katika masuala ya kuzijua haki zao katika usawa wa kijinsia," anasema.

Vyeti hivyo vilitolewa katika makundi mbalimbali yaliyolishiriki kuwania tuzo za masuala ya jinsia, yakiwa ni mashindano makubwa yaliyozishirikisha nchi 15 wanachama wa SADC.

Katika hilo, anawaasa washindi na washiriki kwa jumla, kwamba watumie mafanikio hayo katika maeneo yao, wazidi kuzungumzia mafanikio na mikakati iliyowekwa

> **Gender Link na wenyeji wenu TGNP Mtandao, mmefanya kitu kizuri kwa nchi na kitasaidia kuwaelimisha wananchi katika masuala ya kuzijua haki zao katika usawa wa kijinsia.**



na serikali katika kupambana na masuala ya ukatili.

Pia, Grace anawapongeza washiriki wa mwaka jana waliosaidia kuitangaza Tanzania kupitia mikakati ya kupambana na ukatili wa kijinsia, hata ikasaidia kuongoza kufanya vizuri katika masuala la jinsia na kufuatiwa na Malawi.

Kwa mujibu wa ofisa huyo wa serikali, Tanzania inatambua usawa wa kijinsia ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya Taifa na ndio maana imeridhia mikataba ya kimataifa, yenye makubaliano lukuki ya kutekelezwa.

Anasema, hivi sasa serikali imeandaa Mpango wa Taifa wa Kupunguza Ukatili wa Kijinsia kwa asilimia 50, ifikapo mwaka 2021.

Grace anasema, kuna mikakati ya miaka mitano ya maendeleo ikijikita katika Sera ya Wazee, Watoto na Walemavu na Tanzania imejikita katika maazimio matano ya ajenda za mkutano wa Beijing, unaohusu jinsia, inayojumuisha usimamizi na uwezeshaji kiuchumi, kwa wanawake na ajira.

Grace anasema, hivi sasa kuna vituo vilivyoanzishwa kukabili dhana nzima ya ukatili wa kijinsia na serikali imeshatenga asilimia 10 ya kuwawezesha wanawake na vijana.

Baadhi ya
washiriki
oshinda k
masuala y
wakionyes
vyeti wali
bidhiwa k
shindano
der Links,
ya mtanda
wa SADC,
Dar es Sal
**PICHA: YA**
**PROTACE**

a





wali-
atika
a jinsia,
sha
vyoka-
utoka
na Gen-
ndani
ao
jijini
aam.
ASMINE

#### MSHINDI ANENA

Rehema Mwinyi, ni mmoja wa washindi wa vyeti vilivyotolewa, anasema siri ya ushindi wake, kuwa ni alivyojiamini kuisaidia jamii iliyokuwa na changamoto za kimaisha na kufanikiwa kuwainua kimapato.

Anatoa simulizi kwamba, wana kikundi cha kuweka na kukopa maarufu kama 'vicoba' kinachojulikana kwa jina la Maendeleo Vicoba na kimeanzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wanawake kwa kuwainua kiuchumi na kuwawezesha wanawake walio na mazingira magumu.

Binafsi, anashukuru asasi ya TGNP Mtandao, iliandaa mashindano yaitwayo Jenda Festival, ambayo alishiriki na kuwaona kinamama walioleta bidhaa zao katika maonyesho na walitoa ushuhuda, jinsi walivyoweza kubadilisha maisha yao kupitia biashara.

"Nilipata elimu. Nilianzisha kikundi ambacho tupo wanawake 29 na wanaume sita. Tumekuwa tukitengeneza sabuni za chooni, batiki, jiki na kutengeneza pilipili,"anasema.

Anaongeza kwamba, kuanzishwa kikundi hicho kumesaidia kuwainulia kipato wanawake na hata kuwawezesha wanawake kutojihusisha katika mambo ya ndoa za utotoni. Rehema anasema, wanawake wengi wamekuwa wakichukua mikopo na kuweka dhamana mali za ndani na baada ya kufanikiwa, waliunda kikundi hicho akijibuna kwamba, kudhalilishwa sasa hayupo tena.

Anasema, kutokana na kupata taarifa za kuwapo shindano, aliamua kujikita katika shindano kwamba na ameweza kushinda.

Kutokana na matokeo hayo, hivi sasa rehema anatarajiwa kuiwakilisha Tanzania katika kuwania tuzo zitakazofanyika nchini Afrika Kusini.

"Kwanza nawashukuru GDSS ambao walinipa taarifa kuwa kuna mashindano. Nilitumia fursa hiyo kushiriki na kueleza ninayoyafanya kupitia kikundi na nilifanikiwa," anasema.

Anatoa wito kwamba vikundi vikisikia ipo katika makundi, wanaposikia fursa zinazotolewa wajitokeze ili waweze kujulikana na kupata uzoefu kutoka kwa makundi mbalimbali yanayoshiriki.

#### MWANAHARAKATI

Seleman Bishagazi, ni mwanaharakati ngazi ya jamii, anayejitambulisha kwamba kwa sasa yupo katika mradi anaoutambulisha wa ukeketaji, katika eneo la Kipunguni, Dar es Salaam.

Anasema, huko Kipunguni nje ya jiji la Dar es Salaam, wanaishi na jamii kutoka mikoa mbalimbali ya nchini na wamefanikiwa kushinda kupata cheti katika mashindano.

Bishagazi anasema, anatoa uzoefu wa kuwanusuru watoto 34 waliowekwa kwa ajili ya kukeketwa na waliongea na ngariba, wanaodaiwa waliwakeketa mabinti kwa gharama ya Sh. 50,000.

Anasema, kwa wasichana walioanza mapenzi kabla ya kukeketwa, hatua ya kukeketwa kwao huendana na faini ya ng'ombe wawili, tofauti na asiyekeketwa.

Bishagazi anasema, vijana hao baada ya kuwaelimisha na kuwanusuru, wanawapatia elimu ya ujasiriamali, ushonaji, kilimo, ufugaji na kuwaingiza mikopo, waibuke kiuchumi.

"Siri ya Mradi wa Hakeketwi Mtu, ilifanikiwa kwa sababu walijengewa uwezo wa kielimu kutoka TGNP Mtandao, " anasema na kuongeza kuwa mradi huo wameona wawapatie elimu, ili waweze kupata pesa waachane na ukeketaji.

Anasisitiza kwamba ukeketaji unasababisha umaskini, hivyo matamasha yanapoandaliwa wananchi na jamii, yanasaidia cha muhimu kinachotakiwa kufanyika.

Kuhusu tamasha la jinsia la mwaka huu linaloandaliwa na TGNP Mtandao anawataka wajitokeze kushiriki, ili waweze kupata elimu itakayowasaidia maishani.

#### BOSI NGO

Janet John, Mwenyekiti wa asasi ya Bint Makini Foundation, ni mshiriki na mshindi wa mashindano ya Gender Link, anayesema wamekuwa akifanya miradi mingi inayowahusu wasichana.

Anasema, alifanya katika upande wa elimu na kuona kuwa mabinti wengi, wamekuwa wakikumbana na changamoto kutokana na hali zao.

Waliamua kutoa mafunzo kwa mabinti waliokosa elimu na kwamba, wameshaanza kuwasaidia wasichana na alishiriki mashindano ya SADC katika upande wa elimu na aliweza kufanikiwa kushinda kutokana na kazi yake.

Anasema kwamba, anaishukuru TGNP Mtandao, imekuwa ikimjenga kupitia mafunzo yanayotolewa kila anayoiita Jumatano ya GDSS.

#### OFISA TGNP

Anna Sangai, ni Ofisa wa Programu Harakati na Ujenzi wa Nguvu za Pamoja kutoka TGNP Mtandao, anasema mwaka jana, Tanzania iliongoza kufanya vizuri katika kuzungumzia masuala ya jinsia ikifuatiwa na Malawi.

Anasema, kinachotakiwa ni watu kujifunza takwimu zinazosaidia kutoa taarifa ya kujua ukweli wa tatizo na anawataka washiriki wanaokosa nafasi za ushindi, bado wana nafasi za ushindi kupitia fursa kama hizo zijazo.

***•Soma zaidi ya SADC uk. 18***



Mshiriki wa masuala ya jinsia wa SADC, akiwasilisha jambo.

# Maisha mapya ya 'Panya Road' mstaafu, Polisi sasa wateja wake



Shughuli za kujiajiri zikiendelea katika 'kijiwe' anachotumikia, Salum Kilango, mstaafu wa 'panya road.' **PICHA: MTANDAO**

MIAKA mitau hadi 10 iliyopita, hawa walikua vijana hatari, waliokuwa na uwezo wa kufanya uhalifu wowote, bila ya woga wa mikono mirefu ya dola au madhara kwao. Hapo ina maana, kuiba, kukaba, kupora hata hatari ya kuua.

Ni vijana waliunda vikundi vilivyofahamika kama 'Panya Road' ambavyo vilitikisa Jiji la Dar es salaam katika maeneo toauti kama Tandale na Buza, kwa uhalifu unaoendana na madhara kwa wanaoibiwa.

Lakini wanachama wa kundi hilo, leo hii wameachana na vitendo vya uhalifu kwa hiari na kuanzisha kijiwe chao cha kuosha magari.

Sasa wanapata kipato kujihudumia na kuendesha familia zao, Salum Kilango, akiwa miongoni mwa vijana hao zaidi ya 30, katika eneo la Gongolamboto, jijini Dar es salaam

Kilango, anasimulia jinsi alivyoishi maisha ya hatari alipokuwa akijihusisha na uhalifu na ilitawaliwa na mfumo wa 'ama zake ama zangu' anayemkaba na kumuibia.

Kwa zaidi ya miaka 10, yeye na wenzake walikuwa wahalifu wa kuogopwa na jamii, lakini sasa anatubu kwa kauli: ''Baada ya kukutana na wenzangu majanga yaliyowakuta watu waliochomwa na moto waliingia jela kwa kweli ilinibidi ninyooshe mikono juu.''

Kilango hivi sasa anafanya shughuli mbalimbali za kijamii katika mtaa anaoishi na majirani zake, ikiwa ni njia ya kurejesha uaminifu katika jamii yake, ambayo ilikuwa ikimtenga au kumuogopa kutokana na historia ya maisha aliyoyaishi awali.

''Sehemu nyingine napata ajira, lakini nashindwa kuaminika na jamii kutokana na sura yangu, wale wote, jamii iliyokuwa pale mimi sifanani nao,'' anasema Kilango

Lakini, kutokana na changamoto ya ajira, anasema wako vijana 30 walionzisha biashara ya kuosha magari, kazi ambayo huwapatia kipato anachosema 'si haba' kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya familia zao.

Pia, anakiri uhasama baina yao na Polisi haupo tena, kwani ni sehemu ya wateja wao na mmoja wa wanakikundi hao anaeleza:

''Hapa tupo kwa ajili ya kutafuta pesa, tunaaminika hata polisi wanatuachia magari yao tunaosha kuna vitu kama simu flashi na vitu vingine vya thamani''.

Mama anayejitambulisha kwa jina la Mariam, ni mke wa Kilango, ambaye alifichwa na mumewe kuhusu kazi anayofanya, ingawa aliisikia tu mtaani lakini kwa sasa ni familia kamili yenye watoto wawili waliotawaliwa na furaha kamili.

''Mwanzoni sikujua, lakini baadae tulipozoeana nikajua shughuli zake nikachukulia kawaida tu. Nilikuwa na wasiwasi mwanzoni kutokana na maisha tuliyokuwa tunaishi, lakini kwa sababu nilimpenda nilichukulia kawaida,'' anaeleza.

Mfumo wa wahalifu wa 'panya road' walivamia sehemu kwa ghafla wakiwa kundi kikubwa na kupora kikatili kila kilicho mbele yao.

**+ Kwa mujibu wa BBC**

BIASHARA

UTALII MAGAMBA

# Hifadhi pekee yenye mbega weupe, weusi na panzi wenye rangi bendera ya taifa

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa Lushoto**



Kilele cha Mlima Kigulu, kipo ndani ya Hifadhi ya Msitu Magamba.

NDANI ya hifadhi ya Magamba iliyoko Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, kuna mambo mengi ya kuvutia, ambayo si ya kusimuliwa kwa Mtanzania. Wanapaswa kuchangamkia fursa.

Baadhi ya maoni ya watalii wa ndani waliozuru hifadhi hiyo kupitia safari iliyoandaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) mapema mwezi huu, wanawataja wanyama kama mbega weusi na weupe (black and white Colobus monkeys).

Pia, wapo sungura, paa wa aina mbalimbali na ndege wenye sura na sauti  za kipekee kama bundi, vipanga na jamii za mwewe ambao kitaalamu wanaitwa 'Usambara nightjar' na jamii nyingi za vipepeo.

Katika mazungumzo na Nipashe, watalii hao wa ndani, wanaeleza kuwa waliopelekwa na TFS, katika hifadhi ya mazingira asilia ya Magamba wana nafasi ya kujivunia mali za taifa, kwa kuangalia vivutio ndani ya hifadhi hiyo asilia Magamba, kwa punguzo maalum.

Ni bei iliyotolewa kwenye Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), baada ya kutembelea na kujiandikisha katika banda la wakala hiyo.

Watalii wa ndani wanasema, Watanzania wanawajibika kupongeza jitihada zinazoendelea kuifanya serikali iendeleza maliasili za taifa, zinazochangia kuongeza pato la nchi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, watalii hao wanawaongezea ari ya Watanzania kuwa umefika wakati Watanzania wafungue macho kuona mali nyingi walizonazo na kubadili tabia zao kwa kuzithamini, kuzilinda na kuzitunza, ili ziendelee kuwa sehemu ya kukuza uchumi wa taifa.

Watalii hao baada ya kuingia katika hifadhi hiyo asilia Magamba, wanadodosa kufahamu kila kitu walichokiona hifadhini, kutokana na kuvutiwa na yaliomo, ambavyo wengi wanasema hawajawahi kuviona.

**MTALII & TFS**

Faustina Simon, ni mtalii wa ndani nchini, anayesema kwamba alishawishika kutembelea katika hifadhi hiyo, baada ya kusikia yaliyoko wilayani Lushoto, aliyokuwa akisikia ina milima mirefu na hali ya hewa ya baridi.

"Nilikuwa natamani tangu muda mrefu niende Lushoto kwa sababu nilikuwa sijui panafananaje zaidi ya kusikia kwamba ni sehemu yenye milima sana," anasema na kuongeza:

> **"Miti inatengeneza vitu vingi mbali na dawa, hapa kuna miti ambayo inatengeneza dawa ya kung`arishia viatu, kwa hiyo elimu tu ya kazi zinazofanywa na misitu ukija hapa inatosha kabisa.**

"Tena pana baridi, lakini nilipofika Sabasaba Saba na kupita katika banda la TFS ndipo nilikuta tangazo la safari ya kuja Magamba, nilifurahi na nikaomba nipewe muongozo na nilipoelekezwa nikawa nimeomba."

Anaendelea: "Nashukuru Mungu kwamba nimeweza kukidhi haja ya kiu niliyokuwa nayo muda mrefu na nimeona vitu vingi vizuri ambavyo sikuwahi kufikiria kwamba ningeviona katika maisha yangu.

"Nimebaini kwamba kumbe Tanzania tuna vitu vizuri ambavyo hatuvijui, mimi nawashauri Watanzania wenzangu, watafute muda na wajinyime kuja kujionea mambo mazuri kama haya  waone zawadi ambayo Mungu ametupa hapa Magamba," anasema mtalii huyo.

**MWAKLILISHI TFS**

Balozi wa Misitu TFS, Nelly Kazikazi, ni Mshindi wa Pili wa Taji la Miss Tanzania, anasema mbali na kazi kubwa inayofanywa na TFS kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa misitu, bado mwitikio ni mdogo.

"Mbali na kuwa balozi, leo kuja hapa Magamba nimejifunza mambo mengi ambayo nilikuwa siyajui. Watu wengi tukipita labda njiani kwa mbali tunaona miti, lakini huenda hatujui kwamba miti ni dawa.

"Miti inatengeneza vitu vingi mbali na dawa, hapa kuna miti ambayo inatengeneza dawa ya kung`arishia viatu, kwa hiyo elimu tu ya kazi zinazofanywa na misitu ukija hapa inatosha kabisa," anasema Nelly.

Anafafanua kuwa, ametembelea misitu na kuangalia aina ya mimea, wanyama wadogo wanaovutia na kuangalia mapango ya Wajerumani na Jiwe la Mungu, sehemu iliyotumika kusafirishia magogo kutoka milimani Magamba, kwenda bondeni Mombo.



Mbega weupe na weusi wakiwa katika Hifadhi ya Magamba: **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Nelly anasema, katika hilo walipitia kwenye miti mbalimbali inayotumika kutengeneza dawa za binadamu, ni sehemu ya kivutio kikubwa.

**MAGAMBA ILIVYO**

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Magamba, Getrude Nganyagwa, anasema ina ukubwa wa hekta 9283.9 na inazungukwa na vijiji 21.

Pia, anataja kuwapo mimea, wanyama wadogo na wakubwa, ndege, vipepeo na utulivu wa kipekee na anafafanua, hatua zilizochukuliwa kuwa: "Serikali imeweka juhudi kubwa katika msitu huu kuhakikisha kwamba unahifadhiwa kwa sababu una faida kubwa kwa jamii inayozunguka, kwa taifa na kwa dunia."

"Kwa hiyo tunapata hela kutoka serikali kuu kwa ajili ya uhifadhi na siri ya kufanikiwa kuhifadhi hii ni kutokana na mkakati imara tuliouweka kwa ajili ya kupambana na vitendo vya uhalifu ndani ya hifadhi  na tumewekeza zaidi kuelimisha jamii inayozunguka hifadhi kuhusu umuhimu wake," anaongeza.

Getrude anafafanyua kuwa, baada ya jamii kuona juhudi za serikali kutunza hifadhi hiyo na jitihada za kuwaelimisha, tayari imeshatabua ushiriki wa wananchi katika uendelezaji hifadhi hiyo.

Mhifahi huyo mkuu, anasema pia wao ni chanzo cha maji kinachotumiwa na vijiji  21 vinavyoizunguka hifadhi hiyo, kama inavyofafanuliwa na Getrude: "Tunafurahi sana kwa sasa tumeanza kuona matunda ya uhifadhi huu na tunaona Watanzania wengi wameanza kuamka."

Anaendelea: "Wameanza kufahamu kwamba kuna utalii zaidi ya ule waliokuwa wanaufahamu wa mbuga za wanyama pekee, na tunaishukuru serikali yetu kupitia TFS imewekeza sana kutangaza utalii wa mazingira, tunaiopongeza sana na tumeanza kuona matunda.

"Kwa mtu ambaye bado hajaelewa anaweza asitambue umuhimu wa hifadhi hizi, lakini kwa hawa ambao wamejua wamekuwa wakija mara kwa mara, kwanza wanasema vivutio vilivyopo katika hifadhi hii ni tofauti na vile walivyozoea na pia wanavutiwa na madhari."

**OFISA TFS**

Ofisa Misitu, Ugavi na Uenezi kutoka Wakala wa Misitu Tanzania, Shaban Kiula, anasema misitu ya hifadhi asilia ndiyo hifadhi pekee zinazotumika kama utalii ikolojia ambazo zinakuwa na mimea ya kipekee ambayo haipatikani sehemu nyingine.

Anasema, katika hifadhi 17 zilizo chini ya TFS, ndani yake kuna mengi kama vile viumbe, mimea ambayo wakati mwingine vinaweza kupatikana katika hifadhi moja na isiwepo katika hifadhi nyingine.

"Katika hifadhi zetu hizi 17, kuna hifadhi mojawapo ambayo ina mdudu anaitwa panzi, ambaye ana rangi ya bendera ya taifa. Vile vile ukienda sehemu nyingine za hifadhi utakuta kuna vinyonga wenye mapembe, ambao unakuta nao wanapatikana sehemu hiyo tu na sehemu nyingine hakuna ," anasema Kiula..

"Vile vile hifadhi nyingine unakutana na miti ya kipekee ambayo katika sehemu nyingine haipatikani. Kwa hiyo, hifadhi hizi ni muhimu sana na Watanzania nao wazifahamu kwa sababu tumekuwa tukipokea wageni kutoka nje, ambao wakija wanashangaa sana kuona vitu kama hivi

"Wanaona kama ni maajabu wakati sisi wenyewe hatuelewi kama ni vizuri na ndiyo maana tunazidi kuwahamasisha wavijue na viwasadie, wasiwaache wageni tu ndiyo wanufaike," anasema.

Anataja, baadhi ya hifadhi hizo za mazingira asilia zilizo chini ya TFS mpaka sasa kuwa ni pamoja na Amani, Muheza, Niro, Korogwe, Magamba, Chome, Uruguru, Mkingu, Udzungwa, Kilombero West, Rondo na Minziro.

Kiula anasema kila mwaka wamekuwa wakichagua hifadhi mojawapo na kutoa 'ofa' kwa wanaohudhuria katika maonyesho ya Sabasaba katika banda la TFS kuwapeleka katika hifadhi wanaokuwa wameichagua kwa mwaka husika.

Anasema, katika maonyesho ya mwaka jana, walichagua hifadhi ya mazingira asilia ya Amani ambako ndipo walikowapeleka watalii na mwaka huu wamechagua Magamba.

Anasema TFS ina mpango wa kwenda kuhamasisha elimu ya mazingira asilia kuanzia mashuleni lengo likiwa ni kuwajengea tabia ya kuithamini na kuihifadhi.

**DC LUSHOTO**

Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, January Lugangika, anasema utalii wa Ikolojia wilayani Lushoto kupitia hifadhi ya Magamba, umekuwa ni chagizo ya neema katika wilaya hiyo kwa kuwakutanisha wageni kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Anasema, mbali na faida za maji wanayoyapata kutokana na hifadhi hiyo ya Magamba, pia wananchi wamekuwa wakipata faida nyingine ya kufuga nyuki na kuvuna asali.

# Biashara katika picha



Ofisa Mkuu wa Wateja Wadogo na Wakati wa benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza matokeo ya hati fungani ya benki hiyo. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa NMB, Ruth Zaipuna. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), Emmanueli Kakwezi (kushoto), akielezea jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, kuhusu taasisi hiyo itakavyotoa elimu kwa wajasiriamali, katika maonyesho ya Nanenane yatakayofanyika Agosti 8, mkoani Simiyu. Katikati ni Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka na Kaimu Mkurugenzi  wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania(TanTrade), Bonifasi Michael. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mkazi wa kijiji cha Bukima, Musoma Vijijini mkoani Mara, Ladislaus Manumbu na vijana wake wakihudumia shamba lao la mihogo aina ya mkombozi ambayo inasadikiwa kuwa inahimili magonjwa. **NA MPIGA PICHA WETU**

UCHUMI

# Safari mpya SADC kuibua Utalii wa Ukombozi nchini

• Simulizi ndefu tangu jumuiya hiyo kuzaliwa



Nyumba aliyotumia Samora Machel, iliyoko katika kambi ya Nachingwea.

**INATOKA UK.13**

Juhudi za Mwalimu Nyerere, ziliwezesha kufanyika kwa Mkutano Mkubwa wa iliyokuwa chombo cha ukombozi kiitwacho Pan African Frontiline Movement of East Central and Southern Africa (PAFMECA), katika Jiji la Mbeya.

Pia, Rais Mstaafu wa Zimbabwe, Robert Mugabe alifanya mikutano yake ya harakati, katika zama hizo za kusaka uhuru wa nchi yake.

Mwalimu Nyerere alipopata fursa katika Mkutano wa iliyokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), aliwasilisha ajenda ya ukombozi kwa nchi zilizokuwa huru za Afrika na wakaazimia Tanzania kuwa kitovu cha ukombozi mwa Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika.

Tangu wakati huo, Tanzania ilikuwa nyumbani kwa harakati zao na waliwezeshwa kupata misaada kutoka nchi wanachama wa OAU (sasa AU). Aidha, walikuwapo watoaji msaada kutoka nje ya Afrika, nchi za Scandinavia, China, Cuba na Urusi (USSR).

Wakati huo, nchi hizo zilizokuwa hazijapata uhuru ni pamoja na Afrika ya Kusini, Angola, Comoro, Msumbiji, Namibia na Zimbabwe.

Ni zama baadhi ya nchi zilikuwa huru, lakini ziliandamwa na migogoro ya hapa na pale na kuzalisha makundi makubwa ya wakimbizi waliokimbilia na kuishi Tanzania.

Hao wanatoka nchi kama Malawi, Burundi, Rwanda, Kongo DRC na Uganda.

Pia, Tanzania ilishiriki kuunga mkono wapigania uhuru wa vikundi vya Polisario wa Morrocco na Palestine Liberation Organization (PLO) wa Palestina.



Baadhi ya makazi mengine ya wapigania uhuru, yaliyokuwapo Kongwa, Dodoma.

> **"Tanzania, pia ina historia ya kuwa na ofisi za ukombozi Afrika na wanaharakati wake.**

Kutokana na historia ya Ukombozi, Tanzania inalazimika kutambua na kuweka kumbukumbu, kuhifadhi na kuutangaza ili isifutike kwa wote waliopata uhuru. Ili historia ya uhuru wao ikamilike, ni lazima kuitaja Tanzania kama rafiki aliyesaidia wao kujikomboa.

**URITHI WA UTAII**

Umuhimu wa Tanzania katika ukombozi wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, urithi wa utalii wa ukombozi wa bara hilo unaelezwa unapaswa kuenziwa kwa manufaa ya wanufaika, yaani nchi zilizopigania uhuru wao, wakiwa uhamishoni Tanzania.

Mratibu Msaidizi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere na Mkuu wa Mkoa Mstaafu, Gallus Abeid, anasema kuuenzi ukombozi wa Afrika, Tanzania ina mchango mkubwa sana katika historia hiyo na fursa ya kuwa na utalii wa ukombozi, hali itakayowaletea tija, kama zilivyo nchi anazozitaja; Misri na Israeli.

Abeid anakadiria utalii wa ukombozi utavutia watu milioni 300, wanachama wa Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambako wanajua historia zao hazikamiliki bila ya kuwapo nafasi ya Tanzania.

Anasema, kwamba ni jambo litakalowasaidia vijana wa sasa na vizazi vijavyo wasioelewa maana ya ukombozi, kilichofanywa na wazazi wao na waasisi wa mataifa hayo, katika kuzikomboa nchi zao.

Mzee Abeid anasema si sahihi kwa kudhani maeneo hayo yatatembelewa tu na walioishi nchini wakati wakipigania uhuru na kwamba, kuwapo haja ya kuutangaza utalii wa ukombozi, ili ulete matunda ya kiuchumi, kama inavyofanyika katika nchi nyingine.

Anasema, kuna majina makubwa nje ya Tanzania, ambayo wahusika katika kupigania uhuru wakiyasikia, wanakumbuka enzi za harakati, mfano nafasi ya Waziri Mkuu Mstaafu Dk. Salim Ahmed Salim;, Marehemu Brigedia Hashim Mbita,

Pia, anawataja na mashujaa wa vita waliozikwa katika makaburi ya mashujaa ya Nachingwea, Mtwara, Kongwa, Mgagao Iringa, Mazimbu, Dakawa - Morogoro na Bagamoyo.

Mwalimu Nyerere alianzisha Kambi za wapigania uhuru maeneo ya Kongwa Dodoma, Kihesa Mgagao na Chuo cha Mkwawa Iringa, Kingolwira, Kituo cha Maendeleo cha Solomon Mahalangu Mazimbu na Dakawa Morogoro. Kaole Bagamoyo, Makongorosi Chunya na eneo la Mwanjelwa Mbeya.

Tanzania ilikuwa kitovu cha vyama vikuu vya ukombozi barani Afrika African National Congress -ANC na Pan African Congress-PAC za Afrika Kuisini; Movement for People Liberation of Angola - MPLA cha Augustino Neto wa Angola; Zimbabwe African National Union - ZANU cha Robert Mugabe na Ndambaningi Sithole, pamoja na wapiganaji wao wa Zimbabwe National Liberation Army -ZANLA.

Tanzania ilikua ngome ya ukombozi wa Msumbiji (FRELIMO) chini ya Eduardo Mondlane na baadaye Samora Machel; pia chama cha Namibia cha Southern West Africa People's Organization (SWAPO) kinachoongozwa na Sam Nujoma.

Pia, kuna vyama vya wapambanaji chini ya vyama vya siasa kama vile Zimbabwe People Revolutionary Army (-ZIPA), African National Liberation Army (ZANLA); Front for Liberation of Zimbabwe (FLORIZ) cha Herbert Chitepo na Shamuyarira, nao waliishi katika kambini nchini Tanzania.

Umuhimu wa historia ya ukombozi wa Afrika, unadhihirika nchini Tanzania, kutokana na viongozi wakuu wa vyama vya

UCHUMI

# Safari mpya SADC kuibua Utalii wa Ukombozi nchini

ukombozi kama Samora Machel, Eduardo Mondlane, Augustine Neto, Robert Mugabe Thabo Mbeki, Jacob Zuma, Sam Nujoma na wengineo kuishi nchini.

Aidha, wengine kama Rais wa sasa wa Zimbabwe Emmerson Mnangwaga aliishi eneo la Kaole Bagamoyo.

Uwepo wa kambi za wapigania uhuru hapa nchini, kuliwaunganisha wao na Watanzania kuwa kama ndugu na ukarimu wa Watanzania uliwafanya kuchanganyika kiasi kwamba haikuwa rahisi kutofautisha yupi ni Mtanzania na yupi mpigania uhuru.

**SHUHUDA IRINGA**

Mama Maria Zakayo wa Mgagao, Kihesa Iringa aliishi jirani na moja ya kambi za wapigania uhuru wa Afrika Kusini.

Anasema, alikutana na mmoja wa wapigania uhuru na kuanza naye uhusiano, uliowapatia watoto wawili; mmoja yuko Afrika ya Kusini na mwingine Iringa.

Anasema, muunganiko uliopo kati ya Watanzania na watu waliokuja kwa ajili ya kuhangaika na uhuru wa nchi zao, umeendelea hadi sasa kwani baada ya kuwa na mtoto ambaye yuko Tanzania, mawasiliano yanaendelea kuimarika na historia hiyo inaendelea kudumishwa.

Tanzania, pia ina historia ya kuwa na ofisi za ukombozi Afrika na wanaharakati wake

**MZIZI WA SADC**

Historia ya SADC, inatajwa kuanzia mawazo Mwalimu Nyerere pamoja na marais Milton Obote wa Uganda na Kenneth Kaunda wa Zambia, waliona ni ushirikiano wa kiuchumi utakaozisaidia nchi za Kusini mwa Afrika katika harakati zao za ukombozi.

Njia hizo za kiuchumi zilikuwa ni barabara ya Dar-es-salaam kuanzia bandarini mpaka Zambia, Reli ya Tazara kuanzia Dar-es-Salaam mpaka Kapiri Mposhi jirani na mpaka wa Zambia na Zimbabwe.

Pia, kulikuwapo bomba la mafuta la Tanzania na Zambia (TAZAMA Pipeline) na Bomba la Mafuta la Tanzania na Uganda, ambalo halikufanikiwa, kwa kuwa Rais Milton Obote alipinduliwa na Iddi Amin.

Kufanikiwa kwa baadhi ya nchi Kusini mwa Afrika kuwa huru, kulichangia kuzaliwa kwa -SADCC, iliyobuniwa Jijini Arusha, mwaka 1979, muasisi wake, Julius Nyerere, aliyeshirikiana na marais wa Kenneth Kaunda wa Zambia, Samora Machel wa Msumbiji, Sir Seretse Khama wa Botswana, na Augustino Neto wa Angola.

Tanzania na nchi nyingine nane, zilitia saini tamko la kuanzishwa rasmi SADC, ambayo jukumu kubwa lilikuwa kuhamasisha umoja wa kisiasa ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi husika.

Mwaka 1992, Mwalimu Nyerere alikuwa mwenyekiti wa Tume ya Kusini iliyohamasisha SADCC kuwa Jumuia ya Maendeleo ya Uchumi Kusini mwa Afrika - Southern Africa Development Cooperation -SADC.

Urithi huo mkubwa wa ukombozi wa Kusini mwa Afrika, bado unahifadhiwa nchini na kuimarishwa vyema ukiwa na nafasi ya kuuchochea ukuaji wa utalii kihistoria, kuwa sehemu muhimu ya kihistoria hasa ya ukombozi wa nchi za Kusini.

Ni nafasi sasa kwa wadau mbalimbali wa historia, wizara ya maliasili na utalii, watafiti, wasomi na wataalamu wa masuala ya ukombozi wakakaa pamoja na kuanzisha mkakati kabambe wa kutumia historia ya ukombozi wa Afrika kama moja ya vyanzo vya mapato lakini pia itambulike kama sehemu muhimu ya kihistoria.



Makazi aliyotumia Samora Machel, katika kambi ya Kongwa.

> “Kulikuwapo bomba la mafuta la Tanzania na Zambia (TAZAMA Pipeline) na Bomba la Mafuta la Tanzania na Uganda, ambalo halikufanikiwa, kwa kuwa Rais Milton Obote alipinduliwa na Iddi Amin.



Makaburi ya wapigania uhuru wa Msumbiji, Zimbabwe na Afria Kusini, yaliyoko Kongwa, mkoani Dodoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO**.

BIASHARA

# Brela yaeleza itakavyotinga Nanenane Simiyu na ajenda ya usajili kidigitali

**Na Sabato Kasika**




Watumishi wa Brela wakiwa kwenye banda lao la kutolea elimu kwenye maonyesho ya Nanenane, huku askari wa Jeshi la Wananchi wakisoma vipeperushi vyao, mjini Bariadi. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU**

KATIKA kufanya biashara, kuna taratibu na fursa za kisheria, ambazo mjasiriamali au mfanyabiashara anatakiwa kutambua na kuzingatia kabla na hata baada ya kuwekeza katika biashara anayotaka kufanya.

Miongoni mwake ni usajili majina ya biashara, kampuni, alama za biashara. Nchini, mwenye mamlaka ya kufanya hivyo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela).

Brela imekuwa ikizunguka katika mikoa mbalimbali nchini kuwaelimisha wananchi kutambua fursa za kisheria katika kuanzisha biashara na pia kusajili majina ya biashara.

Mbali na kuzunguka katika mikoa mbalimbali, kila mwaka taasisi hiyo ya inashiriki katika maonyesho ya Wakulima kitaifa, kwa ajili ya kusajili alama za biashara, leseni za viwanda, biashara, usafirishaji wa mifugo na mazao ya chakula ndani na nje ya nchi.

Katika maonyesho ya Nanenane ya mwaka huu yanayoendelea kwenye viwanja vya Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu, Brela ni miongoni mwa washiriki zaidi ya 300.

Emmanuel Kakwezi, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, anafafanua kuwa wamejipanga kutoa elimu kuhusu shughuli zinazofanywa na taasisi hiyo ya serikali.

Kakwezi anasema, siyo mara ya kwanza Brela kushiriki Nanenane, kila mwaka inashiriki kuona shughuli kilimo, ufugaji na uvuvi zisiwe zinakidhi mahitaji ya nyumbani.

Anasema hoja yao ni kilimo kiwe cha kibiashara, hivyo ni nafasi ya pekee kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa kutumia Nanenane kupata elimu toka Brela, kwa kuzingatia kuwa kila mwaka wanaongezeka wafanyabishara wapya.

**IKOJE ELIMU?**

"Kila mwaka tunashiriki, kwa kuwa bado wapo baadhi ya wananchi wasio na uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa kurasimisha majina ya biashara na kampuni," anasema.

Kakwezi anasema, watumishi wa taasisi hiyo pia wamekuwa wakizunguka mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kazi hiyo na sasa maonyesho hayo ya Nanenane.

|"Vilevile tunawashauri wafanyabiashara wasiishie kusajili tu jina la biashara, bali pia waende katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kupata Namba ya Mlipa Kodi (TIN), pia waendelee katika halmashauri zao kupata leseni ya biashara," anasema.

Anahimiza umuhimu kwa wote wanaotumia majina ya biashara yaliyosajiliwa, ndio maana wanatoa elimu na kurasimisha majina ya biashara na kampuni kwa vile wengi wao wanafanya biashara bila kuzingatia hilo.

"Ninaweza kusema kwamba hii ni habari njema kwa wakazi wa mikoa ya kanda ya ziwa, wajitokeze kwa wingi kusajili majina ya biashara, kampuni, usajili alama za biashara na huduma za usajili wa haki miliki, usajili leseni za viwanda, usajili leseni za biashara," anasema.

> "Elimu inayotolewa na Brela inasaidia wananchi kuepuka utapeli uliowahi kufanywa na wasio waaminifu, kwa wanaotaka kusajili kampuni na majina ya biashara.

Kakwezi anataja masharti ya mtu binafsi na kampuni, katika maombi ya leseni ya biashara kununua na kusafirisha mifugo kitaifa na kusafirisha nje ya nchi, ambayo ni muhimu yazingatiwe.

Anasema, elimu inayotolewa na Brela inasaidia wananchi kuepuka utapeli uliowahi kufanywa na wasio waaminifu, kwa wanaotaka kusajili kampuni na majina ya biashara.

Kakwezi anasema, Brela imekuwa pia ikitoa mafunzo maalumu kwa umma kujifunza jinsi ya kutumia mfumo wa usajili wa kampuni na majina ya biashara, ambao hawawezi kutapeliwa.

**LESENI BINAFSI**

Anasema ni lazima mhitaji awe na cheti cha usajili wa wadau wa sekta ya nyama kutoka Bodi ya Nyama Tanzania, kitambulisho cha mwombaji wa leseni na hati ya mlipa kodi TIN namba ya biashara.

Kakwezi anataja kingine kuwa ni utambulisho wa kuwa ana mahali pa kufanyia biashara ikiwamo mkataba wa pango wa ofisi, leseni ya makazi au hati na cheti cha kibali.

"Hayo ni masharti ya muhimu kwa mtu binafsi anayekata leseni ya kufanya biashara ya kununua na kusafirisha mifugo kitaifa na kusafirisha nje ya nchi, ambayo kimsingi ni muhimu kuyazingatia," anasema.



Watumishi wa Brela wakiwahudumia wateja wao kwenye banda lao jana, katika maonyesho ya Nanenane.

**KAMPUNI, MAJINA, BIASHARA**

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela anasema wahusika wanatakiwa kuwa na hati ya kuandikishwa kama kampuni, mkataba wa makubaliano kati ya wabia na hati ya TIN.

"Wanatakiwa kuwa na cheti cha usajili wa sekta ya wadau wa nyama kutoka Bodi ya Nyama Tanzania cheti cha kibali cha kodi kutoka TRA, mkataba wa pango wenye mihuri ya mwanasheria na kodi iwe imelipwa na uthibitisho wa uraia wa wenye hisa," anasema.

Anasema, hatua hiyo pia inalenga kuhimili ushindani uliopo katika soko la Afrika kwa kuzingatia ubora wa bidhaa zinazotengezwa nchini, hivyo wao kama taasisi ya serikali wanawajibika na umakini.

"Brela pia imekuwa ikiandaa mafunzo kwa wafanyabiashara na umma kwa ujumla kuhusiana na kupata huduma za usajili kwa njia ya mtandao ikiwamo kuwajengea uwezo katika ulipaji wa madeni kwa wateja wao," anasema.

Anasema wanaendelea kuweka mikakati, ambayo itawasaidia wafanyabiashara kuondokana na changamoto mbalimbali, ambazo zimekuwa zikiwakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.





Mkazi wa jiji akimsaidia mwendesha guta kulisukuma, huku likiwa limesheheni mzigo katika Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala Sharif Shamba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanaofuja fedha za ushirika watumiwa salamu

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imeanza kuwatolea macho viongozi wa vyama vya ushirika ambao wanatumia vibaya fedha za vyama kwa maslahi yao binafsi, na kwamba watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Angalizo hilo lilitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Kivuma Msangi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa kikao cha Baraza la Madiwani, na kusema wameanza kufuatilia vyama hivyo kama sehemu ya majukumu yao kuhakikisha fedha zinazopatikana kwenye ushirika zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kivuma alisema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya viongozi wa kufanya matumizi mabaya ya madaraka ikiwamo matumizi mabaya ya fedha ambapo hujilipa posho za safari na vikao bila kufuata utaratibu.

"Halmashauri tumejipanga kikamilifu kufuatilia mienendo vya vyama vya ushirika ili kuhakikisha usalama wa fedha na miongozo unafuatwa hasa kwa viongozi ambao wana maslahi yao binafsi ni wajibu vyama hivyo kuwanufaisha wakulima," alisema Kivuma.

Alisema baada ya kufuatilia na kubaini ubadhirifu kwa viongozi wa vyama vya ushirika na Amcos, watafikishwa kwenye vyombo vya sheria kujibu tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka.

Awali, Diwani wa Viti Maalum Kata ya Igurusi, Lucy Ngondo, alisema baadhi ya Amcos na Mamcos vimefungwa kwa sababu ya malimbikizo ya madeni.

Alisema miongoni mwa sababu zilizosababisha ni usimamizi mdogo wa viongozi wa hasa kwenye masuala ya fedha na kutolea mfano wa Saccos ya Chimala ambayo imefungwa kwa sababu ya kudaiwa na taasisi za kifedha. Aliishauri serikali kuliangalia upya suala la viongozi wanaoteuliwa kusimamia vyama wilayani Mbarali kutimiza majukumu yao kama inavyotakiwa badala ya kuwa sehemu ya kukwamisha maendeleo ya vyama.

Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Daniel Kamwela, alisema changamoto inayosababisha vyama vya ushirika vilivyo vingi kufungwa na kufa ni wanachama kutorejesha mikopo kwa wakati.

Alisema katika kukabiliana na changamoto ya malimbikizo ya madeni na hatimaye Saccos na Amcos kufungwa, viongozi wa vyama wilaya walishauri vyama kuweka sera mathubuti na kufanya marekebisho ya mikataba ya mikopo ili kudhibiti wakopaji korofi.

Alisema kuishia Juni 30, vyama vya ushirika wa akiba na mikopo tisa vya Madibira Saccos, Mkunywa, Mbarali Teachers, Kongolo Quary na UWACHI vilikuwa na sera za mikopo ambazo zimeidhinishwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na kufanya marekebisho ya mikataba yao. "Vyama vya ushirika wa akiba na mikopo sita viliingia mikataba ya mawakala wa kukusanya madeni kutoka wanachama waliokiuka kurejesha mikopo ambapo kwa mwaka 2018/2019 kuishia Juni 30 jumla ya Sh. milioni 103 zilikuwa zimekusanywa na mawakala wa kudai madeni kutoka katika vyama vya ushirika," alisema Kamwela.

# Wanahabari wafundwa kuripoti uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Mwalimu Nyerere ambayo inajihusisha na masuala ya kudumisha amani, umoja wa maendeleo ya watu wote ikiwa ni sehemu ya kuenzi misingi aliyoiacha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, imewakumbusha waandishi wa habari mkoani hapa kuzingatia uzalendo na maadili kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Akizungumza jana jijini Mbeya wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya, yalikuwa na lengo la kuwakumbusha kuzingatia ujenzi wa amani kabla, wakati na baada ya uchaguzi, Prof. Francis Matambalya kwa niaba ya Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, alisema ili watekeleza majukumu yao bila changamoto, lazima wazingatie sheria na taratibu za nchi.

Alisema waandishi wanapaswa kuzingatia maadili ya kazi zao ambayo yawapa mwongozo wa mambo gani wanayopaswa kuyafanya kwenye kipindi cha uchaguzi, ili jamii iweze kuhabarishwa kile kinachoendelea kuanzia mchakato wa uchaguzi na uchaguzi wenyewe.

Alisema Taasisi ya Mwalimu Nyerere imekuwa mstari wa mbele katika kuikumbusha jamii kuenzi na kufuata misingi aliyoicha Mwalimu Nyerere ambayo inalenga kulinda amani ya nchi na kila mmoja kuwajibika kwa nafasi yake katika kuliletea taifa maendeleo.

"Taasisi yetu haifungamani na upande wowote wa chama cha siasa, lakini kwa kutambua na kuenzi yale aliyoyaacha mwasisi wetu tunaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wanahabari kudumisha amani, umoja na mshikamano ili kujiletea maendeleo," alisema Prof. Matambalya.

Aliwashauri kipindi cha uchaguzi kuzingatia matumizi ya lugha zenye staha kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa jamii pia uchambuzi wa kina wakati wa kuandika habari ili kuwasaidia wasomaji kuzielewa habari zinazochapishwa kuepuka ushabiki na uchochezi.

Ofisa Programu kutoka Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Edgar Mwandemani, aliwakumbusha waandishi wa habari kuzingatia Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ambayo inawataka kutimiza wajibu wao kwa kufuata sheria.

Alisema waandishi ni wadau muhimu hasa kuwahabarisha wananchi juu ya mambo yanayotokea na kusisitiza kabla ya kuandika habari, wanapaswa kujiridhisha ili kuepuka mkang'anyiko.

"Waandishi wa habari ni wapishi ambao wana jukumu la kutulisha chakula kitamu na chenye ladha na ili chakula kiwe kitamu, lazima kuwapo na maandalizi ambayo yatasababisha chakula kiwe kitamu taifa linawategemea," alisema Mwandemani.

Mwandishi Mkongwe kutoka Gazeti la Raia Mwema, Felix Mwakyembe, aliwataka wanahabari kujiandaa vyema katika kipindi hiki cha uchaguzi ikiwamo kuwa na uelewa wa kutosha juu ya masuala ya uchaguzi.

# Wanawake walia ukatili wa wafugaji

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WANAWAKE wanaojihusisha na kilimo katika Wilaya ya Chunya, wamelalamikia kupigwa na fimbo na wafugaji wanaochunga mifugo ili kulisha mifugo kwenye mashamba.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Marryprisca Mahundi, wakati wa akifungua mkutano wa mradi wa uboreshaji na usimamizi wa rasilimali za umma kwenye sekta ya kilimo na mifugo unaotekeleza na asasi za kiraia, alisema alipokea malalamiko kutoka kwa wanawake wakulima wakidai wawapo mashambani wafugaji huwapiga fimbo ili wapate nafasi ya kuingiza ng'ombe kwenye mashamba.

Alilaani kitendo hicho kwa madai ni uvunjifu wa haki za binadamu pia ni ukatili wa kijinsia na kuapa wafugaji wote wanaohusika na vitendo hivyo tayari wamejulikana, hivyo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alizitaja kata ambazo wafugaji wake wanafanya vitendo hivyo ni Upendo, Mamba, Lualaje, na kwamba ufuatiliaji unaendelea ili kuwakamata wahusika.

Aliwashauri wafugaji kuacha mara moja tabia hiyo, na kwamba endapo vitendo hivyo vya udhalilishaji na vipigo kwa wanawake vikiendelea, hakutakuwa na maana ya kuwapo kwa jukwaa la wakulima na wafugaji ambalo jukumu lake ni kuwatetea.

Katibu Mtendaji wa mashirika yasiyo kuwa ya kiserikali Mkoa wa Mbeya (MBENGO-NET) anayejishughulisha na kukuza utawala bora na uwajibikaji kwa jamii, Paulo Kitha, alisema vipigo vya wanawake havikubaliki, na kwamba mradi wa uwajibikaji ambao unalenga kuongeza ushiriki wa wananchi katika kuchangia miradi ya maendeleo katika sekta ya kilimo na mifugo, utasaidia kumaliza changamoto hizo.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Chunya, James Kidayi, aliwataka wanaojihusisha na vitendo hivyo kuacha haraka mara moja.





# Wakazi wa Tambukareli wapatiwa viwanja

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa viwanja mbadala 144 ambavyo vyenye thamani ya Sh. bilioni nne kwa wananchi wa mtaa wa Sechelela Kata ya Tambukareli ili kufidia maeneo yao yaliyochukuliwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA). Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema jana kuwa wananchi hao ni kati ya 5,000 waliokuwa wamechukuliwa maeneo yao walikuwa wakiishi mtaa wa Sechelela bila kupewa maeneo mbadala.

"Wakazi hawa ambao tumewapatia viwanja watalipia kiasi cha Sh.700,000 kwa miezi sita gharama ambazo kwa kila mtu ataweza kununua kiwanja, lakini kama tungeamua kuviuza viwanja hivyo, basi kila mwananchi angetakiwa kutoa Sh. milioni saba na tungepata Sh. bilioni nne," alisema Kunambi.

Alisema mpaka sasa wametoa viwanja mbadala 3,000 kati ya 5,000 ambavyo wanatakiwa kuvitoa na lengo ni kuhakikisha wananchi wote wanapatiwa viwanja. Alisema kuwa kutokana na hali hiyo wananchi hao watakiwa kulipa fedha hiyo katika kipindi cha miezi sita, huku akiwasisitiza kulipa fedha hiyo kwa muda ili kumiliki ardhi.

Hata hivyo, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja na miezi minane mpaka sasa Jiji limefanikiwa kupima viwanja 112,000.

Diwani wa kata hiyo, Juma Mazengo, aliishukuru serikali kwa kutambua kilio cha wananchi na kuwapatia viwanja mbadala katika eneo la kielimu la Nala.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Sechelela, Norbet Pangaselo, alisema mgogoro wa eneo hilo umedumu kwa muda wa miaka minne bila kupatiwa ufumbuzi, lakini katika hatima yake imepatikana baada ya kukabidhiwa viwanja hivyo.



Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), Dk. Abdalah Seni, akimkabidhi vifaa vya elimu mwanafunzi Shikila Kisuda wa Shule ya Sekondari Ntyuka ya jijini Dodoma jana. Mhadhiri huyo, alikabidhi vifaa hivyo ili kuunga mkono juhudi za serikali kutoa elimu nchini bila malipo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viatu vya nje vyaliteka soko la ndani

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

JOZI milioni 40 za viatu zimekuwa zikiingizwa kila mwaka nchini, huku uzalishaji wa ndani ukiwa ni jozi milioni 1.3, kiwango ambacho kinatakiwa kuongezeka ili kudhibiti soko la ndani.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Bidhaa za Mifugo, Usalama wa Chakula na Lishe kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gabriel Bura, kwenye mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi yaliyoandaliwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Dodoma.

Bura alisema viatu vinavyoingizwa nje ya nchi vinateka soko la ndani na kwamba kiwango cha uzalishaji wa bidhaa za ngozi bado ni kidogo na kuwataka wazalishaji kuungana ili kuzalisha bidhaa nyingi za ngozi ikiwamo viatu vyenye ubora ili kuweza kuliteka soko.

"Ni jambo la kufurahisha kuona wazalishaji wadogo wanaweza kuzalisha bidhaa za ngozi na ule mnyororo wa thamani unaongezeka," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwamo asilimia 35 ya kodi kuongezwa kwenye bidhaa za mtumba na serikali kuondoa kodi kwenye bidhaa za kusindikia. Alieleza wanaendelea kufanya kazi kuona wazalishaji wanachukua hatua mbalimbali, lakini kuna changamoto ikiwamo ubora wa bidhaa zinazozalishwa, wengi wanafanya kazi bila kuwa na hakimiliki.

Aliwataka Watanzania kuwa na utamaduni wa kununua bidhaa za ndani huku akidai kuwa wizara hiyo imeanzisha dawati la sekta binafsi ambalo huunganisha wazalishaji na benki ya kilimo.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Msaidizi Sekta ya Uchumi Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba, akifunga mafunzo hayo, alisema Sido imekuwa ikiunga mkono juhudi za serikali kutekeleza Sera ya Tanzania ya viwanda.

Alisema bidhaa nyingi za ngozi zinazotengenezwa zimekuwa na ubora, hivyo kuwataka wahitimu hao kutumia fursa ya mafunzo waliyoipata kwa kuanzisha viwanda vidogo na kuboresha kazi zao ili kuweza kukabiliana na soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema Jiji la Dodoma limetoa zaidi ya Sh.bilioni mbili kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali, hivyo watumie fursa hiyo kuwekeza kwenye sekta ya ngozi. Awali, Meneja Miradi wa Sido Mkoa wa Dodoma, Stephano Ndunguru, alisema shirika hilo linafanya jitihada kuhakikisha watu wengi wanapata mafunzo hayo.

Alisema kwa mwaka 2018/19 wameweza kutoa mafunzo kwa vijana 124 kupitia kozi nne na wengine wameweza kujiajili na wanazalisha bidhaa.

# Watakiwa kuchangia sekta elimu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JAMII imeshauriwa kuendelea kuiunga mkono serikali kwa kuchangia elimu ili kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi wenye mazingira magumu.

Ushauri huo ulitolewa jana na mdau wa elimu nchini na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Ombeni Msuya, wakati wakukabidhi vifaa vya elimu kwa wanafunzi wanaotoka kwenye familia zenye mazingira magumu wa Shule ya Sekondari Ntyuka iliyopo jijini hapa.

Dk. Msuya alisema jamii inatakiwa kuiunga mkono serikali katika kutoa huduma ya elimu kwa kuchangia vifaa na vitu mbalimbali ili kuwawezesha wanafunzi kuipenda elimu.

"Serikali ilipotangaza elimu bila malipo haikumaanisha kuwa kila kitu mwanafunzi atapatiwa bure, ilimaanisha kuwa ilibeba baadhi ya mahitaji kama ada na gharama zingine, lakini hata sisi watu wengine tunatakiwa kuunga mkono kwa kusaidia wenzetu katika kupatia elimu," alisema.

Alivitaja vifaa vya elimu walivyochangia kwa wanafunzi wa shule hiyo kuwa ni madaftari, kalamu, vifuti na sare za shule.

Alibainisha kuwa jinsi ya kuwapata wanafunzi hao wahitaji wamekuwa wakishirikiana na wakuu wa shule husika pamoja na viongozi wa kijamii ili kuwatambua.

Aidha, alisema jinsi ya kupata vifaa hivyo wamekuwa wakichangisha kutoka kwa marafiki zao na wadau wengine wa elimu kwa kupewa vifaa moja kwa moja au fedha.

Mdau mwingine, Dk. Abdalah Seni, Mhadhiri wa Udom, alisema wamekuwa wakisaidia maeneo mbalimbali nchini.

Alisema walianza na Mkoa wa Dodoma, lakini wameweza kusaidia vifaa hivyo katika mikoa ya Pwani na Lindi na mpango uliopo ni kuendelea na maeneo mengine kutokana na vifaa wanavyopata.

Dk. Seni alisema lengo la kutoa misaada hiyo ni kutoa motisha kwa wanafunzi wanaotoka familia maskini kupenda kujifunza na kuongeza ufaulu kwa baadhi ya shule.

"Kuna baadhi ya shule tulikuta mwanafunzi hafiki shule kwa sababu hana daftari za kuandika pamoja na kalamu, lakini baada ya kuwapatia vifaa hivyo waliweza kufanya vizuri katika masomo yao na kuacha utoro," alisema.

Mkuu wa Shule ya Ntyuka, Anitha Mgaya, aliwashukuru wadau hao wa elimu kwa kuona umuhimu wa kuisaidia shule yake. Aliwaomba wadau wengine kuendelea kuikumbuka sekta ya elimu na hasa wanafunzi hao wanaotoka kwenye mazingira magumu ili waipende elimu.





# Uhamiaji yatakiwa kuongeza kasi utoaji pasipoti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI mbalimbali wanaofuata huduma katika Idara ya Uhamiaji Zanzibar wamewataka watendaji wa idara hiyo kuongeza kasi ya utendaji wa kazi hasa katika suala la upatikanaji wa hati za kusafiria.

Waliyasema hayo huko makao makuu ya idara hiyo Kilimani Mjini Zanzibar wakati Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Injinia Hamad Yussuf Masauni, alipofanya ziara katika idara hiyo.

Walisema licha ya kazi ngumu wanazofanya watendaji hao, lakini wazidi kuongeza kasi kwa kuwa idadi ya wananchi wanaofika katika idara hiyo kupata huduma ni kubwa.

Akizungumza mbele ya Naibu Waziri Masauni, mwananchi mmoja Muhammad Muhamed, mkazi wa Tomondo, alisema wanatumia muda mwingi kusubiri huduma idarani hapo.

"Tunajua kuwa wafanyakazi wa idara hii wanakazi nzito hasa katika suala hili la ubadilishaji wa hati za kusafiria wa mfumo wa kielektroniki, lakini waongeze kasi maana tumekuwa tunatumia muda mwingi wakati na sisi tunamajukumu yetu mengine," alisema.

Vile vile, alisema kama watendaji ni kidogo ni vyema serikali ikaongeza wafanyakazi katika idara hiyo ili wananchi waweze kupata huduma kwa haraka.

"Zaidi ya saa mbili nipo hapa nasubiri huduma, huku shughuli zangu zingine za kiuchumi zikiwa zimesimama," alisema.

Naye Hawa Said alisema kuwa zoezi la ubadilishaji wa hati za kusafiria wa kielektroniki limekuwa na usumbufu kwao.

Alisema zaidi ya mwezi mmoja sasa anafuatilia hati yake ya kusafiria, hivyo ameiomba serikali kuharakisha zoezi hilo ili hati hizo ziweze kupatikana kwa muda mchache.

"Ni kweli wafanyakazi wanajitahidi kutuhudumia, lakini sijui tatizo ni nini tumekuwa tukichukua muda mrefu wa kupata hati za kusafiria," alisema.

Kwa upande wake Masauni aliwataka watendaji hao kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuondoa changamoto zilizoelezwa na wananchi hao.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni akizungumza na wananchi waliofika Makao Makuu ya Uhamiaji Visiwani Zanzibar jana, kupata pasi za kusafiria za kielektroniki. Wa pili kulia ni Kamishna wa Uhamiaji, Johari Suluhu. **PICHA: WMNN**

# Viongozi watunza fedha waonywa dhidi ya tamaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa vikundi vya ushirika wanaopewa dhamana ya kutunza fedha wametakiwa kutotawaliwa na tamaa kwa kupora akiba inayochangwa na wanachama na baadaye kuwakimbia.

Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Makame Shams, akizungumza na wanachama wa vikundi vitatu vilivyomo kwenye wadi ya Sogea jimboni humo, alisema kupora fedha za wanachama ni zambi na dhuluma isiyoweza kusameheka.

Akielezea kusikitishwa na tabia hiyo, alisema baadhi ya viongozi na wanachama wanaoaminiwa wanasahau malengo ya kuanzishwa vikundi vya ujasiriamali na kuweka akiba, ambayo ni kuwakomboa wananchi na umaskini.

Vile vile, alisema kupoteza uaminifu na kuvifilisi vikundi hivyo, kunakwenda kinyume na Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inayotilia mkazo kuwawezesha wananchi ili kujiajiri kwa kuwa ajira serikalini hazitoshi kwa kila mtu.

"Kuna kikundi kimoja hivi karibuni, kilipata mtihani kwa kiongozi wao kutoweka na zaidi ya Sh. milioni saba na hadi sasa hakuna anayejua wapi alipo huku wanachama wakiwa wamebaki na majuto," alieleza Shamsi. Hata hivyo, mwakilishi huyo alisema pamoja na changamoto zinazovikabili vikundi mbalimbali katika jimbo lake, ataendelea kushirikiana na uongozi wote wa jimbo kuhakikisha vinastawi ili visisambaratike kama ilivyokwisha kutokea katika maeneo mengine.

Kwa upande mwingine, Shamsi aliwataka vijana wanaomaliza masomo katika ngazi ya sekondari na vyuo, kujikusanya pamoja na kuomba mikopo katika taasisi mbalimbali zinazowezesha vikundi vya ushirika badala ya kukunja mikono wakisubiri ajira za serikali ambazo ni chache.

Pia, aliwahimiza kuvisajili vikundi vyao ili vitambulike rasmi, akisema kufanya hivyo kutarahisisha kupata mikopo na hata misaada kwa ajili ya kujiimarisha na hivyo kutengeneza mustakabali mzuri wa maisha yao.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa vikundi vinavyojishughulisha na kazi za ufundi kama vile useremala, kujisajili ikizingatiwa kwamba Wizara ya Biashara na Viwanda ina utaratibu wa kuviwezesha kitaalamu kupitia mfuko wa viwanda vidogo chini ya taasisi ya SNIDA.

"Kiwanda ukikisajili, kuna fursa ya kukopeshwa mashine unayoitaka ya kuendeshea shughuli zako za uchongaji kwa teknolojia ya kisasa, lakini kwa mazingira yanayoonekana ni vigumu sana kupata vitu hivyo. Jisajilini na mimi ninaahidi kukuunganisheni na taasisi kama hizo ili mfike mbali," alisema.

Akizungumzia kikundi cha kuweka akiba, aliwasisitiza umuhimu wa wanachama wanaoomba na kupata mikopo, kuhakikisha wanalipa kwa wakati ili mtaji uweze kuzunguka na kuwanufaisha wengine, vinginevyo watavivua vikundi vyao.

Aliwaomba wanachama wanaokabidhiwa dhamana ya kutunza fedha kufanya kazi hiyo kitaalamu na kuziweka benki, lakini alikataa utaratibu wa kutoa usimamizi wa zaidi ya watu wawili wanaoaminika.

Mwakilishi huyo alikabidhi jumla ya Sh. 1,500,000 kwa vikundi vitatu vilivyomo jimboni humo kwa lengo la kuvipa msukumo wa kutekeleza majukumu yao kama Ilani ya CCM inavyoelekeza, ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wake baada ya awali kuvikabidhi vikundi 23 msaada kama huo.

Naye Diwani wa wadi ya Sogea, Mohammed Said Mohammed, alimshukuru mwakilishi huyo, huku akiwasisitiza wanachama wa vikundi vilivyopata fedha hizo kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na kuahidi kuongeza pale atakapoona utendaji mzuri wa shughuli zao.

Kwa upande wao wanachama wa vikundi hivyo walieleza changamoto mbalimbali zinazowakabili, ikiwamo uhaba wa mitaji, ugumu wa kupata mikopo, vitendea kazi pamoja na ukosefu wa elimu ya kuendesha miradi na Shamsi aliahidi kuzitafutia ufumbuzi.

# Wajasiriamali watakiwa kuchangamkia mkutano wa SADC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amewataka wajasiriamali wa Zanzibar kuitumia fursa ya maonyesho ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ya wiki ya viwanda inayotarajiwa kufanyika katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam.

Akizungumza ofisini kwake Migombani, alielezea umuhimu wa kushiriki kwa wawekezaji wa viwanda, wajasiriamali wa Zanzibar na jinsi watavyojitangaza kupitia mkutano huo ambao utaanza Agosti 4 hadi 9, mwaka huu.Alisema Wazanzibari wanaweza kushiriki katika wiki ya viwanda kwa kutangaza bidhaa zao ambazo zina kiwango na kujulikana ndani ya soko kwa kupitia maonyesho hayo.

Alisema Zanzibar kuna fursa nyingi kwa upande wa SADC na kuwataka wafanyabiashara, wajasiriamali kutoa bidhaa zinazokuwa na mvuto ikiwamo mwani, vanilla, mafuta ya karafuu, mafuta ya nazi na baadhi ya bidhaa nyingine adhimu za Zanzibar.

"Tuacheni woga tutangaze biashara zetu, wajasiriamali waonyeshe mambo ya Kizanzibar yenye mvuto yakiwamo ya utalii, spice (viungo) za kila aina tulizonazo hapa Zanzibar," alisema.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kutumia fursa ya kufanya mambo mengi katika wiki hiyo ambayo yatasaidia kutangaza biashara na milango iko wazi ya kuendeleza sekta ya biashara nchini. Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda, Juma Hassan Reli, alisema SADC ni Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika ambao umoja wake umeundwa kwa kurahisisha wafanyaji biashara na kuweka vigezo mbalimbali vya kuichumi.

Aliwataka wafanyabiashara kuwa na uwiano wa kodi ili kuweka umoja wa soko na uchumi kwa kubadilishana uzoefu na kuingiza kipato.

Alisema wageni wanaokuja ni viongozi wakuu wakiwamo mawaziri makatibu na marais na hiyo ni nafasi pekee ya kujitangaza kupitia wageni hao kwa kununua bidhaa zao.

Kwa upande wao wafanyabiashara wa Zanzibar walisema wamefarijika na uwapo wa maonyesho ya wiki ya viwanda Tanzania kwa kuwa watajitangaza na kupata utaalamu, kubadilishana mawazo na kujenga uhusiano na wafanyabiashara na wajasiriamali wenzao kutoka nchi mbalimbali.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine (wa pili kulia), akikabidhiana mkataba wa makubaliano na Mkuu wa Kitengo cha Biashara toka Benki ya Stanbic, Fredrick Max (wa pili kushoto), kwenye kikao jijini Dar es Salaam lengo ikiwa ni kutoa mikopo ya vifaa na nyenzo za kilimo kwa wafanyakazi wa sekta za umma na binafsi ili kukuza sekta ya kilimo na mifugo hapa nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri zatakiwa kujenga shule mabweni

**Restuta Damian,** BUKOBA

WADAU wa elimu Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera wameshauri kila Halmashauri ya Mkoa wa Kagera kujenga shule za bweni zitakazopokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wenye ulemavu ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi katika baadhi ya shule.

Shule hizo ni za Msingi Mugeza Museto na Mugeza Viziwi ambazo zimekuwa zikipokea watoto kutoka nje na ndani ya Mkoa wa Kagera.

Ushauri huo ulitolewa juzi wakati wa utambulisho wa mradi wa Haki Elimu kwa watoto wenye ulemavu katika Manispaa ya Bukoba, unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu hasa watoto, vijana na wanawake (TEKLA) kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS). Mradi huo utatekelezwa katika kata tano za Wilaya ya Bukoba.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mugeze Mseto, Hemed Mussa, alisema hupokea watoto wenye ulemavu kutoka Mkoa wa Kagera kwani shule hiyo yenye mchanganyiko wa wanafunzi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo upungufu wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Shule yetu imekuwa ikipokea wanafunzi wenye ulemavu wa aina zote ambao hukaa shuleni na wale wa kawaida wanaosoma na kurudi nyumbani, lakini kutokana na kutokuwapo miundombinu ya kutosha, vifaa na walimu tunalazimika kwa mwaka kupokea wanafunzi kumi tu kutoka mkoa mzima, hivyo unakuta asilimia kubwa ya wenye uhitaji wakikosa nafasi," alieleza Mussa.

Alisema sera ya elimu inasema kila mwalimu mmoja anapaswa kufundisha wanafunzi watano wenye mahitaji maalum, lakini unakuta anafundisha zaidi ya 40, yenye wanafunzi wenye ulemavu zaidi 150, huku wasioona wakiwa 42 na kwamba ina walimu watano tu wa mahitaji maalum. Alisema endapo halmashauri za mkoa wa Kagera zitakubali kutenga bajeti kuhakikisha zinajenga shule katika maeneo yao na pale watoto wenye ulemavu wa kawaida wakawachanganya na wengine katika shule zilizoko katika maeneo yao itasaidia kupunguza msongamano na jamii itawatambua.

Mkuu wa Shule ya Mugeza Viziwi, Osea Kato, alisema shule hiyo inapokea watoto wenye mahitaji maaluma na kuwafundisha masomo ya shule ya msingi, lakini shule inayochukua watoto viziwi ni hiyo ambayo ni ya bweni kwa Kanda ya Ziwa na wana uwezo wa kuchukua watoto hao wote.

"Kwa hiyo tunapoanzisha suala la elimu jumuishi kuna watoto ambao ni viziwi, lakini wana baki ya usikivu kwa maana wanaweza kujifunza kwa kusoma midomo au wakipata mashine za kuongeza sauti zao wakaweza kujifunza katika shule za kawaida ili mradi wapate walimu wenye elimu maalum wa kuwaongoza, hivyo hao wa aina hiyo wakipelekwa katika shule za kawaida au wakajengewa katika maeneo yao, itasaidia wale viziwi kabisa wapate nafasi ya kuingia katika nafasi hii," alisema Mwalimu Kato.

Mratibu wa Shirika la Tekla, Kasaaju Mugisha, alisema malengo ya mradi huo ni kuongeza uandikishwaji wa watoto wenye ulemavu katika shule za kawaida, kuongeza ushiriki na ufaulu wa watoto hao darasani. Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatusi Kinawiro, katika hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, Morce Limbe, alisema dhana ya elimu jumuishi ni pana na serikali imeweka juhudi ili kuwezesha kuwanufaisha watoto wenye ulemavu ambapo utekelezaji wake unahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali.

# Wakulima wahamasishwa kushiriki 88

**Na Mwandisghi Wetu,** SIMIYU

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imewataka wakulima na wafugaji nchini kutumia muda maonyesho ya Nanenane ambayo yanafanyika kitaifa mkoani Simiyu, kujifunza na kuchangamkia fursa za mikopo na inayotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo.

Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, alipongeza matayarisho makubwa kwa ajili ya maonyesho hayo, huku TADB ikiwataka Watanzania na hasa wakulima kushiriki kwa uwingi.

"Twendeni Nanenane Simiyu, huduma za kifedha na ushauri kwa miradi ya wakulima wadogo zitatolewa," ilisema taarifa hiyo na kuongeza kuwa kama Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini imejipanga.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, TADB imejipanga pia kukidhi haja na kutatua changamoto za upatikanaji wa mitaji na uwekezaji katika kilimo.

"Benki ya Maendeleo ya Kilimo imeleta mapinduzi na ubunifu kwa uanzisha mikopo ya wakulima wadogo chini ya udhamini wa ushirika, ufadhili wa miradi ya kibiashara ya kilimo, ukopeshaji wa jumla mikopo mseto na mikopo jumuishi na taasisi

washirika pamoja na kufadhili utafiti na kutoa ushauri wa kifedha katika kilimo," ilisema taarifa hiyo.

Ushiriki wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwenye maonyesho ya Nanenane umekuwa na manufaa makubwa kwa wakulima na wafugaji kwani hupata majawabu sahihi na suluhisho la changamoto zao.

# Wadau kilimo wafunguka upatikanaji mbolea

**Na Enock Charles**

WADAU wa kilimo wameipongeza kampuni ya mbolea ya YARA Tanzania kwa kufanikisha upatikanaji na usambazaji wa mbolea kwa wakati na kufuata bei elekezi sambamba na msimu wa kilimo mwaka 2019/20.

Walisema hayo walipozungumza baada ya mkutano jijini Dar es Salaam uliowakutanisha mawakala, wasambazaji wa mbolea wa kampuni hiyo na wadau wa kilimo kujitathmini kiutendaji kwa msimu uliopita na pia kupeana mikakati ya usambazaji mbolea kwa msimu mpya wa kilimo unaokuja.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara na Miradi wa Benki ya Mendeleo ya

Kilimo (TADB), Augustino Matutu Chacha, alisema YARA Tanzania inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima kwa wakati na kumpatia elimu stahiki ya matumizi ya mbolea hiyo na kupelekea tija ya uzalishaji mazao kuongezeka.

"TADB iliingia makubaliano na YARA katika kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima ili kuchagiza mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao nchini," alisema Chacha na kuongezea kuwa benki hiyo inaendelea kushirikiana kuhakikisha changamoto za wakulima zinapatiwa ufumbuzi. Alisema mafanikio yanayopatikana sasa katika sekta ya kilimo katika kuzalisha mazao yenye tija yanatokana na matumizi sahihi ya mbolea, elimu ya kilimo bora na upimaji wa afya ya udongo zoezi ambalo YARA imekuwa ikilifanya maeneo mengi nchini.

"Tutaendelea kushirikiana nayo kuhakikisha malengo ya nchi ya kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 inafikiwa kwa vitendo kwa kuongeza tija katika uzalishaji mazao ambayo yatachochea ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao," alisema Chacha. Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), Geoffrey Kireng, alisema uendelezaji wa sekta ya kilimo nchini unategemea ushiriki wa wadau mbalimbali katika kutekeleza azima ya serikali ya kufanya mageuzi kwenye kilimo.

"Ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma ndiyo chachu ya kuchagiza maendeleo nchini kwa hali hiyo itapelekea usawa katika utendaji na kuondoa changamoto mbalimbali zinazokwamisha maendeleo hali itakayochochea maendeleo," alisema Kirenga.

Alisema sekta binafsi ndio yenye wataalamu, teknolojia na mitaji, hivyo kwa kushirikiana na sekta ya umma kutachagiza maendeleo na kuifanya nchini kufikia uchumi wa kati na viwanda kwa kuongeza tija katika uzalishaji.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephane Ngailo, alisema mbolea ya YARA ina viwango vizuri na rafiki kwa mazingira hivyo wakulima wakiendelea kutumia mbolea hii itasaidia kuongeza tija na uzalishaji.

"YARA iendelee kutekeleza majukumu yake katika kuhakikisha mbolea zinawafikia wakulima kwa wakati na kuhakikisha ubora wa mbolea za YARA unaendelea kubaki vilevile ili tija ya uzalishaji wa mazao uendelee kuongezeka," alisema Ngailo.

## HABARI KIMATAIFA

# Wabunge wapokea kontena 'hewa' la misaada

**NAIROBI,** Kenya

KATIKA hali isiyo ya kawaida, wabunge nchini Kenya wamepokea kontena tupu lililodaiwa kuwa na vifaa vya msaada kutoka China.

Taarifa kutoka Kenya zimeeleza kuwa kontena hilo lenye vifaa vya msaada lilipelekwa katika makao ya bunge liliwasili likiwa halina kitu ndani.

China imesema tukio hili ni la kwanza kuwahi kutokea na kwamba kwa miaka mingi imekuwa ikitoa misaada ya kirafiki kwa Kenya, ikiwamo vifaa tiba, vifaa vya ofisi, msaada wa chakula na vyote vimekuwa vikiwasilishwa vikiwa salama.

Msemaji wa Jeshi la Kenya, Charles Owino, akizungumza na vyombo vya habari kuhusu tukio hilo alisema: "Sina taarifa kabisa kuhusu taarifa hizo isipokuwa nimezisikia kupitia mitandao."

"Kwa kawaida huwa tunapata maelezo kutoka kwa mkuu wa polisi na sijui kama ni mambo ya mitandao ya kijamii ama ni kweli kwa sababu sijapata taarifa kwa mkuu wa upelelezi hivyo pengine niulizie halafu baadaye tuweze kuzungumza."

Alisema hana habari kama kontena hilo liliwasili likiwa tupu.

Katika hatua nyingine, uchunguzi unaripotiwa kuidhinishwa kupitia idara ya makosa ya jinai nchini humo katika kinachotajwa na vyombo vya habari Kenya kuwa ni kubaini mazingira yaliyojitokeza ya kontena hilo kutoka China kuwasili Kenya likiwa tupu.

Tukio hili limewagusa raia wengi wa Kenya huku baadhi wakisema kuwa ni jambo lililoaibisha Kenya.

Vifaa vilivyoorodheshwa vikiwa pamoja na kompyuta mpakato, na projekta zilikuwa msaada kutoka Bunge la Taifa la China na mzigo huo ulipaswa kufikishwa Kenya kupitia ubalozi wa China nchini humo.

Katika taarifa iliyowasilishwa na Karani wa Bunge la Kenya, Michael Sialai alithibitisha kuwa kontena lililowekwa nembo ya mizigo ya kidiplomasia liliwasili Julai 30 kama ilivyotarajiwa lakini baada ya kufunguliwa, hakukuwa na kitu ndani yake.

Kwa mujibu wa Karani wa Bunge la Kenya, ubalozi wa China jijini Nairobi iliingia mkataba na kampuni ya usafirishaji iliyojulikana kwa jina M/S Bollore Africa Transport & Logistics Ltd kusafirisha kontena hilo.

"Kweli kontena liliwasili katika viwanja vya bunge Julai, 30, ambapo niliwateua maofisa kadhaa kutoka kwenye bunge waweze kuthibitisha mzigo kwa ulinganifu na kile kilichoelezwa kuwasilishwa na ubalozi wa China," alisema Sialai na kuongeza:

"Baada ya kufungua kontena, ilithibitishwa kuwa lilikuwa tupu. Wakala na maofisa wetu kwa pamoja walinifikishia suala hilo na kuamua kuwa maofisa wa DCI wapatiwe taarifa hiyo, suala ambalo lilifanyika ipasavyo". **BBC**

# Mwanajeshi Korea Kaskazini atokomea Korea Kusini

**NAIROBI,** Kenya

**Chombo cha habari cha Korea Kaskazini kilisema uzinduzi huo uliosimamiwa na Rais Kim Jong un ulikuwa ni kufanyia majaribio makombora hayo.**

MWANAJESHI mmoja kutoka Korea Kaskazini ametorokea Korea Kusini baada ya kuvuka mpaka unaoyatenganisha mataifa hayo mawili hasimu.

Mpaka huo unalindwa kwa ulinzi mkali na wanajeshi wa nchi hizo, kila moja ikijilinda dhidi ya mwenzake.

Taarifa iliyotolewa na majeshi ya Korea Kusini ilieleza kuwa mwanajeshi huyo alibainika kuvuka mpaka huo usiku.

Mwanajeshi huyo bado hajatambulika lakini kwa taarifa zilizotolewa alikuwa na hamu ya kuhamia mji wa Seoul, alisema mkuu huyo.

Inaelezwa kuwa idadi kubwa ya wananchi hutoroka Korea Kaskazini kila mwaka, lakini utorokaji kupitia kuvuka mpaka wa mataifa hayo mawili umeelezwa kuwa ni hatari.

Mnamo Novemba 2017, mwanajeshi wa Korea Kaskazini alipigwa risasi 40 na wanajeshi wenzake alipokuwa akivuka mpaka huo kutorokea Korea Kusini.

Katika tukio la hivi karibuni mtu huyo alionekana majira ya saa sita siku ya Jumatano karibu na mto Imjin, ambao maji yake hutoka Korea Kaskazini na kuelekea Korea Kusini kupitia mpaka huo unaolindwa sana Magharibi mwa Rasi ya Korea.

Alikamatwa na wanajeshi wa Korea Kusini na kuzuiliwa.

Hatua hiyo inajiri siku moja tu baada ya Korea Kaskazini kurusha makombora mawili ya masafa mafupi.

Chombo cha habari cha Korea Kaskazini kilisema uzinduzi huo uliosimamiwa na Rais Kim Jong un ulikuwa ni kufanyia majaribio makombora hayo.

Majaribio hayo yalikuwa ni onyo kwa Korea Kusini kuhusu zoezi la kijeshi la pamoja na Marekani linalotarajiwa kufanyika muda wowote. **BBC**



Wanajeshi wa Yemen wakiokoa wenzao katika kambi ya Al Jalaa baada ya kujeruhiwa na makombora yaliyorushwa na waasi wa Kihouthi na kuua watu zaidi ya 60. **PICHA: REUTERS**

# Mtoto wa kiume wa Osama afariki



**WASHINGTON,** Marekani

MTOTO wa kiume wa mwasisi wa kundi la Al-Qaeda, Osama Bin Laden, Hamza, amefariki dunia.

Taarifa iliyotolewa na maofisa wa ujasusi wa Marekani ilieleza kuwa sehemu na siku aliyofariki Hamza Bin Laden bado haijafahamika.

Februari, mwaka huu, Serikali ya Marekani iliahidi kutoa dola milioni moja kwa ajili ya mtu yeyote atakayetoa taarifa zitakazosaidia kutambua ni wapi alipo Hamza.

Hamza Bin Laden, anayedhaniwa kuwa na umri wa miaka 30, alikuwa ametoa ujumbe mbalimbali wa sauti na video akitoa wito wa kufanya mashambulio dhidi ya Marekani na nchi nyingine.

Pia aliwatolea wito wapiganaji wa jihadi kulipiza kisasi mauaji ya baba yake aliyeuliwa na kikosi maalum cha Marekani nchini Pakistan Mei 2011.

Kadhalika, alikuwa amewatolea wito watu wa rasi ya Arabia kulipiza kisasi. Saudi Arabia ilimnyang'anya uraia Machi, mwaka huu.

Hamza alikuwa katika kifungo cha nyumbani nchini Iran lakini ripoti nyingine zilisema kuwa huenda alikuwa akiishi katika mataifa ya Afghanistan, Pakistan na Syria.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilisema kuwa nyaraka zilizokamatwa katika uvamizi wa mwaka 2011 katika nyumba ya baba yake ya Abbottabad, Pakistan, zinaonyesha kuwa Hamza Bin Laden alikuwa anaandaliwa kuchukua utawala wa Al-Qaeda.

Vikosi vya Marekani pia viliripotiwa kubaini video hiyo ya harusi yake akimuoa binti wa ofisa mwingine wa ngazi ya juu wa Al-Qaeda ambayo ilidhaniwa kufanyika nchini Iran.

Baba mkwe wake alikuwa ni Abdullah Ahmed Abdullah au Abu Muhammad al-Masri, ambaye bado anatafutwa kwa madai ya kuhusika katika mashambulio ya ugaidi ya mwaka 1998 dhidi ya balozi za Tanzania na Kenya.

Al-Qaeda ni kundi lililotekeleza mashambulio mabaya ya ugaidi ya Septemba 11, 2001 dhidi ya Marekani, lakini hadhi yake kwa sasa imeshuka katika kipindi cha miongo kadhaa iliyopita baada ya kuibuka kwa umaarufu wa kundi la Islamic State. **BBC**

# CEED yaelimisha wajasiriamali usimamizi biashara ya mazao

**Na Beatrice Shayo**

KITUO cha Ujasiriamali na Maendeleo ya Utendaji (CEED) kimewakutanisha wafanyabiashara mbalimbali wa mazao ya kilimo na usindikaji wa vyakula na kuwapatia elimu ili waweze kusimamia biashara zao na kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari, mwakilishi kutoka CEED, Fred Laiser, amesema lengo la mkutano huo ni kuwapatia elimu kuhusu usimamizi wa biashara zao na kuwakutanisha na wajasiriamali kutoka nje ya nchi ili kujifunza zaidi katika sekta hiyo.

Alisema mafunzo hayo yamejikita katika maarifa ya biashara ambayo yatawasaidia kuwainua pamoja na kuchangamkia fursa za uwekezaji.

"Sisi CEED kazi yetu ni kuwainua wajasiriamali mbalimbali nchini hasa wa mazao ya kilimo pamoja na mifugo. Leo tupo hapa kwa ajili ya kuwapa elimu ya usimamizi wa biashara zao hasa zinapokuwa kubwa kwa sababu biashara inapokuwa kubwa changamoto nazo zinaongezeka," alisema Laiser.

Naye Elizabeth Swai ambaye ni mjasiriamali wa kuku, alisema amefurahia kupata mafunzo kutoka kwa wakufunzi wa kimataifa ambayo yatamwezesha kuendeleza biashara yake.

"Unapokuwa mjasiriamali kuna changamoto mbalimbali unazokutana nazo, jambo muhimu ni kutakiwa kuwa mbunifu kila wakati na kutoa huduma bora au kuwa na bidhaa zenye ushindani sokoni," alisema Swai.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kisimani, Vicent Laizer (kulia), alipotembelea maonyesho ya mwaka wa tisa ya sayansi na teknolojia yaliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Benki kuwezesha wakulima kubeba uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imesema inaendeleza jitihada zake kwa wakulima za kuwezesha sekta ya kilimo nchini inabeba uchumi wa nchi.

Pia kwa muda mrefu benki hiyo imekuwa ikitangaza kuwasaidia wakulima kama ajenda yake kuu, kutokana na asilimia kubwa ya Watanzania kutegemea na sekta hiyo.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema hayo wakati akikabidhi Sh. milioni 30 na fulana 300 kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, kama udhamini wa benki hiyo kwenye maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) kitaifa yanayofanyikia mkoani humo.

Magesse alisema, benki hiyo imekuwa haifanyi kazi ya kutunza fedha za wateja wake pekee, bali pia jamii katika nyanja mbalimbali za kilimo, ufugaji, elimu, afya na biashara.

Alisema, katika maonyesho hayo benki hiyo imejipanga kuhakikisha inatoa elimu kwa wakulima, wafugaji jinsi ya kulima kisasa na kitaalamu ikiwa pamoja na kuwaeleza jinsi gani benki hiyo inaweza kushiriki kwenye kilimo kwa kuwapatia mikopo.

"Kwenye maonyesho ya mwaka huu ambayo yatakuwa bora zaidi, ushiriki wetu kama benki utakuwa mkubwa zaidi na umelenga kuwasaidia wakulima, tutakuwa na bidhaa za wafugaji wa ng'ombe, na wakulima wa mazao ya pamba, tumbaku na kahawa, lakini hata matrekta tutakuwa nayo," alisema Magesse.

Aliwataka wakulima kujitokeza kwa wingi katika maonyesho hayo hasa kwenye banda la NMB ili waweze kupata elimu itakayowafanya walime kisasa kwa kutumia teknolojia na kuzalisha kwa tija.

Akiongea baada ya kupokea mchango huo, Katibu Tawala huyo ameishukuru benki hiyo kwa mchango wake, ambao alisema utawezesha kuboresha zaidi eneo ya Nyakabindi ambako sherehe hizo zinafanyikia.

## Serikali yaahidi kusaidia vijana

INATOKA UK. 8

teknolojia katika sekta hizi," alisisitiza waziri huyo akizindua rasmi maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya "Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa ukuaji wa uchumi wa nchi".

Aidha, aliahidi wataendelea kutoa mafunzo kwenye sekta ya ufugaji wa samaki kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi sambamba na mafunzo wezeshi katika sekta ya uvuvi, na kuahidi wizara hiyo kuendelea kushirikiana na mikoa na halmashauri zote za wilaya kuhakikisha inaboresha sehemu sahihi za ufugaji ili kuhamasisha wananchi kufanya ufugaji ulio bora hasa wa ng'ombe na mbuzi.

Alisema wana imani kwa kuziguza sekta hizo, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto ya migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa ikirudisha nyuma maendeleo ya nchi, huku kwa upande wa wakulima akihimiza wahamasishwe matumizi ya zana bora za kilimo kama vile matrekta, mashine za kupandia na kuvunia mpunga, pamoja na mashine za kupukuchua mahindi.

Mhagama alisema kupitia timu ya wataalamu wa wizara yake wamefanyika utafiti kujua aina ya udongo uliopo kwenye kila kanda na pembejeo zinazoweza kutumika katika kanda hizo sambamba na kuzitaka taasisi za kifedha kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima, wafugaji na wavuvi kulingana na uwezo wao na kuimarisha matumizi sahihi ya maji katika kuboresha miundombinu ya umwagiliaji mashambani na maeneo ya kulishia mifugo.

## NMB yakusanya bil.83/- mauzo hatifungani

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imekusanya Sh. bilioni 83.3 kutokana na mauzo ya awamu ya tatu ya hatifungani yaliyofanyika kati ya Juni 10 na Julai 8, mwaka huu.

Akitoa taarifa juu ya mauzo hayo jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Fedha wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema katika hatifungani hiyo, benki ilitarajia kukusanya Sh. billioni 25, lakini wamevuka lengo kwa asilimia 333.

"Haya ni mafanikio makubwa na hii inaonyesha kuwa Watanzania wana imani kubwa na benki yao na kwamba wanajua katika kuwekeza kupitia NMB fedha zao zinakuwa katika mikono salama," alisema Zaipuna.

Sambamba na kuvuka lengo hilo, Zaipuna alisema benki imepata idhini kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ya kupokea maombi yote ya mauzo ya hatifungani hizo .

Kutokana na idhini hiyo, mkuu huyo alisema wateja walioshiriki katika ununuzi wa hatifungani hizo, wameshaarifiwa kuwasilisha maombi yao na kwamba leo wataorodheshwa katika masoko ya mitaji.

Pia alisema wateja ambao hawakupata nafasi, watanunua hatifungani hizo katika masoko ya mitaji yaliyoorodheshwa na kwamba vyeti vya umiliki vitatolewa kwa wahusika baada ya mwezi mmoja kuanzia sasa.

Zaipuna alisema kutokana na mafanikio hayo makubwa, benki sasa inaweza kupata mikopo zaidi kwa kuwa hatifungani hizo ni dhamana kubwa kwa NMB. Pia alisema makusanyo hayo yataiwezesha benki kutoa mikopo zaidi kwa gharama nafuu.

Naye Mkuu wa Wateja Wadogo na wa Kati wa NMB, Filbert Mponzi, alisema mafanikio hayo katika mauzo ya hatifungani yametokana na elimu waliyoitoa kwa Watanzania, hivyo kujitokeza kwa wingi.

"Watanzania wengi wanaichukulia NBM kuwa ni benki yao kwa sababu mtandao wake umetapakaa nchi nzima hadi vijijini ndiyo maana watu mpaka wa vijijini walishiriki katika mchakato huu wa ununuzi," alisema Mponzi.

Aliongeza kuwa mauzo hayo ambayo yamevuka lengo kwa kiasi kikubwa, yametoa taswira pana zaidi kwa benki katika kuboresha huduma zake na maendeleo kwa ujumla.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MCHANGANYIKO

**KISIMA CHA BEI NAFUU: kilichokamilika tunakuchimbia** kisima na kukuwekea pampu,tutaacha maji yanatoka kisimani kwako tupigie 0714564651/0752737534.

**TUNASAFISHA VISIMA:** virefu na vifupi kwa kutumia machine za kisasa na tunapima ubora wa maji. gharama zetu nafuu,simu:0623528465/0655752175

**NJANI PROPERTY COMPANY (NPC):** tunauza na kununua nyumba,viwanja,mashamba,lete mali kwetu ununue/uuze kwa haraka simu:0714564651/0658910584.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA**


### KUPOTEA KWA CHETI




115356702

**Solomon Mwambingu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye **index namba S0496-388** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1992, katika shule ya Sekondari Jitegemee na cheti chja kidato cha sita chenye **index namba S0119-0582** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1995 katika Shule ya Sekondari Kibaha.

Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi. Polisi Taarifa: **PWA/CHA/RB/178186/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI



11555702

**Edward Essau Lukamya** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1530-0045** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014, katika shule ya sekondari St. Rufino and Ronaldo Agr.

**Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: DAR/KIG/RB/176049/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI




115355802

**Rosemary W. Shayo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1487/0089** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016, katika shule ya Sekondari Boko.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: KMB/RB/8428/19**

### CHETI KIMEPOTEA




115356102

**LAWI JOEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0339-0064** kilichotolewa na **OMUMWANI SEKONDARI** mwaka 1995.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MUS/RB/5506/2019.**

### KUPOTEA KWA CHETI




115355602

**Lilian Emmanuel Hongoli** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4119/009 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2016, katika shule ya Sekondari Consolata.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote Cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/STA/RB/177545/2019**

### CHETI KIMEPOTEA



115356502

**FRANK KUSEKWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0938/0139** kilichotolewa na MBEZI BEACH SEKONDARI mwaka 2005.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: CD/IR/3381/2015.**

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**TIMOTHY MUSA CHIBOTI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina yenye namba za usajili **MC 606 AAD** rangi ya BLUE. Chassis namba **LBR5PJB50B9005079** Engine namba. 11921645.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/169604/2019**

215356002

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**MAOMBI NA: 116 YA MWAKA 2018**
**CRDB BANK PLC.....................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**MSAFIRI MACHUZA SINGILA.......WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA MSAFIRI MACHZA SINGILA**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 12/08/2019 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi. Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 22 Mwezi Julai, 2019.

115356302

### Eneo la biashara (Yard Plot) mita za Mraba 2,723 linauzwa.

Eneo (yard) Lina hati miliki, Kuna maji na umeme pia.

Eneo lipo Msamvu Morogoro, kandokando ya barabara ya Iringa, karibu na BM Garage

Eneo linafaa kwa matumizi ya kiwanda, maegesho ya malori, Hoteli, Hostel, maofisi, maghala n.k,

215338701

**Kwa mawasiliano:**
**godlisten.minja@greenresources.no**
**+255 714 432 979**


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# BARCELONA YASHINDWA KUMUUZA COUTINHO




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA haijapokea ofa yoyote kwa ajili ya kumuuza mchezaji wao waliyemnunua kwa bei iliyoweka rekodi, Philippe Coutinho licha ya kubainisha kwamba inataka kuachana nae kipindi hili cha majira ya joto, kwa mujibu wa Daily Mail.

Coutinho amekuwa na wakati mgumu tangu alivyotua hapo Barca akitokea Liverpool Januari mwaka 2018, ambapo aliweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 145.

Licha ya mchezaji huyo kuonyesha kiwango kizuri wakati akiichezea Brazil kwenye michuano ya mataifa ya Afrika, Copa America, lakini hakuna ofa yoyote iliyopokelewa mezani kwa Barca hadi sasa.

Miamba hao wa soka la Hispania hawakutamka hadharani kwamba wanataka kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ingawa iliripotiwa kuwa wanataka kuachana nae kwa kushindwa kufikia malengo yao.

Hata hivyo, Barcelona wanaweza kumtumia Coutinho katika harakati za kutaka kukamilisha mpango wa kurudisha Neymar kutoka PSG ya Ufaransa.

Ingawa wawakilishi wa Coutinho wamebainisha wazi kwamba, mchezaji huyo anataka kuondoka hapo Barca, lakini hadi sasa hakuna ofa iliyotolewa.

Aidha ripoti zaidi zimebainisha kwamba Coutinho anaweza kuwa mbadala wa kumpata Neymar kwenye mpango ambao pia unaweza kumhusisha Ousmane Dembele.

# Salah, Firmino kuanza dhidi ya Man City

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp anafikiria kuwaanzisha kwa pamoja, Mohamed Salah na Roberto Firmino dhidi ya Manchester City kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii, baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye maandalizi ya msimu mpya.

Liverpool ilikuwa na wakati mgumu wa kupata matokeo kwenye mechi zake za maandalizi ya msimu mpya, lakini baada ya vichapo vitatu, walibadilika na kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Lyon nchini Uswisi, shukrani kwa mabao ya Salah na Firmino walioongoza safu ya ushambuliaji.

Wachezaji hao walirudi kwenye mazoezi Jumatatu baada ya mapumziko ya kipindi cha majira ya joto na walijumuika kwenye mazoezi kwenye kambi ya Liverpool iliyoko katika mji wa Evian nchini Ufaransa wakijiandaa kwa mchezo wa Ngao ya Jamii ambao ni wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya England.

Firmino alicheza dakika 30 za mwanzo na alifunga akiisawazishia Liverpool, huku pia Salah naye akifunga kwenye mchezo huo.


Alitolewa kipindi cha pili kwenye mchezo ambao Liverpool ilitumia wachezaji wake 27 kwenye mchezo huo.

"Tutawaangalia namna watakavyocheza," alisema Klopp.

"Kwa sasa mazoezi yanaelekea mwisho. Tunahitaji kujiandaa na mchezo wetu unaokuja. Manchester City inakuwa tofauti katika kila mchezo utakaocheza nao.

"Lazima tujiandae kikamilifu, naamini watacheza vizuri, Salah na Firmino wataanza kwenye mchezo dhidi ya Manchester City."




# Unai: Nataka Koscielny abaki Arsenal

**LONDON,** England

UNAI Emery ana matumaini ya kumshawishi beki wake wa kati anayetaka kuondoka, Laurent Koscielny kubakia hapo Arsenal.

Naghodha wa Arsenal, Koscielny alikataa kusafiri na timu hiyo kwenda kucheza mechi nne za maandalizi ya msimu mpya nchini Marekani baada ya maombi yake ya kutaka kukatisha mkataba wake ili aruhusiwe kwenda kujiunga na klabu nyingine kukataliwa.

Na sasa anataka kumaliza muda wake wa miaka tisa wa kucheza hapo Arsenal, huku akionyesha nia ya kutaka kurudi nyumbani kwao nchini Ufaransa.

Lakini Emery sasa anajipanga kumbakisha beki huyo mzoefu kipindi hiki cha majira ya joto, kwani safu yake ya ulinzi haiko vizuri hapo kwenye dimba la Emirates.

Baada ya mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya Angers ya Ufaransa, Emery alisema: "Koscielny ni mchezaji muhimu kwa upande wetu bado sijapoteza matumaini ya kumpoteza na naamini ataendelea kubakia na sisi msimu ujao.

"Nazungumza nae mara kwa mara na najaribu kumshawishi kubakia na sisi. Lakini kwa sasa mpango wake ni kutaka kuondoka na hilo linatufanya sisi kufanye mabadiliko kwenye safu ya mabeki wa kati."




# NEYMAR AIAMBIA PSG HATAICHEZEA TENA

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR ameiambia Paris Saint-Germain kwamba, hataichezea tena timu hiyo wakati akijaribu kulazimisha uhamisho wa kwenda Barcelona, kwa mujibu wa Daily Mail.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kurudi kule Nou Camp, lakini klabu hiyo imemwambia hatakwenda popote kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili.

Kwa mujibu wa gazeti la Hispania, SPORT, Neymar anajaribu kulazimisha kuondoka na hana mpango wa kukubaliana na matakwa yao.

Katika ukurasa wa kwanza wa gazeti la SPORT la jana Alhamisi ulisomeka: "Neymar ameweka wazi kwamba hataki tena kuvaa jezi ya PSG katika mechi yoyote kwa sababu anataka kuondoka."

SPORT pia Jumatano liliripoti kwamba, PSG ina matumaini nyota huyo wa Brazil atakubali kubakia hapo na atakubali kubakia kwa msimu mmoja zaidi.

Hata hivyo, Neymar anataka kuondoka klabuni na ameamua kufanya mazoezi ya peke yake wakati PSG ikiwa kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya nchini China.

Bado hajacheza mchezo wowote tangu alivyorudi kutoka likizo ya kipindi cha majira ya joto na inaonekana kwamba ataendelea kuweka mgomo ili kulazimisha uhamisho wake kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

Hadi sasa, Barcelona imewapa ofa ya fedha na wachezaji wawili kwa ajili ya kumchukua Neymar, lakini mabingwa hao wa Ufaransa wanataka walipwe pauni milioni 165 ili kumwachia nyota huyo wa zamani wa Santos.

Mmiliki wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, anapanga kukutana na Rais wa Barcelona, Josep Bartomeu, katika mkutano wa chama cha klabu za Ulaya Agosti 15 mwaka huu.

# Napoli yamfungia kazi Zaha

**ROME,** Italia

NAPOLI inapanga kutoa ofa ya pauni milioni 60 kwa klabu ya Crystal Palace kwa ajili ya kumsajili winga wake, Wilfried Zaha baada ya kumkosa Nicolas Pepe ambaye amesajiliwa Arsenal.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, sasa imeamua kumfungia kazi mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast baada ya kumkosa Pepe.

Bosi wa Napoli, Carlo Ancelotti sasa amehamishia nguzu zake kwa Zaha mwenye umri 26 kwa ajili ya kuimarisha timu yake.

Arsenal baada ya kumsajili Pepe sasa nafasi ya kuendelea kumfukuzia Zaha haipo tena baada ya ofa yao ya kwanza ya pauni milioni 40 kukataliwa na Palace.

Everton nayo ilijaribu kumsajili Zaha, lakini ofa yao ya pauni milioni 55 ilikataliwa na Eagles hao.

Lakini Napoli sasa wanaandaa ofa ya pauni milioni 60 kwa ajili ya kumsajili Zaha na wataituma mapema wiki hii.

Zaha mwenyewe ameshaiambia Palace kwamba anataka kuondoka hapo kwenye dimba la Selhurst Park kipindi hiki cha majira ya joto akiwa na nia ya kwenda kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo Napoli wamefuzu.




# Cavani aikataa Inter Milan




**MILAN,** Italia

INTER Milan imejikuta kwenye wakati mgumu kuwashawishi washambuliaji wapya kujiunga nao msimu huu, baada ya Ednson Cavani kukataa kutua kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, kwa mujibu wa La Gazzetta dello Sport.

Hadi sasa Inter imeshindwa kumsajili Romelu Lukaku, na sasa mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Edinson Cavani naye amekataa ofa ya kujiunga nao.

Mshambuliaji wa Roma, Edin Dzeko ambaye wanamtaka pia, lakini usajili wa mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City unaonekana kukwama.

Kocha mpya wa Inter, Antonio Conte pia ana furaha kumuuza mshambuliaji, Mauro Icardi ili kupata fedha za kununua fowadi mwingine.

Cavani ameamua kubakia Paris msimu huu, huku mkataba wake ukimalizika kipindi cha majira ya joto kijacho, ili kumfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kuamua hatima yake.

Wakati Icardi akielekea Juventus, miamba hao wa Serie A wanaonekana pia wakaribia kumchukua Lukaku katika usajili ambao utamhusisha Paulo Dybala kwenda Manchester United.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




## MOURINHO AMCHAMBULIA LAMPARD ZOUMA, ABRAHAM

Chelsea ilikosolewa sana kwa idadi kubwa ya wachezaji zaidi ya 30 wanaocheza nje kwa mkopo...

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amemwambia Frank Lampard awatumie Kurt Zouma na Tammy Abraham wakati huu Chelsea ikitumikia kifungo cha kusajili nyota wapya.

**'Blues' kwa sasa hawawezi kusainisha mchezaji mpya hadi dirisha lijalo la Januari kufuatia Fifa kuikuta na hatia ya kuvunja kanuni ya usajili ya kusajili mchezaji wa chini ya miaka 18 (U-18). Hata hivyo, timu hiyo ya Ligi Kuu England imekata rufaa kuhusu uamuzi huo.**

Christian Pulisic alikamilisha usajili wake kutoka Borussia Dortmund ambao makubaliano yalifanyika tangu Januari, wakati Mateo Kovacic amekamilisha usajili wake wa mkopo kutoka Real Madrid kuwa wa jumla, lakini kocha mpya Lampard vinginevyo hakuweza kuingiza sura mpya katika dirisha hili.

Wakati huu Eden Hazard akiwa ameelekea Madrid, Gonzalo Higuain akirudi Juventus na beki mzoefu Gary Cahill akisepa, Lampard inawezekana sasa akalazimika kutumia vipaji vya makinda katika msimu ujao.

Mourinho, ambaye alitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England akiwa Stamford Bridge wakati Lampard akiwa mchezaji, amesema kuna vipaji vingi katika hazina ya kiungo wake huyo wa zamani.

"Nadhani kila kocha anapenda kuchezesha makinda kutoka katika akademi yake," aliiambia Sky Sports. "Swali ni: bidhaa gani kutoka katika akademi? Unawezaje kufanya nao na kuboresha?

"Nadhani Chelsea ni klabu ya kipekee katika hilo. Ninaweza kutoa mfano: Chelsea inahitaji beki wa kati- Kurt Zouma! uhitaji kununua, uhitaji kutumia fedha. Zouma!

"Ni bingwa wa England, ameichezea Chelsea, ameichezea Stoke [City] katika Ligi Kuu, ameichezea Everton kwenye Ligi Kuu, ameichezea Ufaransa. Ni wachezaji wako, ametolewa kwa mkopo, wapi utakapokwenda kununua mchezaji mzuri zaidi yake? Tayari unaye yeye.

"Unahitaji mshambuliaji kinda - Tammy Abraham! Ni wakwako. Anaijua klabu. Amekulia klabuni, amesomea klabuni. Anacheza kwa mkopo, tayari amecheza baadhi ya mechi za Ligi Kuu England, anacheza Daraja la Kwanza ('Championship') lakini Championship katika daraja la juu akiwa na majukumu ya kucheza klabu kubwa kama Aston Villa. Yupo tayari.

"Je, unahitaji kununua mshambuliaji kinda wa kati? Hapana! Na Chelsea ilikosolewa mara nyingi kwa idadi kubwa ya wachezaji wanaocheza nje kwa mkopo, zaidi ya wachezaji 30, wachezaji 40, lakini sasa wakati umefika na wanajibu ambalo hakuna yeyote anayeweza kuwa nalo.

"Tatizo pekee kwao ni kwamba wamepoteza wachezaji maarufu. Eden Hazard ni mchezaji wa kipekee kwa Chelsea na wamempoteza, mbali ya hilo sioni tatizo lolote kwao."

## ZISIKUPITE

### DYBALA ATAKA 350,000 UTD

MANCHESTER United bado inazingatia mbadala wao wa kumfuata Paulo Dybala, 25, wakati huu mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina akijadili na Juventus kuhusu mustakabali wake wiki hii na akielezwa ameitaka klabu hiyo kumlipa pauni milioni 350,000 ili kujiunga nayo. ***(Manchester Evening News and Mail)***

### PEPE MALI YA ARSENAL- LILLE

RAIS wa Lille, Gerard Lopez amethibitisha winga Muivory Coast Nicolas Pepe, 24, atauzwa Arsenal kwa euro milioni 80 (pauni milioni 73). ***(RMC Sport - in French)***

### NAPOLI KUMGEUKIA ZAHA

NAPOLI inajiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 60 kwa winga wa Crystal Palace, Muivory Coast Wilfried Zaha baada ya kumkosa Nicolas Pepe. ***(Mail)***

### YASUBIRI OFA KWA COUTINHO

BARCELONA inataka kumuuza kiungo Philippe Coutinho, lakini bado haijapokea ofa kwa Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(ESPN)***

### ARSENAL YAMTAKA RUGANI

ARSENAL imetoa ofa ya kuipata huduma ya beki wa kati wa Juventus na Italia, Daniele Rugani, kwa mkopo wa misimu miwili. ***(Gazzetta dello Sport, via Sun)***

### YAJIPANGA KWA GBAMIN

EVERTON inafanyia kazi mpango wa kuipata saini ya kiungo wa Mainz na Ivory Coast, Jean-Philippe Gbamin, 23, hapo Goodison Park. ***(Liverpool Echo)***

### BAYERN KUIANGUKIA MAN CITY

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic amesema Manchester City inastahili kuombwa radhi baada ya kocha Niko Kovac kueleza kwamba miamba hiyo ya Bundesliga inajiandaa kumsainisha mkataba winga Mjerumani Leroy Sane, 23. ***(Sport Bild - in German)***

### KOSCIELNY AKOMALIA KUSEPA

NAHODHA Laurent Koscielny, 33, bado anataka kuondoka Arsenal majira haya ya joto licha ya mazungumzo yanayoendelea kati ya beki huyo na klabu. ***(Independent)***

### MALCOLM KUUZWA ZENIT

ZENIT St Petersburg inajiandaa kumsainisha mkataba winga wa Barcelona, Malcolm, 22, baada ya klabu hizo mbili kukubaliana ada ya uhamisho ya takriban pauni milioni 36.5. ***(Goal)***

### ARSENAL YAISUBIRI OFA

ARSENAL inajiandaa kumruhusu beki Mjerumani Shkodran Mustafi kuondoka majira haya ya joto, lakini Roma bado haijatoa ofa licha ya kuhusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Romanews, via Star)***

### LIHADJI AWINDWA, UTD, BARCA

MANCHESTER United ipo tayari kutoa upinzani kwa Barcelona katika mbio za kuipata saini ya mshambuliaji wa Marseille, Mfaransa Isaac Lihadji, 17, majira haya ya joto. ***(La Provence, via Mail)***

HABARI MICHEZO

# NDAYIRAGIJE AGEUKIA WACHANA NYAVU STARS

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya mashabiki kuhofia Taifa Stars kuweza kupata matokeo ugenini nchini Kenya dhidi ya Harambee Stars, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo ya Taifa ya Tanzania, Mrundi Etienne Ndayiragije, amewatoa hofu Watanzania kwa kueleza kuwa ana imani kubwa na kikosi chake kuelekea mchezo huo wa marudiano na kwamba tatizo la kukosa na nyavu amekuwa akilifanyia kazi.

Taifa Stars itarudiana na Harambee Stars Nairobi, Kenya Jumapili na mshindi wa mechi hiyo ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), atakutana na mshindi kati ya Burundi ama Sudan Kusini.

Katika mechi ya awali iliyochezwa Uwanja wa Taifa Jumapili iliyopita timu hizo zilitoka sare tasa wakati Burundi ilianza vema kwa ushindi wa mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Sudan Kusini.

**Hata hivyo, Stars inahitaji ushindi wowote ama sare ya mabao yoyote ili kusonga mbele kufuatia timu hizo kutoka sare tasa hapa nyumbani.**

Ndayiragije jana alimwambia mwandishi wetu kuwa kutokana na uwezo wa wachezaji wake hana wasiwasi kwani wamekuwa wakizidi kuimarika kila iitwapo leo na wanatambua kwamba wana kazi kubwa ya kufanya vizuri nchini Kenya hasa baada ya mchezo wa kwanza kutopata matokeo.

"Tatizo letu kubwa lilikuwa ni umaliziaji wa nafasi ambazo tumezitengeneza jambo ambalo tumelifanyia kazi, hivyo tunakwenda ugenini tukiwa na imani ya kushinda, mashabiki watupe sapoti," alisema.

Katika hatua nyingine kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Ibrahim Ajibu huenda akaukosa mchezo huo kutokana na kuendelea kuuguza majeraha aliyoyapata katika mechi ya awali Uwanja wa Taifa.

Kaimu Kocha Msaidizi wa kikosi hicho, Juma Mgunda, alinukuliwa jana jijini Dar es Salaam akisema kuwa bado hajawa fiti na kwamba daktari anaendelea kufuatia afya yake.

"Wachezaji wengine wote wapo fiti isipokuwa Ajibu bado daktari anaendelea kufuatilia majeraha yake aliyoyapata kwenye mechi ya awali," alisema.



Mshambuliaji mpya wa Real Madrid, Eden Hazard (katikati), akiwa katika harakati za kuwania kumiliki mpira dhidi ya kiungo wa Tottenham Hotspur, Harry Winks kwenye mchezo wa Kombe la Audi uliopigwa Uwanja wa Allianz Arena mjini Munich, Ujerumani Jumatatu wiki hii. Spurs ilishinda 1-0 kupitia kwa Harry Kane. **PICHA MTANDAO**

# TFF yafunguka kukamilika usajili

Na Shufaa Lyimo

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeeleza kuridhishwa na utekelezaji wa klabu katika suala zima la kukamilisha majina ya wachezaji waliowasajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019-2020.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Kamati ya Usajili TFF, Baraka Kizuguto, alisema klabu zote zimekamilisha majina ya wachezaji wao katika muda uliopangwa.

"Jana (juzi) klabu zote zimefanikiwa kukamilisha usajili kama ilivyopangwa wamefuata utaratibu tuliowawekea," alisema Kizuguto.

Aliongeza kuwa wanashukuru wamemaliza salama usajili huo na kudai baada ya kamati husika kupitia usajili huo watatangaza kila kinachoendelea.

"Baada ya kamati husika kupitia usajili huo tutatangaza kwa wadau wa soka hapa nchini wajue kinachoendelea," alisema.

## Balozi Seif Iddi awafunda ZFF

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limetakiwa kusimamia vema sheria pamoja na kanuni ilizojiwekea za kuendesha mpira wa miguu ili kuepuka migogoro inayoweza kushusha kiwango cha mchezo huo nchini, imeelezwa.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ndiye aliyetoa ushauri huo kwa uongozi mpya wa ZFF na kufafanua kuwa wapo baadhi ya viongozi waliowahi kushika madaraka ndani ya kilichokuwa Chama cha Soka Zanzibar (ZFA) kwa sasa ZFF, lakini walishindwa kuzitekeleza sheria hizo na hatimaye kufikia hatua ya kupelekana mahakamani jambo ambalo linakwenda kinyume cha uendeshaji wa vyama vinavyosimamia na kuendesha soka kitaifa na kimataifa.

Akizungumza na uongozi mpya wa ZFF ofisini kwake Vuga jana, Balozi Seif alisema vurugu zilizokuwa zikishuhudiwa kutokea ndani ya uongozi wa iliyokuwa ZFA kipindi cha nyuma zilichangia kudorora kwa kiwango cha soka Zanzibar.

Balozi Seif alisema uongozi wa sasa hauna budi kuelewa kwamba wao ndio watakaobeba lawama zitakazotolewa na wapenzi wa soka nchini endapo kiwango cha soka kitaonekana kushuka miongoni. Aidha, aliupongeza uongozi huo wa ZFF, kwa kuchaguliwa kuongoza shirikisho hilo na kueleza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshaamua kujikita katika ujenzi wa viwanja vya michezo katika kila wilaya ya Unguja na Pemba ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa ilani yao ya uchaguzi.

Mapema Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu, alisema shirikisho hilo limejipanga kuendesha soka kwa kuzingatia sheria na kanuni za Fifa na Caf.

## ZFF yasogeza mbele usajili

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limeongeza muda wa usajili wa wachezaji kuelekea msimu mpya ambapo sasa dirisha hilo litafungwa rasmi Agosti 8, mwaka huu.

Dirisha la usajili Zanzibar lilitarajiwa kufungwa rasmi Julai 31, mwaka huu, lakini sasa limesogezwa mbele kwa siku nane zaidi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na jana kwa vyombo vya habari na Ofisa Habari wa ZFF, Adam Natepe, ilieleza kuwa shirikisho hilo limeongeza muda kutokana na kujitokeza mapungufu mbalimbali katika kipindi hiki cha usajili.

Ilieleza kuwa mapungufu hayo ni pamoja na kuchelewa kuchukuliwa fomu za usajili kwa wakati hasa kutoka kisiwani Pemba.

Aidha, taarifa hiyo imezitaka klabu kutumia fursa hiyo kufanya usajili kwani ZFF haitaongeza muda mwingine.

# Michezo

Ijumaa Agosti 2, 2019

Nipashe




Neymar aiambia PSG hataichezea tena UKURASA 29

NDOO...




Kiungo wa Tottenham, Moussa Cissoko, akinyanyua kombe juu akiwa na wachezaji wenzake baada ya kukabidhiwa kufuatia kutwaa ubingwa wa Audi Cup kwa kuifunga Bayern Munich kwa penalti 6-5 baada ya mechi kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 katika Uwanja wa Allianz Arena, Ujerumani juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Simba sasa kidigitali

**Na Shufaa Lyimo**

## ●●● Mabilioni zaidi kumiminika ikilenga mashabiki na wanachama milioni 10, yaingia mkataba na Benki ya...

KLABU ya Simba imezidi kujitanua ikielekea kujiendesha kidigitali zaidi baada ya jana kuingia mkataba na Benki ya Equity wa kutengeneza kadi za kielektroniki kwa ajili ya wanachama na mashabiki ili kuiwezesha kukusanya ada na mapato mbalimbali kisasa ikiwamo viingilio vya uwanjani, lakini pia kupata takwimu sahihi za mashabiki wao.

**Akizungumza na waandishi wa habari jana katika hafla hiyo fupi ya kuingia mkataba huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema, mkataba huo utaleta mafanikio makubwa ndani ya Simba na utakuwa endelevu.**

Akielezea faida kubwa kwa klabu katika kadi hizo alisema ni makato yanayopatikana wakati wa kufungua akaunti ambapo jumla itagharimu Sh. 14,500, kukusanya ada kisasa na mara moja kwa mwaka, na kupata takwimu sahihi za mashabiki iwapo kila shabiki atafungua akaunti.

Alisema kadi hizo zitatumiwa na wanachama na mashabiki kuweka akiba ya pesa na kutoa pindi wanapotaka kutumia, lakini kulipa ada ya kila mwaka, kununua tiketi za kuingia uwanjani, na kupata punguzo la mpaka asilimia 10 kwenye maduka makubwa ambayo watashirikiana nayo.

Alisema kadi hizo zitaanza kutolewa Septemba Mosi, mwaka huu, kwa kuwabadilishia kadi wanachama wa sasa na baadaye mchakato huo utaendelea kwa wanachama wapya na mashabiki.

Hata hivyo, Magori alisema kuwa lengo lingine la kuingia mkataba na benki hiyo, ili kuwasaidia kuwaweka pamoja wanachama na mashabiki kuwa familia moja.

"Tunashukuru Equity Benki kukubali kushirikiana na sisi, tunaamini tutapata mafanikio makubwa kupitia mfumo huu," alisema Magori.

Aidha, aliongeza kuwa, mfumo huu utakuwa na kadi za aina mbili ambazo ni za wanachama na mashabiki nchi nzima.

"Kwa upande wa Simba Card, wataanza kwa wanachama waliopo kwanza watabadilishiwa kadi zao na kupewa utaratibu wa benki vile vile zitawasaidia kuweka akiba pamoja na kununua tiketi za kuingilia uwanjani, taratibu zote tutazianza Septemba Mosi," alisema Magori.

Kuhusu utaratibu huo, Magoro alisema klabu itapata pesa za kutosha kutokana na michango itakayokuwa inapata.

Kwa upande wa kadi za mashabiki alisema hii itamhusu mtu yeyote ambaye ni shabiki wa Simba.

"Hii kadi ya shabiki muda wowote anaruhusiwa kuchukua kadi mradi awe Mwanasimba na kila mwezi anatakiwa alipie Sh. 1000," alisema Mtendaji huyo.

Alisema kadi zote zitakuwa na mfumo mmoja wa kutumia kama zilivyo kadi za ATM na kudai hii itazidisha mafanikio kwa upande wao. Kwa upande wa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Robert Kiboti, alisema amefurahi kusaini mkataba na Simba na kudai ni miongoni mwa timu kubwa hapa nchini inayopata mafanikio makubwa kisoka.

"Nimefurahi kuungana na Simba kwa sababu ni moja kati ya klabu yenye mafanikio makubwa hapa nchini," alisema Robert.

Hata hivyo, alisema mkataba huo utawawezesha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kunufaika kipesa pamoja na kupata mapato kwa njia ya kiteknolojia.

"Tutahakikisha mapato yanafanyika kiteknolojia na ninaamini kwa hiki tulichokifanya tutanufaisha mashabiki zaidi ya milioni 10,"alisema Mtendaji huyo.

Aidha, alisema watazidi kuboresha maisha ya kila mwanachama na hata kwa wale wenye maisha ya chini ili kila mmoja aweze kupata kadi hizo. Vile vile alisema kila mwanachama atalipia kadi hizo kiasi cha shilingi 10,000 na shilingi 1000 kila mwezi ambapo jumla kila mwaka atalipa shilingi 14,500.

Wakati huo huo wachezaji wa klabu hiyo leo watamtembelea mdhamini wao SportPesa pamoja na Kampuni ya Azam TV.

Akizungumza jana, Msemaji wa timu hiyo, Haji Manara alisema hiyo ni mwendelezo wa wiki yao ambayo ina mambo makubwa.

"Kesho asubuhi (leo), timu yetu itamtembelea mdhamini wetu pamoja na kwenda Kituo cha Azam TV huu ni mwendelezo wa wiki yetu," alisema Manara.

Pia alisema leo na kesho wanachama wote wa matawi ya Mbagala na Kituo cha Mabasi Ubungo, watashirikiana kwa pamoja kuchangia damu na wachezaji watakwenda Hospitali ya Ocean Road kujulia hali wagonjwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002